

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 17 Desemba, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka 2013.

MHE. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI):

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka 2013.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 120

Kuleta Walimu na Kujenga Nyumba Zao

MHE. MWIGULU L. N. MADELU (K.n.y. MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA) aliuliza:-

Kwa kutumia jitihada binafsi na Mfuko wa Jimbo, Mbunge wa Jimbo la Nzega ameanzisha ujenzi wa shule tatu za Kidato cha Tano na Sita:-

(a) Je, ni lini Serikali itaunga mkono jitihada hizi kwa kujenga nyumba za Walimu kwenye shule hizo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuleta Walimu na kusajili shule hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, kwa jitihada anazozifanya kuboresha utoaji wa elimu nchini. Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada hizi kupitia Mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari na kutenga fedha kila mwaka kupitia Mpango wa Bajeti za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2010 na 2013, kupitia Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II), Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 11.9 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ujezi wa nyumba za walimu na Halmashauri ya Wilaya ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Nzega ilipatiwa shilingi milioni 72 zilizoufaisha Shule za Sekondari za Budushi, Undomo, Shigamba na Milambo Itobo. Kupitia Mfumo wa kugawa ruzuku ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGCDG), mwaka 2013/2014 Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imepokea shilingi milioni 420 na kati ya hizo shilingi milioni 105 zimepangwa kupelekwa katika ujenzi wa nyumba za walimu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Sekondari Puge na Chifu Ngelengi zinazotarajiwa kuwa za Kidato cha Tano hazijakamilisha vigezo vya kuweza kusajiliwa na kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano kwa kukosa madarasa ya kutosha, vyoo, mabweni, maabara na samani. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imeshauriwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani na kuweka kipaumbele kupitia bajeti za Halmashauri ili kukamilisha mahitaji muhimu katika shule hizi. Aidha, napenda niwahakikishie Wananchi wa Nzega kuwa, mara vigezo vyote vitakapokamilika ikiwemo kuwa na miundombinu muhimu, Serikali itakuwa tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge katika kuharakisha usajili wa shule hizo na kuzipatia walimu wa kutosha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwigulu Nchemba!

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini niseme kwamba, kuna maeneo mengi sana ambayo jitihada za Wananchi zimefikia kiwango ambacho zikiungwa mkono shule zile zingesajiliwa na zingeanza kutumika mapema zaidi. Yapo maeneo mengi ambako Wananchi wamejitahidi na wameshajenga kwa kiwango hicho, lakini kutokana na ukomo wa bajeti wa Halmashauri, shule hizo zinachukua muda kukamilika kwa sababu Wananchi walewale wanatakiwa washughulike kwenye sekta zingine pia.

Je, ni kwa nini basi Serikali isitoe kipaumbele kwa maeneo ambayo Wananchi wameshaonesha njia kwa kiwango hicho kwa kutenga bajeti maalum ya kuunga

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MWIGULU L. N. MADELU]

mkono maeneo ambayo yameshaonesha jitihada badala ya kuziachia tu Halmashauri na kusababisha majengo ambayo Wananchi wametumia jitihada kubwa kuyajenga yabaki bila kutumika kwa kipindi kirefu kwa sababu wanasubiri kujikusanya upya na kutengeneza maeneo hayo kama ilivyo eneo la Kichangani pale Misigiri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi na Mbunge wa Iramba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mwingulu Nchemba, anachosema ni kweli kama kuna mahali na ndivyo ilivyo katika nchi yetu kwamba Wananchi wamejitoa, wametoa nguvu zao, wamefanya kazi, unachotegemea Halmashauri hizi zitaungwa mkono na Serikali na ndivyo vitu ambavyo nimekuwa navieleza hapa. Hili eneo analolisema sijalipata vizuri kwamba liko Iramba au kule Nzega, lakini haitaondoa maudhui ya jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Halmashauri ya Nzega tunayoizungumza ukiangalia katika mapato yake, fedha zimekwenda kule na nimesema katika MMES II shilingi milioni 105 zimeelekezwa katika eneo hilo na katika *Local Government Capital Development Grant* wamepelekewa fedha pia shilingi milioni 72, lakini hazikuenda sasa katika shule hizi ambazo Dkt. Hamisi Kigwangalla anazizungumzia.

Pia nataka nitoe taarifa hapa kwamba, kupitia mrabaha ambao umetokana na machimbo, Halmashauri hii imepata shilingi bilioni 2.3, sikumbuki vizuri ile *figure* lakini *at least* najua kuna fedha zimepatikana pale na hizi ni *own source* ambazo kama tunazungumza habari ya elimu, duniani kote sasa hivi *investment* kubwa ya Mataifa makubwa yote inapelekwa katika kitu kinachoitwa elimu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Maoni yangu na ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kwamba, hawa wakae wafikirie jinsi ambavyo wanaweza wakatumia sehemu fulani ya mrabaha ule ikasaidia katika jambo lile wakati Serikali tukiendelea na jitihada hizi za kusaidia kama anavyoshauri Mheshimiwa Nchemba.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali lingine, Mheshimiwa Felix Mkosamali!

Na. 121

Wabunge Kualikwa Kwenye Vikao vya Halmashauri

MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. FELIX F. MKOSAMALI) aliuliza:-

Baadhi ya Wabunge wamekuwa hawapati taarifa za kila siku za Halmashauri ikiwa ni pamoja na kutoalikwa kwenye baadhi ya vikao hata wakiwa Majimboni:-

(a) Je, kwa nini Makatibu wa Wabunge wasiwe wanaalikwa katika vikao ikiwa Wabunge hawapo Majimboni na walipwe posho?

(b) Je, kwa nini Serikali isiagize Halmashauri zote nchini kufanya hivyo ili Wabunge wapate taarifa za Halmashauri zao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zote nchini huendesha vikao vyake kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu zilizotungwa chini ya Kifungu cha 70 cha Sheria ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na Kifungu cha 42 (1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zote huandaa ratiba ya vikao vya Mabaraza kwa mwaka mzima na ratiba hiyo hukabidhiwa Wajumbe wote. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) imefanya mapitio upya ya Kanuni za Kudumu za Halmashauri ambapo imeongeza Kifungu cha 6 (ii) na 7 (ii) ambacho kinatamka kuwa, Mikutano yote ya Baraza la Madiwani itapangwa na Baraza la Madiwani kwa kuzingatia Vikao vya Bunge ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuhudhuria Mikutano ya Baraza la Madiwani. Endapo italizimika kuitishwa kwa Mikutano hiyo ya Baraza wakati Vikao vya Bunge vinaendelea, Mkurugenzi Mtendaji atamjulisha au atawajulisha Wabunge husika kuhusu kikao hicho ili waweze kuhudhuria.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zinaelekeza kwamba, Wajumbe wa Vikao vya Halmashauri ni Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waheshimiwa Madiwani katika maeneo yao. Hata hivyo, Makatibu wa Wabunge hawazuliwi kuhudhuria Vikao vya Mabaraza ya Madiwani, ambavyo vinaruhusu Wananchi wote kuhudhuria ingawa hawatapewa fursa ya kuhoji jambo lolote wala kulipwa posho kwa kuwa wao siyo Wajumbe. Kwa hiyo, itakuwa ni vigumu kuziagiza Halmashauri kuwaalika Makatibu wa Wabunge kwani kufanya hivyo itakuwa inaenda kinyume na taratibu zilizoлезwa katika jibu (a). (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa baadhi ya Halmashauri zimekuwa zinaandaa vikao makusudi kabisa na pengine Wabunge hatupati taarifa; kwa mfano, katika Halmashauri yangu na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOSES J. MACHALI]

hata katika Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Kibondo ambako Mheshimiwa Felix Mkosamali anatokea na ndiyo maana ameuliza swali hili. Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na Halmashauri hizi kuzingatia ratiba za Wabunge? (*Makofi*)

(ii) Ameeleza kwamba Makatibu wa Waheshimiwa Wabunge ni ruhusa kuhudhuria kwenye vikao hivi, lakini hawatalipwa posho kama Wananchi wengine wa kawaida; lakini Watendaji mbalimbali kwa mfano Watendaji wa Kata na Maafisa Tarafa katika Halmashauri yangu huwa wanaalikwa na kuhudhuria kwenye vikao hivi na wanalipwa posho. Kwa nini kunakuwa na misingi ya ubaguzi, hawa Makatibu wa Wabunge wasilipwe wakati hawa Maafisa Tarafa na Watendaji wanalipwa posho wakati hawachangii chochote katika vikao vile; kwa nini wanalipwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana, *please!*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili yaliyoulizwa na Mheshimiwa Moses Machali, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, kuhusu hawa ambao hawatoi taarifa, tunazo Kanuni hapa nimekuja nazo na nitasema kwa kifupi kwa sababu naheshimu Kiti. Tumeelekeza Halmashauri zetu na Ofisi yako Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya Bunge hapa, imetoa maelekezo kusema kwamba, wakati Vikao vya Bunge vinaendelea, tutengeneze ratiba ambazo zitaachana na kipindi hiki ambacho sisi tuko hapa kwa sababu sisi ni Madiwani.

Mimi siwezi kukaa hapa nikabishana kuhusu jambo hili kwa sababu linanihusu hata mimi; mimi nina Halmashauri inayoitwa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, nataka wakati watakapokaa pale niwepo. Kwanza, Mbunge ana *input* kubwa kwa sababu anakuja kwenye vikao hivi vikubwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

vya kitaifa, kwa hiyo, unategemea mchango wake utakuwa ni mkubwa katika ile Halmashauri inayohusika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazi siwezi kui-*miss* kabisa. Natoa kauli hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni marufuku, kwanza, *underline the word* marufuku, kuitisha kikao bila kumwambia Mbunge. Mheshimiwa Samwel Sitta, wanapokutana pale Urambo ni haki yako kama Mwakilishi wa Wananchi kupewa taarifa kuhusu kikao hicho labda wewe mwenyewe ushindwe na utoe udhuru kwamba hutaweza kwenda kule. Hiyo ndiyo kauli ya Serikali, hatuwezi tukawa tuna-*debate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti pale kwako Ilala ni haki yako na mimi nasema kama kuna Wakurugenzi Watendaji ambao wanafanya hivyo, tuleteeni majina yao tushuke nao jumla jumla, eeh ndiyo kwa kifupi tu hatuwezi kukaa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu hii habari ya posho inayozungumzwa hapa. Hawa Maafisa Tarafa wanaozungumzwa hapa, wamewekwa pale kwa utaratibu ambao ni wa kiserikali na *circular* ikaenda kule. Maafisa Tarafa hawa ni Watumishi wa Serikali. Afisa Tarafa ni mkono wa kuume wa Mkuu wa Wilaya. Tunataka wakati tunapokwenda kumhoji pale ajue, mpaka wale wanaoitwa Makatibu Tawala wa Wilaya wanakwenda pale, ili Mkuu wa Wilaya aonekane yuko *on top of business*, anajua kitu kinachoendelea katika Halmashauri.

Kinachozungumzwa sasa hapa ni kwamba, ruhusu utaratibu huo huo kwa hao ambao ni Makatibu wa Wabunge. Katibu wa Mbunge ni Katibu wa Mbunge siyo mwajiriwa wa Serikali. Kama ipo hoja ya msingi hapa tunafikiri Makatibu wetu waende kule, itabidi sasa tuanze kutoa mapendekezo; unaweza ukaenda kwenye *Association of Local Authorities of Tanzania* ukaisema hiyo au unaweza ukaipeleka katika Halmashauri ikaletwa hapa tukabadili sheria ili tuweze ku-*accommodate* hawa watu ambao wanazungumzwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nitafurahi sana nikisikia Makatibu wa Wabunge wanaruhusiwa kuingia katika vikao kwa sababu utakuwa ni msaada mkubwa sana kwangu. Hatuna tatizo na hilo, kama tukifuata taratibu tunaweza tukazungumzia jambo hili ili kuweza ku-*accommodate*. Nafikiri Mheshimiwa Machali *you have a point*, lakini nazungumzia sheria hapa, nikiubali Mheshimiwa Sitta ataniuliza nimekusikia unawaambia Makatibu wa Wabunge watakuwa wanaingia kwenye vikao, watalipwa na posho.

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na swali namba 122. Mheshimiwa Aliko Kibona!

Na. 122

Hitaji la Gari Hospitali Teule ya Isoko – Ileje

MHE. ALIKO N. KIBONA aliuliza:-

Hospitali Teule ya Isoko inahudumia Wananchi wengi katika Tarafa ya Bundali, Bulambya na Wilaya jirani lakini haina gari la kubebea wagonjwa, akina mama wajawazito na watoto, licha ya jiografia iliyopo kutoruhusu usafiri wa baiskeli:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa *Isoko DDH* kama ilivyofanya kwenye Hospitali nyingine nchini?

(b) Je, ni lini Serikali itaweka watumishi wa kutosha wenye sifa, vifaa tiba na dawa katika Hospitali ya Wilaya Itumba ili kuondokana na aibu ya Wananchi kufuata matibabu hayo Malawi?

(c) Kwa kuruhusu Wananchi wetu kupata huduma muhimu kama afya, elimu, matangazo, sukari na kadhalika kutoka Malawi; je, haishushi heshima ya nchi na kuwaondolea Wananchi uzalendo wa nchi yao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Hospitali Teule ya Isoko haina gari la kubebea wagonjwa. Halmashauri katika bajeti ya mwaka 2012/2013 iliomba maombi maalum ya shilingi 98,817,860/= kwa ajili ya ununuzi wa *Land Cruiser Hardtop Ambulance*. Fedha zilizoombwa zilipatikana na taratibu za manunuzi zinaendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wanaohitajika katika Hospitali ya Wilaya ya Itumba kwa mujibu wa lkama ni 198, watumishi waliopo kwa sasa ni 97. Hata hivyo, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Halmashauri iliomba kibali cha kuajiri watumishi 54 ili kujaza nafasi zilizozizi wazi.

Halmashauri inaendelea kufuatilia upatikanaji wa watumishi hao katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na watakaopatikana watapangiwa katika vituo vyenye uhitaji. Ili kuhakikisha Hospitali ya Wilaya inatoa huduma bora kwa wananchi, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Halmashauri iliidhinishiwa jumla ya Sh. 37,640,980/=; kati ya fedha hizo, Sh. 26,437,342/= ni za ununuzi wa dawa na Sh. 11,202,538/= ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Fedha zote zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao utaratibu ambao unaruhusu mtu yeyote kwenda nje ya nchi kwa ajili ya kupata matibabu au elimu kwa kibali maalumu. Aidha, kibali hicho hutolewa na Serikali endapo huduma hiyo haipatikani hapa nchini. Utoaji kibali hicho pia huzingatia mapendekezo ya mamlaka husika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Kuhusu Wananchi kutumia sukari kutoka nchi jirani, imebainika kwamba, ipo biashara ya magendo ambayo imekuwa ikiingizwa hapa nchini bila kufuata taratibu; mfano, katika Wilaya ya Ileje mwaka 2012 hadi Novemba, 2013 zilikamatwa tani 1.5. Bodi ya Sukari Tanzania ndiyo imepewa mamlaka ya kutoa vibali vya kuingiza sukari ndani ya nchi endapo kuna mahitaji au kusafirisha sukari nje ya nchi kwa misingi ya soko huria. Hivyo, hatua zimekuwa zikichukuliwa na Serikali kwa wale wote wanaokiuka utaratibu huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kibona!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuhusu ununuzi wa gari la wagonjwa, fedha ziliombwa na zimepatikana shilingi milioni 98.8.

Nataka kujua fedha hizo ziko wapi, nani anashughulikia ununuzi huo na mchakato umefikia hatua gani mpaka sasa hivi?

(ii) Kwa mujibu wa Naibu Waziri anasema, watumishi watakapopatikana watapangiwa katika vituo vyenye uhitaji, ina maana Utumishi wanapata shida kupata watumishi:

Je, Waziri anaweza kuiruhusu Halmashauri ikisaidiana na Mbunge wake, waweze kutafuta watumishi popote walipo na wailetee Tume ya Utumishi ili waajiriwe katika vituo vyetu tuondokane na kero ya kuwahudumia Wananchi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi tunazozitungumzia hapa zilikuwa katika Akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ileje. Wanaohusika na jambo hili kwa maana ya kuwapatia hilo gari na ninamwomba Mheshimiwa Kibona anisikilize hapa ili aende akafuatilie na atusaidie, katika utaratibu wa manunuzi, wametumia *single sourcing*. Maana yake nini? *Single source*, nikieleza hapa najua utanizuia utaniambia niache, lakini niseme tu kwamba, amepatikana Toyota na ndiyo ambao wanatakiwa kutoa hili gari.

Nimezungumza na Katibu wa Hospitali ya Ileje leo asubuhi na ninazo meseji zake ameniletea hapa kumwuliza swali hili hili ambalo naulizwa na Mheshimiwa Kibona. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Katibu huyo amenihakikishia baada ya wiki moja gari hili, milioni 98 ambazo zilitengwa wakati huo, maana yake kwa sasa hivi milioni 98 hazitoshi, ni milioni 150 ndizo zinatosheliza pale. Aje tushirikiane na huyu mtumishi kama alikuwa anasema uongo, mimi na yeye. Kwa hiyo, nataka nimwambie kwamba, *single sourcing* ndiyo ambayo imetumika hapa kwa ajili ya hizo fedha na Toyota ndiyo ambao wataleta gari. Nimemwuliza Katibu wa Hospitali wanategemea kuipata lini, akaniambia ni baada ya wiki moja kutoka sasa.

Pili, hii anayozungumza Mheshimiwa Kibona kwamba nitoe kibali hapa sasa hivi, hii itakuwa ni vurugu mechi. Naomba niseme, utaratibu wa nchi umeelekeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo inayoratibu na kusimamia masuala yote ya utumishi. Yaani pale kwake Ileje kama anataka kuweka watu, hawezi kuwaingiza nje ya mfumo huu niliuzungumza hapa. Kwa nini? Hii bajeti ya kwetu ni *cash budget*, ukiruhusu kila Halmashauri iajiri huko yenyewe inavyojua, kesho utawaona madaktari wako

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEM)]

hapa na bango, "tunataka haki zetu, tunaonewa" halafu itakuwa ni vurugu kubwa sana hapa. Uajiri wote lazima upitie pale utumishi mzee wangu. (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zambi!

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Abdulrahman Kinana, alifanya ziara katika Mkoa wa Mbeya, lakini pia katika Wilaya ya Ileje. Moja ya jambo alilolalamikiwa ni Hospitali ya Wilaya ya Ileje - Itumba kukosa daktari, kwani haina daktari hata mmoja, jambo linalolazimisha wagonjwa wote ambao wako katika maeneo ya jirani pale na Itumba, wanaohitaji *operation* kwenda Hospitali Teule kule Isoko:-

Je, Serikali inatamka nini kuhusu kuwapatia daktari walau mmoja au wawili kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Itumba?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii!

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutoa vibali vya ajira katika Sekta ya Afya unafanyika kwa ngazi za Wilaya. Hivi karibuni zoezi hilo lilikamilika na kila Wilaya walipatiwa vibali vya ajira. Suala la daktari anawekwa wapi au ni sehemu gani katika Wilaya ni maamuzi ya Wilaya husika. Ninachoweza kusema hapa ni kwamba, vibali vya madaktari vimetolewa na madaktari wameajiriwa. Safari hii tulifanya utaratibu mpya wa kuwataka wanaoomba waseme wenyewe wanataka kwenda wapi ili tuondokane

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

na lile tatizo la madaktari kupangiwa sehemu halafu wanaacha kazi wanaenda sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba, katika Wilaya hii inayozungumzwa hapa, nitafuatilia nione ni idadi gani ya madaktari wamepewa na litakuwa ni jukumu la Mganga Mkuu wa Wilaya kuhakikisha kwamba, kila hospitali yenye kuhitaji daktari wanapatiwa daktari badala ya kuwaweka wengi sehemu moja. Kwa hiyo, nitafuatilia suala hilo na nitampatia Mheshimiwa Mbunge maelezo ya kina. *(Makofi)*

Na. 123

Kuyarudisha Mashindano ya Sanaa Shuleni

MHE. RICHARD M. NDASSA aliuliza:-

Kabla ya kufutwa kwa michezo shuleni mwaka 2000, michezo ya sekondari ilikuwa inajulikana kama UMISASETA (Umoja wa Michezo ya Sanaa kwa Shule za Sekondari Tanzania) na iliporudishwa mwaka 2007 neno "Sanaa" likawa limefutwa na kubaki UMISETA, kitu kilichosababisha michezo yote ya sanaa ya kuimba, maigizo na ngoma (Sanaa za Ndani) kuondolewa na hadi sasa sanaa hizi hazifundishwi wala kushindaniwa shuleni:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyarudisha mashindano ya sanaa katika shule zote kuanzia msingi, sekondari na vyo ili kuibua vipaji katika suala zima la sanaa nchini?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, naomba kurekebisha neno UMISASETA na badala yake lisomeke neno UMISSETA - Umoja wa Michezo na Sanaa Sekondari Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kabla ya kusitishwa kwa Mashindano ya Michezo ya Shule za Sekondari mwaka 2000, mashindano hayo yalikuwa yakijumuisha michezo tisa ikiwemo Fani za Sanaa za Maonesho (maigizo, kwaya na ngoma).

Tangu mashindano haya yarejeshwe, Serikali imekuwa ikiongeza michezo ya kushindaniwa kwa awamu ili kuhakikisha kuwa inaendeshwa kwa ufanisi zaidi. Michezo inayochezwa hadi sasa ni pamoja na soka, wavu, kikapu, pete (*netball*), riadha, mpira wa meza, mpira wa mikono (*handball*) na mchezo wa bao ambao ni moja ya fani ya sanaa. Aidha, kuanzia mwaka 2009 mchezo wa soka unawashirikisha wasichana pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuthamini na kutambua hili, mpango wa Serikali kuanzia mwaka 2014 ni kuhakikisha kuwa sanaa za maonesho, yaani nyimbo, maigizo na ngoma zinashindaniwa katika Michezo ya Shule za Sekondari (UMISSETA) na Vyuo vya Ualimu (UMISAVUTA) kuanzia ngazi ya Shule Sekondari na Vyuo vya Ualimu hadi Taifa. Kwa upande wa Shule za Msingi (UMITASHUMTA), msisitizo upo katika michezo na taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa michezo ni ajira, hivyo, itaendelea kuhimiza kufanyika kwa mashindano kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa kwa lengo la kuendeleza na kuibua vipaji kwa vijana wetu. (*Makofi*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kwa kurudisha mashindano ya sanaa katika shule zetu za msingi, sekondari na vyuo, lakini kwa sababu ulimwengu wa sasa sanaa ya kuimba ni ajira, sanaa ya kuigiza ni ajira na sanaa ya ngoma ni ajira:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

(i) Ni kitu gani kilichoikera Serikali hadi ikaamua kuyafuta mashindano haya?

(ii) Kwa kuwa sasa Serikali imekubali kwamba mashindano haya yataanza kufanyika kuanzia mwakani; je, imejiandaa vipi kuhusu suala zima la ualimu na vifaa vya michezo hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nimshukuru Mheshimiwa Ndassa, kwa namna anavyofuatilia michezo kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo. Sasa suala hili kwa pamoja tunaweza tukalitatia kama ambavyo tumesema Serikali itarudisha michezo ya sanaa, nyimbo na maigizo kwenye shule za sekondari mwakani. Hata hivyo, anauliza kwa nini sasa wakati ule tulisitisha; kwanza, niseme kwamba wakati ule shule za sekondari zilikuwa chache sana, takribani shule kama 800, lakini leo hii tuna shule karibu 4600 hivi na kitu. Kwa hiyo, hata uwezo wa ku-*accommodate* mashindano yale sasa hivi inakuwa ni ngumu kidogo.

Vilevile kwa wakati ule mashindano haya yalikuwa yanafanyika wakati wa masomo, hali iliyopelekea wanafunzi na walimu kupoteza siku za masomo. Sasa hivi tuliporudisha mwaka 2007 na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ndiye alitangaza hilo, usimamizi wa kambi za michezo sasa umeimarika. Kwa wakati ule walipokwenda usimamizi haukuwa mzuri, hali iliyosababisha hata baadhi ya wanafunzi kuathirika kiafya na wengine kupata kesi za mimba pamoja na walimu. Vilevile, fedha na michango ambayo ilikuwa inatolewa wakati ule ilikuwa haina usimamizi mzuri, tofauti na sasa ambapo tuliporudisha tumeimarisha jambo hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maandalizi ya walimu; kule kule Mkoani Mwanza kuna Chuo cha Ualimu Butimba ambako ndiko tunatoa mafunzo ya ualimu wa masuala haya ya sanaa na michezo ili kuja kufundisha kwenye shule zetu za msingi na sekondari.

Na. 124

Ujenzi wa Benki ya Wanawake Tanzania Zanzibar

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR aliluliza:-

Eneo la kujenga Benki ya Wanawake kwa upande wa Tanzania Zanzibar limeshapatikana na benki hiyo ni muhimu sana katika kukuza kipato cha Wazanzibari kupitia mikopo:-

(a) Je, mwaka gani benki hiyo itaanzishwa Tanzania Zanzibar?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu Swali la Mheshimiwa Faida Bakari, napenda nitoe maelezo yafuatayo:-

Benki ya Wanawake Tanzania inalo lengo la kupanua huduma zake kwa kufungua Matawi Tanzania Zanzibar na Mikoa mingine. Kwa upande wa Zanzibar, Benki ya Wanawake kwa kushirikiana na Wizara ya Ajira, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO]

ya Fedha Zanzibar, zimekuwa na mchakato utakaopelekea kufungua Tawi au Ofisi ya Mikopo ya Vikundi vya Wajasiriamali wadogo wadogo hasa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Tawi la Benki ya Wanawake Tanzania litafunguliwa Zanzibar baada ya kukamilisha ukarabati wa jengo litakalotumika kwa shughuli za benki na kukamilisha taratibu zinazohusu ufunguzi wa tawi hilo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za ukarabati wa jengo la benki hii zitatengwa baada ya tathmini ya gharama za ukarabati zitakazoandaliwa na wataalam wa ujenzi.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kabla ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, napenda kuishukuru sana na kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza llani yake vizuri. Napenda pia kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika majibu yake inaonekana kwamba Benki hii kwa upande wa Zanzibar itachukua muda kuanzishwa, maana amesema mchakato, tunajua maana ya mchakato. Kwa kuwa Wananchi wa Zanzibar hususan wanawake wana mahitaji makubwa ya kupata katika benki hii ikiwemo mikopo kwa madhumuni ya kuendesha miradi yao mbalimbali:-

(i) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati mwafaka, kwa sababu lipo fungu la Zanzibar; lile fungu la Zanzibar labda kama itawezekana kisheria lihamishwe liende hivi sasa Zanzibar kwenye Benki ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR]

Wananchi wa Zanzibar ili ianze kutoa huduma na mikopo kwa Wananchi na Wanawake wa Zanzibar kabla halijaanzishwa?

(ii) Kwa kuwa jina la Benki hii ni Benki ya Wanawake Tanzania, lakini kabla haijasambaa maeneo yote ya Tanzania, ipo Dar es Salaam tu hivi sasa na wanaume ndiyo wanaopata mahitaji kwa wingi kutoka Benki hii pamoja na mikopo kuendesha biashara zao na benki hii ina jina la Benki ya Wanawake Tanzania. Swali langu liko hapa; je, inakuwaje wanaume wapewe mikopo kabla madhumuni ya kuanzishwa benki hii hayajawafikia Wanawake wote wa Tanzania? Je, haiwezekani Serikali kuanzisha Benki ya Wanaume na wao wakapata mikopo kutokana na benki yao? (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Faida Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Faida Bakar, kwa kuwa mstari wa mbele katika kupigania uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Zanzibar. Vilevile siyo tu kufuatilia masuala ya uanzishwaji wa Benki ya Wanawake, lakini pia masuala ya maendeleo ya Wanawake na Watoto Tanzania Bara na Zanzibar; hongera sana Mheshimiwa Faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikienda katika swali lake la kwanza, fungu la Zanzibar kwa nini lisipitishwe katika Benki ya Watu wa Zanzibar. Kwanza, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Faida Bakar kwamba, Benki ya Wanawake inapata fedha za mtaji siyo fedha za kukopesha. Mikopo tunakopesha kwa kutumia fedha za wateja. Kwa hiyo, pale ambapo tutapata fedha kwa ajili ya kuwawezesha kutoa mikopo, hatutasita kufanya hivyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO]

Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Mkurugenzi wa Benki, Mama Margaret Chacha, alishakwenda Zanzibar, ameongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar na kuona umuhimu wa kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mazungumzo yalishaanza na napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge hasa wanaotoka Zanzibar kwamba, tutafungua shughuli zetu Zanzibar mara tu mtaji wa benki utakapokamilika. Pia tutafanya mawasiliano na wenzetu wa Zanzibar kuhakikisha tunafanya haraka mchakato huu.

Hili la kwanza niseme tu imewezekana, kwa mfano, hata fedha za Benki ya Maendeleo ya Kilimo zilipitishwa pia kwenye *Tanzania Investment Bank*. Kwa hiyo, hicho ni kitu kinachowezekana.

La pili, kwa nini wanaume wanapata fedha kutoka kwenye Benki ya Wanawake. Ni kweli benki ilianzishwa kutokana na maombi ya wanawake hasa wa Umoja wa Wanawake Tanzania - UWT wa Chama cha Mapinduzi ili kuweza kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya wanawake.

Ninataka kumthibitishia Mheshimiwa Faida Bakar kwamba, kati ya wateja ambao wamepata mikopo, karibu asilimia 77 ni wanawake, kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi. Wanaume waliopata mikopo ni karibu asilimia 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtake tu Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba, wanawake tunawahitaji wanaume, hatuwezi kuwabagua. Lazima tufanye kazi pamoja ili kuweza kuwa na maendeleo ya kweli ya Watanzania, ya wanawake na ya wanaume. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda wetu ni mdogo, bado tuna maswali kama kumi.

Na. 125

Tija ya Mashindano ya *Miss Tanzania*

MHE. RUKIA KASSIM AHMED (K.n.y. MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS) aliluliza:-

Mashindano ya *Miss Tanzania* ambayo yalipigwa marufuku na Serikali ya Awamu ya Kwanza sasa yameibuka kwa kasi kubwa sana:-

Je, mashindano haya yana tija gani kwa Taifa?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashindano ya Urembo wa Tanzania hayajawahi kupigwa marufuku bali yalisimamishwa na Serikali miaka ya 1960 na baada ya vipindi kadhaa vya mabadiliko, Serikali iliyaanzisha tena mwaka 1994, kwa kuyaandalia kanuni na taratibu za kuyaendesha.

Kanuni na taratibu hizo zimekuwa zikitoa mwongozo kwa wadau wanaobuni ama kufikiria kuanzisha mashindano ya urembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashindano ya *Miss Tanzania* ambayo huanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa, yamekuwa yenye tija kwa vijana wetu na Taifa kwa ujumla. Mashindano hayo yamewezesha kuibua vipaji na ubunifu kwa washiriki ambao baadaye hupata fursa ya ajira katika makampuni na viwanda mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi. Kwa mfano, Bi. Happiness Magessa, Mshindi wa *Miss Tanzania* Mwaka 2001 ni mwanamitindo maarufu na anafanya kazi zake Marekani na Afrika ya Kusini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana washiriki wa mashindano haya, hupata mafunzo mbalimbali ya kujiamini na kujiendeleza wao binafsi kama vile kujenga uwezo na ubunifu katika sanaa, utamaduni, mawasiliano, siasa na elimu kuhusu afya ya uzazi na mabadiliko ya tabia katika kupambana na Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mshindi wa mashindano haya kitaifa...

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaomba utulivu.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mshindi wa mashindano haya Kitaifa, huliwakilisha Taifa letu katika Mashindano ya Kimataifa ambayo hufanyika katika nchi mbalimbali za ughaibuni. Katika kufanya hivyo, nchi yetu hupata fursa ya kupeperusha bendera ya nchi, kutangazwa kwa maliasili zetu, utalii, sanaa, utamaduni, rasilimali na vivutio tulivyonavyo kama mbuga za wanyama na mandhari nzuri ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mashindano haya yana tija kwa Taifa letu hasa kwa vijana wetu na jamii inayowazunguka kama vile wanamitindo na wafanyabiashara hasa katika Sekta ya Utalii. Serikali itaendeleza jitihada za kuyaimarisha kupitia watayarishaji wa mashindano haya na uangalizi wa karibu wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), kwa kuhakikisha kanuni na taratibu za mashindano haya zinafuatwa.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, bado nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa *Miss Tanzania* wa Mwaka 2012 alikuja hapa Bungeni katika Ukumbi wa Msekwa na ilikuwa ni aibu kubwa kwa sababu hajui kuzungumza lugha yake ya Taifa ambayo ni Kiswahili. Je, mtu anawezaje

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RUKIA KASSIM AHMED]

kupeperusha Bendera ya Taifa wakati hawezi kuzungumza hata Lugha yake ya Taifa? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba, mashindano haya ya urembo yanaleta ajira kwa baadhi ya vijana; je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa ipo haja ya kuyafuta mashindano haya na badala yake tuanzishe mashindano ya sayansi ambayo yataleta tija kubwa kwa Taifa hili? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya yongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mshindi wa mwaka 2012 ambaye alikuwa ni Brigit Alfred kwamba hawezi kuzungumza Kiswahili, alikuja hapa na anazungumza Kiingereza na kama kwa kuzungumza hivyo anaweza kupeperusha bendera yetu au kutuwakilisha kitaifa.

Mimi napenda niseme tu, anaweza kutuwakilisha kama Watanzania na jitihada tunazofanya Kiswahili ni muhimu akifahamu na ninadhani anakifahamu vizuri tu, sielewi ilitokea nini hapa akashindwa kuzungumza Kiswahili. Mimi nimeshakutana naye, tumekwishazungumza na nimeshamsikiliza, anaweza kuzungumza Kiswahili. Sasa nadhani ni tatizo labda la uelewa ambalo ndiyo tunasema wakati wakiingia katika haya mashindano, hufundishwa masuala mbalimbali likiwepo mojawapo la kujiamini. Labda aliona anaweza kuzungumza Kiingereza vizuri zaidi kuliko Kiswahili.

Niseme tu kwamba, wanapokwenda katika mashindano hayo huko nchi za nje, wanazungumza Kiingereza na ninadhani ndiyo maana ameweza kupita katika nafasi ndefu ndefu zaidi kwa kuweza kujieleza vizuri labda kwa Kiingereza huko alikokwenda.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwamba mashindano haya labda yafutwe ili tuweze kuweka mashindano ya sayansi. Kwanza, nadhani hakuna tija kuyafuta mashindano kama haya. Kimsingi, tunawahimiza vijana wetu wawe wabunifu na wenye kujituma ili kuweza kufanya masuala mbalimbali, lakini pia waweze kuingia katika masuala ya kujitafutia kipato, kuitangaza nchi yetu na kuendeleza utamaduni wetu.

Mashindano haya ya *Miss Tanzania* yanachukua nafasi hiyo kubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu kwa kuwatayarisha hawa vijana ambao wanajituma, lakini pia kwa kuwatayarisha wale ambao wameanzisha hiyo kampuni wakifuata taratibu na kanuni zilizowekwa kuweza kuyasimamia vizuri na kuwatayarisha hawa vijana kuweza kushinda na wakienda huko nje huwa wanatangaza nchi yetu kwa bidii kabisa, kwa kufuata taratibu na kanuni zilizopo.

MWENYEKITI: Tunaendelea, Wizara ya Nishati na Madini. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mdogo sana tumebakiwa na maswali manane na tuna dakika 40 tu. Mheshimiwa Sylvester Muhoja Kasulumbayi!

Na. 126

Matumizi ya Nishati

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI) aliuliza:-

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa kwenye Kongamano la Wadau wa Nishati tarehe 8 hadi 9 Aprili, 2010 na Ndugu N.C.X Mwiwaha, ambaye kwa sasa ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, ni kwamba, Watanzania wa kipato cha chini wanatumia asilimia 35 ya pato lao kwa ajili ya matumizi ya nishati:-

(a) Je, kwa sasa asilimia hiyo ya matumizi kwa watu wa kipato cha chini imepanda au imeshuka?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI)]

(b) Je, uvumbuzi wa visima vipya vya gesi asilia vimesaidia matumizi makubwa ya nishati kwa Watanzania wenye kipato kidogo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kipindi kirefu kimepita tangu kutolewa kwa takwimu ya asilimia 35 ya pato inayotumiwa na Watanzania wenye kipato cha chini, upo umuhimu mkubwa wa kuwa na takwimu mpya. Ili kupata takwimu hizo, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali zikiwemo Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), Ofisi ya Takwimu ya Taifa na Tume ya Sayansi na Teknolojia, itafanya utafiti kwa nchi nzima. Utafiti huo utazingatia mambo mawili muhimu yafuatayo:-

(i) Matumizi ya nishati kwa ngazi ya kaya ikiwemo matumizi ya mkaa, mafuta ya taa, kuni na *Liquefied Petroleum Gas (LPG)*; na

(ii) Kipato cha Wananchi waliopo mijini na vijijini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni faraja kubwa kwa nchi yetu kuwa na gesi asilia inayoendelea kugunduliwa. Hadi sasa kiasi cha gesi kilichogunduliwa nchini ni futi za ujazo zipatazo trilioni 46.5. Serikali kwa kupitia *TPDC* ilifanya upembuzi yakinifu juu ya usambazaji na matumizi ya gesi asilia kwa watumiaji wa majumbani, taasisi mbalimbali na magari katika Mkoa wa Dar es Salaam uliolenga kupunguza matumizi ya nishati nyinginezo kama vile mkaa, kuni na *LPG* kwa upande wa kupikia na petroli na dizeli kwa upande wa magari. Kazi hii ilifanywa mwaka 2006/2007 na Mshauri Mwelekezi kutoka China aitwaye *Ultimate Technology Limited*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ya upembuzi yakinifu, Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia Jijini Dar es Salaam utahusisha kaya 30,000, magari 8,000, ambayo yatajaza gesi kupitia vituo vipatavyo 15 pamoja na taasisi na hoteli 10. Gharama za Mradi wa sasa ni Dola za Marekani milioni 65.1. TPDC imemwajiri Mshauri Mwelekezi wa kudurusu upembuzi uliofanyika hapo awali na kupata gharama halisi pamoja na kusanifu michoro ili Mradi ujengwe.

Aidha, katika kuandaa Sera ya Gesi, Sheria ya Gesi na Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia, Wizara inazingatia suala la Wananchi wa kipato cha chini kunufaika na gesi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango kama huu wa matumizi ya gesi majumbani na kwenye magari unaendelea katika Mikoa ya Mtwara na Lindi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Waziri hivi karibuni alinukuliwa na vyombo vya habari akisema kwamba, Watanzania ambao hawawezi kulipia ongezeko la bei za umeme watumie vibatari. Kauli ambayo iliwaumiza sana Wananchi. Nilitaka kujua msimamo wa Serikali ni nini?

(ii) Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema tafiti zitafanyika kupata takwimu sahihi, lakini kwa takwimu nilizonazo ni kwamba, Tanzania inatumia ekari za miti 350 ambazo ni sawa na hekta 800 na kitu kwa siku kwa ajili ya ukataji miti. Wizara ya Nishati na Madini imefanya juhudi gani kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili, Ardhi na Mazingira kuhakikisha inaondoa tatizo hili la uharibifu wa mazingira kwa pamoja ili kupunguza tatizo hili katika nchi yetu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli tarehe 25 mwezi Novemba nilihojiwa na *Radio One* kuhusiana na masuala ya kupanda kwa bei ya umeme. Ninasikitika kwamba, nilinukuliwa vibaya na baadhi ya vyombo vya habari kwa sababu sikusema hicho kama walivyokiandika. Bahati nzuri nilirudi tena *Radio One* nikapewa ile *clip* nikaisikiliza tena na Mkurugenzi wa *Radio One*, Mama Mhavile na kwa kweli maneno hayo hayamo.

Nichukue nafasi hii kuwaomba Watanzania kwamba, wakati mwingine habari hizi zinapopotoshwa zinaondoa hata msingi mzima wa maudhui ya programu iliyofanyika kwenye vipindi vya redio au kwenye magazeti. (*Makofi*)

Nilichoulizwa na *Radio One* ni kwamba, je, katika hali ya sasa ambapo tunapeleka umeme vijijini na sasa mnataka kupandisha bei ya umeme mnadhani Mwananchi wa Kijijini anaweza kulipia gharama hizo? Swali lilikuwa zuri tu na mimi nikasema, kwanza, sitaki kusema kwamba bei itapanda au haitapanda, kwa sababu Wizara ni *level* ya maamuzi. Nikaelezea mchakato jinsi ulivyo kwamba, *TANESCO* wanaomba kwa *EWURA* kwamba wanataka kupandisha bei ya umeme na baadaye *EWURA* wanafanya kazi yao ya kufanya *analysis*, wanapeleka ule ushauri Wizarani. Kwa wakati ule kwa sababu Wizarani tulikuwa hatujaletewa ile taarifa, nisingeweza kuwa kwenye nafasi ya kutoa maoni yangu wakati mimi ni ngazi ya maamuzi. Kwa hiyo, ilikuwa ni vigumu sana kusema ninajisikiaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema mimi na ndipo ninapokuja kwenye swali la Mheshimiwa Kasulumbayi, anasema asilimia 35 ya mapato ya Mwananchi wa Kijijini anatomia katika masuala ya nishati, kwa hiyo, kwa mujibu wa takwimu hizi ambazo zilitolewa ni kweli kwamba,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]
Mwananchi wa Kijijini anatumia gharama kubwa kuhusiana na masuala ya nishati. Ukinunua mafuta ya taa tu, ukawasha kwenye koroboi si sawa na mtu anayetumia umeme ambaye analipa shilingi 20,000 au 15,000 kwa mwezi kwa matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, mwananchi wa Kijijini anapata gharama kubwa sana, ndicho kilichotokea mpaka tukalinganisha hizo bei za kibitari na matumizi mengine.

Mimi ni mtoto wa maskini, natoka kijijini, pengine nimetumia koroboi kuliko hata anayesema naikashifu koroboi. Nimesomea koroboi mpaka namaliza darasa la saba, kwa hiyo, siwezi kusema maneno hayo. Ingawa mchakato wa bei ya umeme bado unaendelea, *EWURA* wataleta Wizarani kwetu na sisi tutaangalia hali ya Uchumi wa Tanzania na soko la uwezo wa Watanzania kununua kama unaweza kukubaliana na ombi hilo la *TANESCO* la kupandisha bei. Kwa hiyo, Serikali hatuwezi kukurupuka tu na mtakumbuka mwaka jana tulikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni takwimu. Hizi takwimu kwa sasa wakati tukiwa hatuna gesi, bei ya umeme tunayoizalisha nchini na tunayowauzia Wananchi gharama yake ni kati ya senti 35 na senti 45 za Kimarekani. Tunatarajia kama gesi itakuja gharama yake itakuwa kati ya senti tano hadi senti nane. Gharama hii itakuwa imeshuka kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 20 kutoka kwenye gharama ya sasa.

Kwa hiyo, unafuu huu utasababisha Wananchi wengi watumie gesi majumbani kuliko kutumia kuni na hivyo tunaweza tukaokoa misitu yetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, swali limechukua muda mrefu sana, tunaendelea na swali Namba 127; Mheshimiwa Mgimwa kwa niaba ya Mheshimiwa Komba!

Na. 127

Kupeleka Umeme Tarafa ya Sadani

MHE. CAPT. JOHN. D. KOMBA (K.n.y. MHE. MAHMOUD H. MGIMWA) aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi kupeleka umeme kwenye Tarafa ya Sadani yenye Kata nne za Ikweha, Sadani, Igombavanu na Isalavanu ambazo zina vijiji 18?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2013/2014, kupitia Mradi Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa kushirikiana na *TANESCO*, imepanga kutekeleza Mradi wa Kupeleka Umeme katika Tarafa ya Sadani. Mradi huo unalenga kupeleka umeme katika Vijiji vya Ndolezi, Isalavanu, Lugoda, Mapogoro, Igombavanu, Sadani, Kibada, Ihanzutwa, Igomaa na Madibira. Gharama ya kufikisha umeme katika vijiji hivyo inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 8.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 74.2; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 24.8; ufungaji wa transfoma 16; na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 300. Aidha, Kata ya Ikweha itajumuishwa katika Miradi mingine ijayo kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi wa kutekeleza Miradi yote ya Mkoa wa Iringa alikwishapatikana, ni Kampuni ijulikanayo kwa jina la *Energy - PTS*.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Ni kweli kama alivyosema mkandarasi ambaye anaitwa *Energya PTS* amepatikana, lakini Mheshimiwa Mgimwa angependa kujua ni lini Kata zake hizo nne za Ikweha, Sadani, Igombavanu na Isalavanu zitaanza kujengwa? (*Makofi*)

(ii) Mradi kama huu upo katika Wilaya yangu ya Nyasa kutoka Mbinga, Mbamba Bay, Mwambao wa Ziwa Nyasa na eneo la Umatengo. Je, ni lini sasa maeneo haya nayo yataanza kujengwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana, swali hili lina wachangiaji wengi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Komba, kama ifuatavyo:-

Kampuni ya *Energya* ambayo imepatikana kwa ajili ya kujenga Miradi ya Umeme Mkoa wa Iringa, inachofanya sasa hivi ni *mobilization*. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumwondoa wasiwasi kwa sababu sehemu kubwa ya vifaa vya ujenzi wa miradi ya umeme vinaagizwa nje. Sasa hivi wameagiza na ninaamini kabla ya mwezi Machi, shughuli kwenye *ground* itaanza. Kwa sasa wanachofanya wanapita na kuweka alama maeneo ambamo nguzo zitapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Miradi kama hii pia ni kweli ipo Nyasa, Mbinga na maeneo yote ya Mwambao mwa Ziwa Nyasa. Nichukue nafasi hii kumwondoa wasiwasi Mheshimiwa Komba kwamba, mikoa ambayo haikupata wakandarasi, maana katika mchakato wa mwanzo tulipata wakandarasi katika mikoa 11 na mikoa mingine yote haikupata wakandarasi; mchakato huo ninaamini kabla ya Bunge hili kwisha utakuwa umekamilika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]
Tulikuwa tumekubaliana na REA kwamba, waukamilishe na wakandarasi wawe wamepatikana katika mikoa yote kabla ya tarehe 18. Nikitoka hapa nitacheki wamefikia wapi ili ikiwezekana niweze kuwapatia Waheshimiwa Wabunge, majina ya wakandarasi waliopatikana kwenye maeneo yao kabla hatujaondoka kwenye Bunge hili. (Makofi)

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza kabisa, kwa niaba ya Wananchi wa Halmashauri ya Meru, naishukuru Serikali kwa Miradi ya Usambazaji wa Umeme Vijijini ambayo inaendelea. Kwa sasa tunapozungumza vijiji vingi vikiwepo Mulala, Nambala, Hurisho, Kata ya Nkwarisambu, Nkwanekoli na maeneo mengine, tayari umeme umekwishafungwa na *Phase II* tayari imeanza na juzi nimeona wakipita kuangalia sehemu ambazo nguzo zinakwenda kuwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Miradi ya Usambazaji wa Umeme Vijijini ikiendelea, zile Kamati ambazo zilikuwa zinaratibu kwa maana ya wale Wananchi, kuna michango ambayo imekuwa ikichangishwa kwa Wananchi na mtu ambaye hachangi hata kama nguzo inapita nje ya nyumba yake, anaonekana hayupo kwenye mfumo na hatapatiwa umeme.

Sasa swali langu ni kujua kutaka tu kwamba hivi hii michango mingine ambayo inachangishwa kwa Wananchi na hizi Kamati ni halali; na kama ni halali uratibu wake kwa maana ya ufuatiliaji uko namna gani? Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]

Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Joshua Nassari, kwa kuwa muungwana na kuishukuru Serikali. Serikali yetu haina ubaguzi, tutafanya kazi kwa Wananchi wa Tanzania kwa sababu walituumini na wakatuchagua na hivyo waamini utekelezaji uliotukuka wa maendeleo yao. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Arumeru yote hii tukimaliza *REA Phase II* itakuwa na umeme.

Nichukue nafasi hii kuwaomba Wananchi wachukue tahadhari kubwa na hapa niseme na Wabunge wote, juu ya matapeli wanaoingilia utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijini. Hiki kitu anachokisema Mheshimiwa Mbunge hapa kwamba, kuna Kamati na michango, mimi ndiyo nasikia leo ingawa ndiye Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Kupitia hiyo nitajaribu kuangalia, lakini najisikia kusema kwamba, hiki kitu siyo halali. Wanaoweka umeme ni *REA* kwa kushirikiana na *TANESCO*, hakuna mtu mwingine tena, hakuna Kamati wala kitu kingine.

Kwa hiyo, huo ni utapeli na ni uongo na pengine tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujua hizo Kamati ni za akina nani na zinafanya hivyo kwa sababu gani. (*Makofi*)

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Swali langu, kama ilivyoainishwa kwenye swali yapo maeneo mengi sana hapa nchini ambako kwenye Tarafa unaweza ukakuta kuna Kata moja tu ndiyo yenye umeme. Suala hili lipo hata Iramba, Tarafa ya Kisiriri ina Kata moja tu ya Kiomboi yenye umeme, Tarafa ya Shelui ina Shelui peke yake, Ndago ina Ndago peke yake, Kinampanda ina Kinampanda peke yake. Kwa nini Serikali isifanye sensa ili kugawa umeme huu kwa uwiano katika Tarafa ambazo hazina umeme?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, bado kuna wachangiaji wawili hapa.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kama ifuatavyo:-

Ni kweli tulipokuwa tunapanga vipaumbele au orodha ya vijiji tuliwashirikisha sana Waheshimiwa Wabunge. Pale ambapo walishiriki tuliamani kwamba, kila mmoja amejaribu kutoa maoni yake juu ya anavyopenda mtandao wa umeme uwe katika maeneo yake. Mtakumbuka tulifanya hivyo katika Bunge la Bajeti la mwaka 2012/2013. Nichukue nafasi hii kama kutakuwa na *gaps* hizo ambazo siamini kwa Jimbo la Mheshimiwa Mwigulu karibu maeneo yote yale ambayo ni muhimu na kupitia uwiano wa Tarafa yote yatapata umeme kupitia *REA Phase II. (Makofi)*

Nampongeza Mheshimiwa Mwigulu, alishiriki vizuri katika zoezi hili na ndiyo maana alipanga vizuri vile vijiji vyake na vyote vitapata umeme kama alivyoomba. Kama kuna wengine ambao mambo hayajakaa vizuri, kwa sasa hatua tuliyofikia hatuwezi tena kwa sababu tumeshafikia hatua ya kumpata mkandarasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Josephat Kandege, nitamalizia na Mheshimiwa Silinde!

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Inafurahisha sana unaposikia Kata na Tarafa zinapatiwa umeme. Naomba kauli ya Serikali kwa zile Wilaya zote ambazo hazijapata umeme ikiwemo Wilaya Kalambo kuna mpango gani mahususi wa kuhakikisha umeme unapelekwa kwanza katika hizi Wilaya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Kandege, kila mara tunapokutana salamu yake ni Kalambo umeme lini! Nimwondoe wasiwasi katika vipaumbele vyetu tulivyoviweka na hata kibajeti Wilaya zote nchini zitachukua kiasi cha shilingi bilioni 70 kuwekewa umeme na Kalambo imo. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, itatekelezwa na Mkandarasi amekwishapatikana.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Halmashauri tangu Dunia ianze kama ilivyo Halmashauri ya Momba, Jimbo la Mbozi Magharibi, katika Kata zake zote hakuna umeme kabisa tangu dunia ianze. Serikali ituambie ni mpango gani maalum wa haraka unaweza kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Momba kupata umeme kabla ya mwaka 2015?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu *short and clear!*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda mpaka Jimboni kwa Mheshimiwa Silinde, tumefanya kazi pamoja. Nachukua nafasi hii kumhakikishia kwamba, Wilaya ya Momba ni miongoni mwa Wilaya ambazo zitapewa umeme kama zilivyo Wilaya nyingine ambazo ni mpya. Wilaya yake ni mpya na ndiyo maana haina umeme. Hata hivyo,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]
nichukue nafasi hii kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba, mkandarasi atapatikana, Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo imechelewa kupata wakandarasi, lakini tutakapopata mkandarasi mara moja tutaanza na kipaumbele ni Wilaya zote mpya nchini.

Na.128

Fidia kwa Wakulima wa Kahawa Kilimanjaro

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA aliuliza:-

Wakati wa mdororo wa uchumi mwaka 2008/2009 Wakulima wa Pamba walilipwa fidia ya pamba yao waliyoiuza kwa hasara:-

Je, kwa nini Wakulima wa Kahawa wa Kilimanjaro wasilipwe fidia ya kahawa yao waliyoiuza kwa hasara?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Benki Kuu, ilitekeleza Mpango wa Kususuru Uchumi kwa kuweka utaratibu na vigezo kwa wale wote walioathirika na mdororo wa uchumi duniani. Waombaji walioathirika na mdororo walitakiwa kuwasilisha maombi yao kupitia benki zilizowapatia mikopo kama uchambuzi wa awali kabla ya kupeleka Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fidia ya Wakulima wa Kahawa yaliyowasilishwa ndani ya muda uliopangwa yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 20.07 na baada ya kufanyiwa uchambuzi kwa kuzingatia vigezo vilivyokuwa vimekubalika kati ya *BoT*, Bodi ya Kahawa Tanzania na wadau wengine, Serikali iliidhinisha kiasi cha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

shilingi bilioni 9.87 kilipwe kwa wakulima wa kahawa kama fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 9.32 zililipwa kupitia Benki ya *CRDB* na shilingi milioni 551.51 zililipwa kupitia Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (*Kilimanjaro Cooperative Bank Limited*), ambapo wakulima na vyama vya wakulima 60 walilipwa na *CRDB* na wale waliolipwa na Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro walikuwa 22 na wote walikiri kupokea fedha hizo. Aidha, shilingi bilioni 9.32 zililipwa kama fidia kwa wakulima wa pamba. Fedha hizi zililipwa kupitia *CRDB*, *TIB*, *KCB* na Benki ya *EXIM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waombaji waliostahili kupatiwa fidia ni wale tu ambao mahesabu yao ya kibiashara yalionesha hasara na ambao waliwasilisha maombi ndani ya muda uliopangwa kwa kuanzia tarehe mosi Julai, 2009 hadi tarehe 30 Juni, 2010. Hivyo, wote ambao hawakupata fidia hii ni ama tathmini ya madai yao haikuonesha hasara waliyopata au waliwasilisha madai yao nje ya muda uliopangwa.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Naibu Waziri wa Fedha, kwa majibu yake. Sasa kule Kilimanjaro tuna tatizo kubwa sana, *KNCU* ilipeleka madai ya hasara ya mdororo nje ya muda, lakini hao hao *KNCU* wamekuwa wanawaambia wakulima kwamba, Serikali itawalipa hao wakulima na sasa hivi wananunua kahawa kwa mkopo kwa shilingi 1,500.

(i) Naomba Serikali ithibitisha *KNCU* inadai shilingi ngapi zinazotokana na mdororo wa uchumi ambazo Wakulima wa Kahawa watapewa kama hakuna mtuambie?

(ii) Kama *KNCU* ilishindwa kupeleka madai yake wakati mwafaka na wakulima sasa hivi wanakatwa karibu shilingi bilioni tano zinazotokana na hilo deni; nani alaumiwe na ni hatua gani zinachukuliwa kwa Viongozi wazembe wa *KNCU*? (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba, wale wote ambao walikidhi zile *criteria*, pamoja na kwamba kulikuwa na ule muda wa kuwasilisha yale maombi...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM): ... baada ya kufanyiwa *assessment* na ikaonekana wanastahiki, basi walilipwa. Kwa sasa hivi ninavyozungumza, hakuna fedha hiyo. Kwa hiyo, ninawaomba sana Wakulima wa Kilimanjaro wajue kwamba, Serikali sasa hivi haina programu hiyo.

Kuhusu swali lake la pili, nani alaumiwe; Serikali tumefanya kazi yetu na kwa sababu *KNCU by then* kama walikuwa na madai mengine yalikuwa hayajakidhi *criteria* na kwamba hatukuweza kulipwa. Kwa hiyo, nadhani hapa Serikali siyo ya kulaumiwa kwani tayari ilikuwa imeweka hizi *criteria* na hawaku-*fulfil*. Hiyo progamu sasa hivi imekwisha, hivyo ndivyo hali ilivyo na natarajia Wakulima wa Kilimanjaro watalifahamu hilo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, halafu Mheshimiwa Machangu na tutamalizia na Mheshimiwa Mnyaa!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia suala la *stimulus package*, Mhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alionesha kwamba zaidi ya shilingi bilioni 48 hazikuwa na maelezo na Serikali ikawa imekubali kwamba utafanyika Ukaguzi Maalum. Nilikuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KABWE Z. ZITTO]

naomba Mheshimiwa Waziri alijulishe Bunge lako Tukufu ni lini Taarifa ya Ukaguzi huo Maalum italetwa Bungeni kwa ajili ya mjadala?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zitto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hilo analolizungumza na sasa hivi Serikali kwa kushirikiana na *BoT* tunatayarisha taarifa ambayo itapelekea sasa Ukaguzi Maalum ufanyike. Kwa hiyo, hilo litafanyika, siwezi nikamwambia lini kwa sababu taarifa ina-*involve stakeholders* wengi. Kwa hiyo, *once* tukimaliza tutaiweka kwa ajili ya kufanyika Ukaguzi Maalum. (*Makofi*)

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliondoa ruzuku katika dawa za kahawa na kwa hiyo dawa zimekuwa aghali sana, kiasi kwamba Wakulima wa Mkoa wa Kilimanjaro wengine wameacha kulima kahawa na badala yake wanalima nyanya na kabeji. Je, ni lini Serikali itarudisha ruzuku hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku inayotolewa kwenye mazao ya kahawa, tunatoa ruzuku upande wa miche kwa maana ya kupata miche bora zaidi. Utaratibu wa ruzuku umegawiwa kwa mazao yote, kuna baadhi ya mazao kama tumbaku haipati kabisa, lakini kulingana na uwezo na upatikanaji wa fedha, Serikali inakusudia kupanua wigo wa ruzuku kwa mazao yote ili wakulima wapate msaada mkubwa zaidi kutoka katika mfumo huo.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Mnyaa!

MHE. MOHAMED HABIB J. MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe na Wabunge wote katika Bunge hili, maisha yote tunasikia fidia kwa wakulima na wafugaji tu, sijapata kusikia fidia kwa wavuvi. Ikiwa uchumi wa nchi hii unajengwa na wakulima na wafugaji tu; ni kwa nini tunasikia fidia za wafugaji wakati wa ukame ng'ombe wanapokufa, lakini hatujasikia fidia kwa wavuvi wanapoharibikiwa na mitego yao, wapoharibikiwa na vyombo vyao, maisha yote faida kwa wakulima na wafugaji. Je, Serikali inataka kutuambia kwamba wana *double standards?* (Makofi)

MWENYEKITI: Waziri wa Uvuvi yupo? Hayupo!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Habib Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Fidia hizi zilizokuwa zinalipwa, hizi zote ambazo zimetajwa kiukweli zilikuwa zinatokana na *natural disasters* na si vyombo ama vifaa ambavyo wanatumia na vitu kama hivyo. Serikali haina mpango wa kutoa fidia katika maeneo hayo. *Once* wavuvi kama wavuvi watakuwa wamekumbwa na *natural disasters*, nadhani Serikali ipo hapa kwa ajili ya Wananchi. Tumeona hata Wananchi wa kawaida, kumetokea *disaster* pale Zanzibar na sasa hivi Serikali kwanza, inanunua meli, lakini pili inaendelea kulipa fidia. Kwa hiyo, zile *natural disasters* ambazo Serikali haiwezi kuzi-*control* zitaendelea kulipwa. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, umejibu vizuri sana. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba!

Na. 129

Kilimo cha Mpunga

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua kilimo cha mpunga katika Kata za Loya na Miswaki, Mbuga ya lwembele kwa umwagiliaji na kupeleka mbegu bora ya *SARO 5* ambazo Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) wanatoa ufadhili wa kiutafiti na majaribio ili wakulima wa Jimbo la Igalula nao wafaidike?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na bwawa kwa ajili ya Skimu za Miswaki, Loya na Goweko ambazo zipo katika Kata za Loya na Miswaki kwenye Jimbo la Igalula. Ukarabati wa Skimu ya Miswaki yenye ukubwa wa hekta 300 upo katika hatua za mwisho za kukamilishwa, ambapo katika mwaka 2012/2013 ilitengwa shilingi milioni 60 kupitia Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (*DADPs*), kwa ajili ya kurekebisha sehemu korofi za mifereji na banio ambapo ukarabati unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Loya ina ukubwa wa hekta 1,000 ambapo tayari upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina umefanyika na kinachoendelea sasa hivi ni usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji inayojumuisha ujenzi wa bwawa, banio na mifereji ya kumwagilia maji mashambani. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Serikali imetenga shilingi milioni 89.6 kupitia Mipango

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Uyui na Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu hii inatarajiwa kutengewa fedha za utekelezaji katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa, banio na mifereji. Aidha, usanifu wa bwawa na miundombinu ya Skimu ya Goweko yenye ukubwa wa hekta 200, umekamilika pamoja na Taarifa ya Mazingira iliyowasilishwa kwenye Baraza la Taifa la Mazingira (*NEMC*), kwa ajili ya kupata cheti cha kuruhusu kuanza ujenzi. Katika mwaka 2014/2015, Serikali inategemea kukamilisha ujenzi wa mifereji ili skimu hii iweze kutumika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa ujenzi wa skimu hizi kutawezesha Wakulima wa Kata za Loya na Miswaki kuwa na uhakika wa uzalishaji wa mpunga na mazao mengine kupitia kilimo cha umwagiliaji. Wizara yangu itahakikisha kuwa skimu hizo zinapatiwa ruzuku ya mbegu bora ya mpunga aina ya *SARO 5* ambazo zina tija kubwa ya uzalishaji na uhakika wa soko.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mfutakamba, ngoja uitwe kwanza.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, niwie radhi kidogo.

MWENYEKITI: Haya sasa uliza swali lako. (*Kicheko*)

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, ni mpango gani Serikali inawaandalia Wanaigalula na wakulima wengine wa zao la Mpunga katika utaratibu wa kuongeza thamani ya zao hilo kupitia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA]

mnyororo wa thamani (*Value Chain*) ili pato lao liongezeke na tuweze kuwa na mpunga au mchele, *Igalula Super Rice*?

(ii) Je, Serikali kupitia SUMA JKT au mpango mwingine wowote ule inaweza kutupatia kwa mkopo matrekta kama 50 hivi ili yalime katika mashamba hayo ya skimu zilizopo na mengine katika Kata 10 za Igalula ili na sisi tuweze kuongeza tija ya pato katika utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*) Igalula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu wa kuweka *value additional* kwenye mpunga kwa maana ya Igalula ni mpango ambao tunauhusisha na maeneo yote yanayozalisha mpunga huko Bahi, Mbarali, Shinyanga na kwingineko. Mpango wenyewe unahusisha kuwakusanya wakulima wadogo wa mpunga ili katika jamii ya kikundi chao waweze kuwa na uwezo wa kukoboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu wazi kwamba, unapokuwa na uwezo wa kukoboa, hata kipato chako kinaongezeka.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi utaratibu ni huo. Kupitia Benki ya *TIB* na benki zingine zenye madirisha ya kuwezesha kilimo, tunahamasisha vikundi vya wakulima wadogo wadogo kuwa na utaratibu wao wenyewe wa kukoboa ili kuongeza thamani kwenye mpunga wao kwa kuwa wakiuza kama mchele wanakuwa wanapata kipato kikubwa zaidi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, utaratibu wa sasa ni kwamba, matrekta 1,800 ya kwanza ya SUMA JKT yalishatolewa yote. Katika utaratibu ule tuliona kuna baadhi ya mikoa ambayo Viongozi wa Mkoa walihamasisha wao wenyewe upatikanaji wa matrekta yale kwa wakulima wao, kama ilivyokuwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa awamu hii ya pili ambayo itakuwa na matrekta zaidi ya 3,000, ikiwa Mkoa wa Tabora utafanya uhamasishaji wa makusudi, Serikali itahakikisha wanapata matrekta haya 50 kwa ajili ya kuboresha kilimo cha *mechanization* katika Mkoa wa Tabora.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Wilaya ya Nkasi kupata Hati Chafu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imesimamisha kupeleka fedha kwenye Mradi wa Skimu ya Lwanfi na kuwatesa wananchi kama wakulima wa mpunga 3,000 wa vijiji saba kando ya Ziwa Tanganyika katika Kijiji cha Kilanda. Je, Serikali inawatendea haki wakulima hao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WAKILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Halmashauri kupata hati chafu na Serikali kusimamisha mgao wa ruzuku katika miradi yake mbalimbali ni jambo ambalo tumekuwa tunalizungumza na linajaribu kupatiwa ufumbuzi, kwa sababu kwa hakika wanaosababisha hasara ni wengine na wanaoumia ni wengine. Naomba nimhakikishie

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Ally Keissy kwamba, jambo hili tutaliangalia na Wizara husika kwa maana ya TAMISEMI na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ili kuangalia kama Mradi huu kweli umekidhi *value for money* kwa maana ya matumizi bora, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Maafisa Kanda wa Umwagiliaji watakwenda kuangalia kama fedha zilizotumika kwenye Mradi huu *specifically*, zimekwenda vizuri ili fedha hizi ziendeleo na Mradi huu ukamilike kwa wakulima hao 3,000 wa mpunga.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa David Kafulila, kwa niaba yake, Mheshimiwa James Mbatia!

Na. 130

Mkoa wa Kigoma Kuwa Mkoa wa Kitumbaku

MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE. DAVID Z. KAFULILA) aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa Mikoa maarufu kwa uzalishaji wa Tumbaku nchini:-

(a) Je, ni kwa nini mpaka sasa Mkoa huo haujapewa hadhi ya kuwa Mkoa wa Kitumbaku ili kusogeza huduma kwa wakulima ambao kwa sasa wanategemea huduma kutoka Urambo?

(b) Je, ni lini Serikali itaupa Mkoa huo hadhi ya Mkoa wa Kitumbaku ili kupunguza hasara wanazopata wakulima wake?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa Mikoa inayozalisha tumbaku nchini ambapo zaidi ya tani 50,000 huzalishwa kwa mwaka na Mkoa huo umepitishwa kulima tumbaku kwa mujibu wa Sheria ya Tumbaku Na. 24 ya mwaka 2001 na Kanuni zake za mwaka 2005. Aidha, pamoja na kiasi hicho cha uzalishaji Mkoa wa Kigoma haujapewa hadhi ya kuwa Mkoa wa Kitumbaku kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha ili Bodi ya Tumbaku iweze kufungua ofisi na kusogeza huduma hiyo karibu na Wakulima wa Tumbaku wa Mkoa wa Kigoma kama ilivyo kwa Mikoa mingine ya Kitumbaku.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mchango wa Wakulima hao wa Tumbaku wa Mkoa wa Kigoma, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku, katika mwaka wa fedha wa 2013/14 inatarajia kufungua ofisi yake Mkoani Kigoma ili kusogeza huduma kwa Wakulima wa Tumbaku wa Mkoa huo na kuufanya kuwa na hadhi ya Mkoa wa Kitumbaku kama ilivyo kwa Mikoa mingine maarufu kwa kilimo cha zao hilo. Hatua hiyo inatarajiwa kuhamasisha uzalishaji wa tumbaku nyingi zaidi na yenye kiwango cha juu zaidi cha ubora ili iweze kupata soko la uhakika na kuwa mchango wa ziada kama zao mbadala kwa uchumi wa Wakulima wa Kigoma. *(Makofi)*

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

(i) Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma kuanzia mpakani mwa Urambo; Vijiji vya Chagu, Lalanguru, Mtego wa Noti, Nguruka yote, Uvinza, Basanza njoo mpaka Kasulu huku maeneo ya Rungwe mpya na Ahsante Nyerere, wanalima tumbaku ya daraja la kwanza; na Tumbaku hii ni sehemu inayolipatia Taifa letu fedha nyingi za kigeni;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

Urasimu uliopo umesababisha Vyama vya Msingi kukopa wakulima hawa tumbaku yao na kuwalipa baadaye hasa maeneo ya Kagwa na Kalela kule Kasulu pia. Serikali katika mchakato huu inasemaje haina fedha wakati fedha za kigeni zinapatikana kutokana na tumbaku hii ili urasimu upungue pia kutokana na bei ya soko la dunia ili wakulima hao waweze kupata haki inayostahili kutokana na nguvu kazi wanayowekeza kwenye uzalishaji wa tumbaku hii? (Makofi)

(ii) Kwa kuwa hakuna Wataalamu wa kutosha na hasa wa Ushirika pamoja na wa Kilimo katika kuwasaidia wakulima hawa ili waweze kujiendeleza kutokana na zao hili la tumbaku; Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha wakulima hawa wanapatikana na siyo kwa Mkoa wa Kigoma tu, pamoja na Mkoa wa Tabora na hasa Wilaya ya Urambo? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kama tulivyosema, katika jumla ya uzalishaji wa nchi nzima wa tani kama laki moja na kitu, Kigoma inazalisha wastani kama wa tani 5,000 kwa Kanda ile ambayo inapakana na Wilaya ya Urambo na ni kweli kwamba, tumbaku inayozalishwa pale ni tumbaku ya daraja zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichosema ni kwamba, siyo kwamba Serikali haina fedha ya kuhudumia wakulima wa Tumbaku wa pale hapana; ilikuwa inakosa fedha ya kuanzisha Mkoa wa Kigoma kama Mkoa wa Tumbaku. Kwa hiyo, tumesema tutafanya hivyo na lengo lake ni kuutoa uzalishaji wa tumbaku kutoka kwenye tani kama 5,000 kwenda kwenye tani kama 20,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, uhamasishaji unaotarajiwa kufanyika pale ni kwamba, tunatarajia kwanza kupata Wataalamu wa Ugani, lakini kubwa zaidi kwenye zao la Tumbaku ni kuongeza *classifiers*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

ambao wataweza kudhibiti ubora wa zao la Tumbaku na hilo kwa sasa hivi ndiyo changamoto kwa maana ya uzalishaji kote. Tumekusudia kutoka *classifiers* 20 mpaka japo 30 katika miaka miwili ijayo na hilo ndiyo changamoto kubwa.

Na. 131

Taasisi za Utafiti na Wakufunzi wa Vyuo vya Kilimo Nchini

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa Wafanyakazi wa Taasisi za Utafiti na Wakufunzi wa Vyuo vya Kilimo nchini kwamba wanapojiendeleza kielimu toka ngazi moja kwenda nyingine hawaongezewi mishahara yao kulingana na ngazi mpya ya elimu waliyoipata:-

Je, Serikali inatoa maelezo gani ya kina juu ya malalamiko haya ya muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya mishahara kwa Watumishi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kama ilivyo kwa Watumishi wengine wa Serikali hutolewa kulingana na Miongozi na Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi za Kada husika.

Kwa mujibu wa Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 24 wa Mwaka 2002 kuhusu miundo ya utumishi ya kada zilizo chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Ibara ya (4) inaelekeza kwamba, Maafisa ambao watahudhuria mafunzo ya muda usiopungua mwaka mmoja na kutunukiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Shahada au Stashahada ya Uzamili (*Postgraduate Diploma* au *Masters Degree*) katika fani inayohusika na kazi zao, watapewa nyongeza mbili za mishahara kuanzia tarehe wanapopata sifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wengine hujiendeleza kwa madhumuni ya kupata sifa mpya za kubadilishwa ujuzi kutoka kada moja kwenda kada nyingine (*re-categorization*). Ili mtumishi aweze kubadilishwa cheo kwa misingi ya sifa hiyo mpya, ni lazima mwenyewe aombe kubadilishwa kada anayoitaka na iwepo nafasi (Ikama) ya cheo hicho na pia iwepo bajeti ya mishahara kwa nafasi ya cheo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni jukumu la mtumishi kuwasilisha taarifa na vyeti vya kuhitimu kwa Mwajiri mara baada ya kuhitimu masomo yake na kuomba kubadilishwa kada au kupewa nyongeza ya mishahara kwa mujibu wa sifa alizojiipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwepo na malalamiko kuhusu wafanyakazi kutoongezwa mishahara baada ya kujiendeleza kielemu. Hata hivyo, hali hiyo inatokana na ukweli kuwa, kasi ya wafanyakazi kujiendeleza kielimu haiendi sambamba na uwezo wa kibajeti wa kugharamia nyongeza ya mishahara hiyo na wakati huo huo kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia ajira mpya. Wizara yangu inaendelea kuwasilisha taarifa muhimu za watumishi kwenye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ili ishughulikie stahili zao kulingana na taratibu za Watumishi wa Umma na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Christowaja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikiri wazi kwamba, majibu ya Naibu Waziri yamenisikitisha sana. Kwa kweli ni majibu ambayo yanakatisha tamaa watumishi na wakufunzi. Mimi nilihitaji maelezo ya kina lakini nilichokipata ni *business as usual*. Sasa maswali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA]

(i) Kwa kukiri kwamba tatizo lipo na kwa Naibu Waziri kusema wazi kwamba kasi ya watumishi na wakufunzi kujiendeleza haiendi sambamba na uwezo wa kibajeti wa kugharimia nyongeza hiyo ya mishahara: Je, Naibu Waziri anataka kuwaambia watumishi na wakufunzi kwamba kelele zinazopigwa kila siku watumishi wajijendeleze ili kuweza kupata ujuzi, ufanisi na maarifa ya kufanya kazi zao sawa sawa ni kelele za chura? (*Kicheko/Makofi*)

(ii) Kama hali hii ya kibajeti haiendi sambamba na kulipa nyongeza za mishahara za watumishi na wakufunzi wanapojiendeleza; ni kwa nini sasa watumishi hawa na wakufunzi wamekuwa wakipewa ruhusa ya kwenda kujiendeleza kabla ya kuwaambia au kuwaeleza yatakayowapata baada ya kwenda shule ili waweze kufanya maamuzi sahihi badala ya kusoma na kupoteza muda na fedha bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba maelezo ya kina na siyo ya kejeli. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru! Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana. Wewe ni mtaalamu wa kujibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi, Mheshimiwa Christowaja anasema kuna *business as usual*. Nadhani labda katika majibu yangu hakunielewa. Nilichosema ni hivi, umuhimu wa wafanyakazi kujiendeleza uko pale pale. Kuna wengine wanajiendeleza kwa vibali kutokana na Idara zao husika na kuna wengine wanajiendeleza wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utaratibu wa *Civil Service* na maeneo mengine yote, wafanyakazi wote wanahamasishwa kujiendeleza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye kilimo labda niseme tu kwamba, hawa Maafisa wa Utaalamu tunaowazungumzia, wa ugani tu peke yao; mwaka 2007 tulipofanya tathmini katika jumla ya mahitaji ya wagani 15,000 tulikuwa na wagani 3,500 tu. Leo tuna wagani karibu 8,500 ambao wameongezwa katika Mfuko wa Serikali, wanalipiwa na Serikali na wanaendelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa upande wa wagani, tuna upande wa walimu, Sekta ya Afya na kadhalika. Ndiyo maana tukasema kwamba watu wanaruhusiwa kujiendeleza, wengine wanajiendeleza kwa upande wa Idara zao na wengine wanajiendeleza binafsi, lakini uwezo wa bajeti ndiyo unaoweza kuwabainishia kwamba wataongezwa mishahara. Hata hivyo, bado kwa sababu ya elimu yao wataendelea kupata stahili zao pale uwezo utakaporuhusu. Kwa hiyo, niliomba kuliweka wazi suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kusema kwamba kama bajeti hairuhusu watu wasiruhusiwe kujiendeleza, mimi nadhani *this is a wrong position*. Tunachosema ni kwamba, kujiendeleza kwa binadamu au kwa mfanyakazi ni jambo zuri la kawaida. Kwa hiyo, tunawahimiza wafanyakazi kwenye kilimo na Sekta nyingine wajiendeleze na kama Serikali kwa jinsi tunavyozidi kupata uwezekano, tutarejea wale waliojiendeleza na kuwapandisha katika ngazi zao stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleweke kwamba, huo ndiyo msimamo wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

Na. 132

Matibabu ya *Fast Track*

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeruhusu matibabu ya "*Fast Track*" katika baadhi ya hospitali hapa nchini:-

Je, kuna Sera au Sheria yoyote inayoelekeza kutolewa kwa huduma hiyo katika hizo hospitali hasa Hospitali za Rufaa kama Muhimbili?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuwepo huduma ya afya kwa wananchi wote, Serikali ilianzisha huduma ya *fast track* katika Hospitali ya Taifa Muhimbili chini ya Mwongozo wa Mwaka 1997, unaoruhusu Hospitali za Serikali kuanzisha huduma hizo.

Madhumuni ya kuanzisha huduma ya *fast track* ni kutafuta njia za kuongeza mapato ya hospitali angalau asilimia 40 ya mapato yake, ikiwa pamoja na:-

(i) Kutoa motisha kwa wataalam wa afya wanaotoa huduma hiyo badala ya kutoka nje ya kituo na kwenda kufanya kazi katika hospitali binafsi; na

(ii) Kuongeza mapato ya hospitali ili kuboresha huduma kwa watu wote hasa wale wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, Madaktari wamekuwa wakipata motisha na kuendelea kutoa huduma katika Hospitali ya Muhimbili na pia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

wagonjwa wasio na kipato wamekuwa wakifaidika kwa kupata vifaa na dawa, kutokana na fedha zinazotokana na tiba hiyo ya *fast track*.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kusikitika kutokana na hii huduma ya *fast track* kwa kusema kwamba, majibu ya msingi yanasema kwamba hii ni kuongeza posho. Juzi juzi hapa tumeona madaktari walivyoongezewa mishahara minono tofauti na kada nyingine za Utumishi.

(i) Wanasema kwamba, kutoa motisha kwa wataalamu wa afya wanaotoa huduma hiyo badala ya kutoka nje ya vituo. Je, ni kweli motisha hii inawafanya madaktari wasitoke nje ya vituo na kwenda kufanya kazi kwenye vituo vingine? (*Makofi*)

(ii) Ni kweli wagonjwa wasiokuwa na kipato wamekuwa wakipata huduma za vifaa mbalimbali kama dawa kutokana na fedha hizo? Je, ni kweli asilimia hiyo inaingia huko wakati hiyo fedha ni asilimia fulani inaenda kwa Daktari, asilimia fulani inaenda kwa *Nurse* anayemhudumia mgonjwa na asilimia kidogo inabaki hospitali? Naomba majibu mazuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana muda wetu umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, wote tuelewe kwamba huduma tunazozitoa kwenye hospitali zetu zote nchini, zinatolewa katika kiwango ambacho kuna upungufu sana na changamoto zikiwa nyingi. Naomba tuelewe tu gharama za uendeshaji na hasa uwepo wa teknolojia mpya, umeongeza gharama za uendeshaji na gharama za mahitaji

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

pamoja na uhitaji wa watumishi, vifaa, vitendea kazi na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano tu, gharama ya kufanyia *service* mashine moja tu kwa mfano ya *CT-Scan*, unahitaji takriban shilingi milioni 140 kwa mwaka au kufanyia *service* mashine ya *MRI* unahitaji karibu takribani shilingi milioni 240 kwa mwaka. Hiyo ni *service* na siyo kununua au kufanya ukarabati. Kwa tafsiri hiyo, tumekuwa na mbinu mbalimbali za kuongeza mapato katika huduma zetu za tiba; moja ni kuwapa motisha watumishi na ni kweli kwamba tunatoa asilimia 50 ya pato lake kwa ajili ya kuwapa watumishi.

Vilevile tunalipa *house allowance* na *leave allowance* kwa pale Muhimbili na vilevile fedha hizo hutumika katika ku-*maintain* na kutoa *service* za vifaa vyake.

Katika tafsiri hiyo, mchango wa *fast track* kwa hakika ni mzuri na kwa kiwango kikubwa karibu asilimia 51 ya mapato yote Muhimbili yametokana na huduma hii ya *fast track*. Kwa hiyo, tunasema ni huduma nzuri na ambayo tunategemea kama tutaweza kufikia katika lengo la kubadilisha na kufanya Watanzania wote kuwa wanachangia Bima ya Afya au wanakuwa Wanachama wa Bima, katika tafsiri hiyo, hata huduma hii ya *fast track* inaweza ikafa yenyewe kwa sababu kila mtu ambaye atafika kwenye vituo vyetu vya tiba atakuwa tayari ni Mwanachama wa Bima na kwa hiyo Bima itakuwa tayari kumlipia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mheshimiwa Mama Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa *fast track* inalenga kuharakisha utoaji wa huduma; na kwa kuwa Mpango wa Maendeleo ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARGARET S. SITTA]

Afya ya Msingi nao unalenga katika kuharakisha kutoa huduma kwa wananchi: Je, Serikali ipo tayari kuharakisha zoezi la kufundisha watoa huduma za afya katika jamii na maeneo mengi ikiwemo Urambo ambako Zahanati nyingi zimejengwa lakini hazina wafanyakazi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, jibu lake ni rahisi tu, ndiyo au hapana, basi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli watoa huduma za afya vijijini ni watu muhimu na tunawahitaji na tayari Serikali ilishaanzisha mpango huu wa majaribio pale Ifakara, ambapo tunawachukua vijana waliomaliza Kidato cha Nne wanapata mafunzo ya huduma hizi za afya vijijini na baada ya hapo wanaenda kufanya kazi katika maeneo ya vijijini wakiwa tayari katika mfumo ambao wanaweza wakajijendeleza baadaye. Kwa hiyo, Serikali itaangalia na kuona namna gani huduma au mpango huu unaweza ukasambaa nchi nzima.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali letu la mwisho, Mheshimiwa Capt. John Chiligati!

Na. 133

Huduma ya Maji kwa ajili ya Treni katika Stesheni ya Saranda

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI aliuliza:-

Treni zote za Shirika la Reli ziendazo bara hupata huduma ya maji katika Stesheni ya Saranda (Manyoni); na maji hayo hutoka katika chemchemi iliyopo Kijiji cha Hika ambapo mabomba yanayosafirisha maji hayo yamechakaa sana:-

(a) Je, ni lini mabomba hayo yatakarabatiwa ili kuzuia upotevu mkubwa wa maji yanayovuja njiani?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI]

(b) Je, kwa nini Shirika la Reli halioni umuhimu wa kuweka vituo vya wananchi kupata huduma ya maji katika vijiji vinavyopitiwa na bomba hilo hasa Hika, Ilaloo na Saranda?

(c) Je, kwa nini Shirika hili halisaidii maendeleo ya Kijiji cha Hika katika Sekta ya Elimu, Afya na Maji kwa kuwa ndiyo walenzi wa chemchemi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Bomba la maji linaloanzia Hika, kwa sasa lipo katika hali nzuri baada ya kufanyiwa ukarabati mwezi Novemba, 2012.

(b) Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) inauona umuhimu wa kuweka vituo vya wananchi kupata huduma ya maji katika Vijiji vya Hika, Ilaloo na Saranda ingawa sababu zifuatazo zimeathiri nia hiyo:-

(i) *TRL* haijaweka gati la kuchotea maji katika Kijiji cha Hika kilipo chanzo cha maji, yaani chemchemi hiyo, kwa sababu maji hayawezi kuwa na nguvu ya kupanda juu ili yaweze kutoka kwenye bomba la wima (*stand pipe*) kwa kuwa vyote vipo katika usawa mmoja.

(ii) *TRL* iliweka bomba la kuchotea maji katika Kijiji cha Ilaloo na wanakijiji waliliharibu muda mfupi baada ya kuwekwa kwake. Tunashauri Serikali ya Kijiji itoe elimu kwa wanakijiji hao kwanza kabla ya kurudisha tena bomba. Aidha, walichukulie bomba hilo kuwa ni mali yao na kwamba linahitaji kutunzwa na kulindwa.

(iii) Huduma ya maji inatolewa kwa wananchi na mifugo katika Kijiji cha Saranda. Wanakijiji wawili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI]

wameunganishiwa maji kwa gharama ndogo. Aidha, Kampuni imeagizwa kufunga bomba kwenye Zahanati ya Saranda haraka iwezekanavyo ili huduma ya maji iweze kutolewa mara moja.

(c) *TRL* ina nia thabiti ya kusaidia Kijiji cha Hika kutoa huduma za jamii katika Sekta za Elimu, Afya na kadhalika, bali hali ya kifedha siyo nzuri, kwani utendaji wa kampuni umeshuka sana. Hali hii inapelekea mapato ya kampuni kushuka kiasi cha kutokidhi kumudu gharama za uendeshaji. Huduma za kijamii zitaanza kutolewa na *TRL* pale mizania yake itakapokuwa mizuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chiligati.

MHE. CAPT. JOHN. Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya kutia moyo ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Nataka tu kujua, ni lini sasa Shirika la Reli litajenga tenki pale Hika ili Kijiji cha Hika kipate maji kwa sababu wao ndiyo wanaolinda ile chemchemi? Sio Hika tu, pamoja na Wanailaloo; pamoja na kwamba elimu itatoka, lakini vilevile ni lini watajenga vituo angalau viwili au vitatu badala ya kimoja kile ambacho wananchi wanagombania mpaka kinaharibika na vilevile pale kwenye Zahanati ya Saranda lini wataweka maji? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa Stesheni ya Saranda, pamoja na kwamba treni zinapata maji pale, lakini vilevile wananchi wa Saranda wanatoa huduma ya chakula, panaitwa *Hilton Hotel* pale; chakula kile kinatolewa katika mazingira ya jua na vumbi:-

Je, Shirika la Reli na Wizara kwa ujumla watakuwa tayari kushirikiana na wananchi wa Saranda kujenga vibanda vizuri vya kulia chakula ili kuimarisha ajira za Wanasaranda na wasafiri wapate mahali pazuri pa kulia chakula? (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana, muda wetu umekwisha. Kwa hiyo, usile muda wangu kwa kueleza mambo mengi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Capt. John Chiligati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ameuliza lini tanki litajengwa katika Kijiji cha Hika? Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kwa kweli kwa sasa hali ya kifedha ya Shirika letu siyo nzuri kiasi kwamba wajibu wake kwa jamii umeshuka kidogo. Tunadhani kwamba mara litakapokuwa na mizania mizuri, *then* huduma hizi zitatolewa.

Nimesema katika jibu la msingi kwamba, kufungwa kwa bomba la maji kwenye Zahanati ya Saranda ambayo inatoa huduma kwa wananchi pale kutafanyika mara moja. Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho kitafanyika lakini tusbiri hali itakapokuwa nzuri tutaweka na miundombinu mingine katika Kijiji cha Hika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya swali la nyongeza; ni kweli huduma za chakula zinatolewa pale na maeneo mengi ya stesheni zetu hayapo katika hali nzuri. Programu iliyopo ya ufufuaji wa Reli ya Kati itahusisha pia kufufua vituo vyote vya treni kuanzia Dar es Salaam mpaka Mwanza, Kigoma na maeneo mengine. Tuombe Mungu jambo hilo litakapotekelezwa, mambo yatakuwa mazuri.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha na muda wetu umekwisha. Sasa nitatangaza wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Wageni sita wa Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo, wakiongozwa na Ndugu Aida Jacob Isidori; karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Wageni 44 wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya TAMISEMI, ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI]

Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya; karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Philipo Mulugo, ambaye ni Mwalimu Gerald Sadala; karibu sana.

Wageni wa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi - Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka, ambao ni Mheshimiwa George Katemelo - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba na Ndugu Marwa Gekondo - Afisa Elimu Sekondari; karibuni sana *(Makofi)*

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo: Wanachama 45 wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT). Karibuni. Naona wapo *basement* kutokana na ufinyu wa nafasi ndani ya Bunge. Karibuni sana Waheshimiwa.

Sasa nitawaomba wale waliowaleta wawapeleke kwenye chai, ndiyo muda wa chai huu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi. Mheshimiwa Lembeli - Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anawatangazia Wajumbe wake kwamba, leo tarehe 17 Desemba, 2013, saa 8.00 mchana, kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa *St. Gasper Hotel*. Usafiri utakuwepo kuanzia saa 7.15 ndani ya Viwanja vya Bunge.

Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, anawatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba, kutakuwa na kikao leo tarehe 17 Desemba, 2013, saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 231, Jengo la Utawala wa Bunge. Nawashukuru sana.

Katibu, hatua inayofuata!

HOJA ZA KAMATI

Taarifa za Kamati za Bunge za Uchumi, Viwanda na Biashara na Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika Taarifa hizo

MWENYEKITI: Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara!

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara. Taarifa hii iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, kwa kipindi cha Februari hadi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema. Aidha, kwa niaba ya Kamati yangu, nichukue fursa hii kumtakia pole Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, ambaye anaendelea kupata matibabu nchini Afrika Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, naomba nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, kwa mchango wao mkubwa uliofanikisha kutekeleza shughuli za Kamati na pia kwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa – Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula – Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga, Mheshimiwa Ester

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)
Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Hussein Nasser Amar, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa David Zakaria Kafullila, Mheshimiwa Vicky Pascal Kamata, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Shawana Bukhet Hassan, Mheshimiwa Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa Josephine Jonson Genzabuke, Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mheshimiwa Eng. Habib Juma Mnyaa na Mheshimiwa Hilaly Khalfan Aeshi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, endelea usiwatambue hao Wajumbe wako, mlishatambuana huko mlilotoka. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kama yalivyotamkwa katika Nyongeza ya Nane chini ya Kanuni ya 118, Sehemu ya Pili 6(1), Kanuni za Bunge zinatamka wazi kuwa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara itasimamia Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Kamati inafanya mambo yafuatayo:-

Kupitia Bajeti ya Wizara inazosimamia; kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosimamia; na kushughulika Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo na kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa ufupi Kamati hii inashughulikia sekta muhimu sana katika ukuaji na ustawi wa nchi yetu. Sekta hizo ni Sekta ya Benki, Biashara, Bima, Viwanda, Uwekezaji na Uwezeshaji.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yetu itajumuisha Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Fedha ambayo ina Taasisi 37 na Wizara nyingine ni Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ina Taasisi 19 na Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezeshaji na Uwekezaji ambayo ina Taasisi nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara inazosimamia; Kamati ilipata fursa ya kupitia utekelezaji wa Bajeti wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji, kwa mwaka 2012 na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka 2013/2014.

MWENYEKITI: Waheshimiwa mnaotoka nje tunaomba utulivu, tafadhali!

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika robo ya mwaka, utekelezaji wa majukumu wa Wizara hizo kwa ujumla siyo wa kuridhisha sana hususan kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezeshaji na Uwekezaji na Wizara ya Viwanda na Biashara katika maeneo ya uwezeshaji na uwekezaji. Hii inatokana na kupata fedha kidogo tofauti na mahitaji halisi ya sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kuchambua Muswada wa Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2013. Kwa kuzingatia maudhui ya Muswada huu, Kamati imeridhika kwa dhati kabisa kuwa upungufu uliojitokeza katika Sheria inayotumika sasa ni mkubwa ambao kwa kiasi kikubwa umekuwa chanzo cha uchumi wetu imara kukosa takwimu bora kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa takwimu ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki ambacho nchi yetu inapitia kipindi kigumu cha mapinduzi ya kiuchumi na kisiasa. Pamoja na hatua kubwa ya maendeleo ya sayansi na teknolojia hususan katika fani ya mawasiliano; hivyo basi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
Kamati ingependa kutoa pongezi nyingi kwa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Takwimu, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina imani kuwa iwapo Muswada huu utafanyiwa kazi mapema na hatimaye kuwa Sheria, basi itasaidia sana katika uendeshaji wa kitengo hiki muhimu cha takwimu na nchi yetu kwa ujumla. Hivyo basi, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba Bunge lako Tukufu liweke katika ratiba Muswada huu ambao tayari umeshafanyiwa kazi na Kamati ili uweze kupita katika hatua zilizosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kushughulikia Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji (*The SADC Protocol on Finance and Investments*), ambayo ilitiwa saini na Wakuu wa Nchi Wanachama tarehe 18 Agosti, 2006 Mjini Maseru, Leshoto. Mpaka sasa kati ya nchi 14, tayari Mabunge ya nchi 11 Wanachama wa *SADC* yameridhia Itifaki hiyo. Nchi tatu ambazo bado ni Zimbabwe, Shelisheli na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, napenda kukuomba kwa dhati Itifaki hii ipewe kipaumbele na Bunge lako Tukufu ili iweze kuwekwa katika ratiba ya Mkutano wa Bunge ujao ili iweze kujadiliwa na hatimaye kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa za utendaji wa Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Mamlaka ya Bima Tanzania, Shirika la Bima Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na *Consolidated Holding Company (CHC)*. Taasisi nyingine zilizowasilisha Taarifa za Utendaji ni Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi (*GEPP*), *PSPF*, *PPF*, *Dar es Salaam Stock of Exchange*, *Tanzania Gambling Board* na *Twiga Bancorp*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika azma ya Serikali kuhakikisha kuwa huduma za benki zinawafikia wananchi wengi walio maskini wanaoishi mijini na vijijini, bado kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
tatizo la kutopatikana kwa mikopo kwa urahisi. Kati ya benki 51 tulizonazo ni benki mbili tu za *National Microfinance Bank (NMB) na CRDB* ndizo zimekuwa na matawi katika ngazi za Wilaya. Mtandao huu wa kibenki unawanyima wananchi wanaoishi vijijini fursa ya kupata mikopo.

Aidha, matatizo ya riba kubwa ambayo yamefikia hadi asilimia 25%, kukosekana dhamana kwa wanaokopa, Watanzania wengi kuogopa mikopo, yameshika hatamu katika kukwamisha wananchi kupata mikopo itakayowakwamua kiuchumi. Serikali inashauriwa kufanya kila liwezakanalo ili kuhakisha kuwa inafanya mageuzi makubwa katika Sekta ya Benki nchini ili Taasisi hizo ziweze kutoa mikopo ya kutosha kwa wananchi na hatimaye waweze kujikwamua na kutoka katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kusikia takwimu za waliokopa benki kuwa ni 773,158 hadi kufika mwezi Machi mwaka huu, 2013 ambapo walikopa jumla ya TZS Trilioni 8.7; kiasi hiki ikilinganishwa na mahitaji ya kiuchumi na idadi ya watu iliyofikia 44,928,923 (Sensa ya 2012).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Taasisi ya *Twiga Bancorp Ltd* ambayo ilisajiliwa mwaka 1992 chini ya Sheria ya Makampuni (*Companies Ordinance, CAP 212*) kwa jina la *National Bureau De change Ltd*. Makao Makuu ya Taasisi hii yapo Dar es Salaam. Taasisi hii ina matawi sita; kati ya hayo matatu yako Jijini Dar es Salaam na yaliyobaki yako Dodoma, Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kufanya vizuri katika soko la kibenki, Taasisi hii ina mtaji mdogo ambao hautoshelezi katika ushindani pamoja na kupata leseni kutoka Benki Kuu ili iweze kuwa benki kamili ya biashara. Benki Kuu ya Tanzania imeweka masharti mbalimbali ili kukidhi vigezo vya Taasisi kuitwa Benki ya Biashara. Sharti mojawapo ni kuwa na mtaji wa shilingi bilioni 15 wakati *Twiga Bancorp* hivi sasa ina mtaji wa shilingi bilioni 7.8 na kuwa na upungufu wa shilingi bilioni 7.2.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa sana na kushamiri kwa matumizi ya Dola ya Kimarekani badala ya Shilingi ya Tanzania katika uchumi wetu. Tatizo hili ni kubwa sana na linachangia kwa kiasi kikubwa katika kuporomosha thamani ya Shilingi ya Tanzania. Matangazo mengi ya ulipaji wa huduma na bidhaa hapa nchini yamewekwa kwa fedha za kigeni, kitendo ambacho ni kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uendeshaji wa maduka ya kubadilishia fedha (*Bureau de Change*) maduka hayo hayatakiwi kufanya shughuli nyingine yoyote zaidi ya kubadilishia fedha za kigeni. Katika uchunguzi wa Kamati imebainika kuwa kuna baadhi ya maduka hayo yanajihusisha na shughuli za kuhamisha fedha kwenda nchi nyingine.

Maduka haya yanatumika kama uchochoro wa kutorosha fedha nje ya nchi na kupelekea kupotea kwa mapato ya Serikali na pia kusababisha fedha yetu kushuka thamani. Tatizo lingine maduka mengi hayatoji risiti kwa fedha iliyozwa au iliyonunuliwa na kwamba hawadai vielelezo muhimu kama vile pasi ya kusafiria na vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006. Sheria hii inasema bayana kuwa, Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa malipo ya bidhaa na huduma hapa nchini (*legal tender*). Pia Kamati inashauri Serikali kuwachukulia hatua za kisheria wamiliki wote wa maduka wanaokiuka taratibu za leseni zao na kuongeza usimamizi zaidi katika maduka hayo katika kukomesha tatizo hilo ambalo likiachwa kwa visingizo vya soko huru linaweza kuleta madhara makubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Uzoefu wa nchi nyingi kama Afrika Kusini, Kenya na Ethiopia unaonesha kuwa huwezi kupata fedha za kigeni kama hujaonesha kitambulisho na pasi ya kusafiria unapohitaji fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na viashiria vyote vya Kimataifa vinavyotumika kuchambua Deni la Taifa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
kuonesha kuwa Deni la Tanzania linalofikia Dola za Kimarekani milioni 12,744.3 kufikia Septemba, 2013 ni vumilivu katika muda wa kati na muda mrefu, bado hatua madhubuti zinahitajika katika kuhakikisha kuwa deni hilo linakuwa katika viwango vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazoshauriwa na Kamati ni kuendelea kuwa waangalifu katika ongezeko la deni hilo, kuhakikisha kuwa mikopo inawekezwa katika uzalishaji na Serikali ikope kwa kuzingatia ushauri na matakwa ya kiuchumi kwa uwazi, kabla ya mkopo, mchanganuo wa maombi ya mkopo yawasilishwe Bungeni yakionesha riba, muda na Taasisi au nchi inayokopwa pamoja na masharti na matakwa mengine. Pia kuyataka Mataifa tajiri, *creditors*, kutusamehe madeni yetu ili tuweze kutumia kiasi hicho cha msamaha kuwekeza katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato ya Serikali yanayotokana na Kodi Nchini: tarehe 26 Agosti, 2013 na tarehe 22 Oktoba, 2013 Kamati ilikutana na Mamlaka ya Mapato nchini (*TRA*), ili kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Mamlaka ya Mapato nchini. Kamati inaipongeza kwa dhati Mamlaka ya Mapato nchini hususan katika kuleta mfumo mpya wa ukusanyaji wa kodi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki. Mifumo ya kielektroniki ambayo *TRA* wameweza kuitekeleza ni pamoja na mfumo wa utoaji wa mizigo unaojulikana kama *TRA Cargo Management System - CMS*, mashine za kielektroniki zinazojulikana kama *Electronic Fiscal Devices - EFD*, mfumo wa kulipia leseni za magari kwa kutumia *M-pesa, Tigo pesa, Airtel Money, MaxMalipo* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo Kamati bado haijaridhika nayo ambayo yamekuwa kikwazo katika ukusanyaji wa kodi hapa nchini. Mambo hayo ni pamoja na Tanzania kuongoza kuwa na misamaha mingi ya kodi hapa nchini (3.1% ya Pato la Taifa) ikilinganishwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
na nchi nyingi za Afrika Mashariki kama Kenya ambayo ni 1% ya Pato la Taifa na Uganda 0.4% ya Pato la Taifa.

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kupunguza misamaha hiyo ili kufikia angalau asilimia moja ya Pato la Taifa kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (*FYDP-1*). Aidha, Kamati ingependa kupata taarifa ya kwa nini marekebisho ya Sheria ya VAT ya 1997 kwa minajili ya kupunguza misamaha ya kodi haijawasilishwa Bungeni licha ya mchakato wake kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kuongezeka kwa bandari bubu ambazo zimekuwa zikitoa mianya mikubwa ya kuingizwa bidhaa nchini bila kutozwa kodi wala kukaguliwa kwa maana ya ubora. Tatizo la bandari bubu na njia nyingine za uingizaji wa bidhaa zinazojulikana kama njia za panya zimekuwa tishio kwa uchumi wetu, ajira ya vijana wetu pamoja na amani yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matumizi ya vifaa vya elektroniki katika kutoa risiti limekuwa ni tatizo kwa watumiaji wa vifaa hivyo na kusababisha maduka kufungwa kufuatia migomo iliyotokea katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro na Dar es Salaam. Wafanyabiashara wanalamikia bei kubwa ya vifaa hivyo ikilinganishwa na bei ya kununulia vifaa hivyo katika nchi za China na Dubai.

Aidha, wafanyabiashara wanalamika kuwa vifaa hivyo vinaandika bei ya juu ukilinganisha na bei halisi. Kufuatia ukubwa wa tatizo hilo, tarehe 9 Novemba, 2013 Mbunge wa Mbozi Mashariki alitaka kupewa maelezo ya Serikali kuhusiana na vifaa hivyo kuuzwa kwa bei kubwa kuliko vinavyonunuliwa. Takribani wiki moja baada ya hoja hiyo kutolewa Bungeni, wafanyabiashara katika Jiji la Dar es Saalaam nao waligoma. Ili kupata ufahamu wa jambo hilo, Kamati yangu tarehe 18 Novemba, 2013 iliwaita wahusika kutoka Mamlaka ya Mapato Nchini wafike mbele ya Kamati ili Kamati iweze kupata ukweli wa ndani wa jambo hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kwamba, Mamlaka ya Mapato nchini wamefanya hivyo katika kuboresha makusanyo ya kodi kwa kutumia njia za kisasa za *TEHAMA*. Mamlaka ya Mapato Nchini ilianzisha utaratibu wa kutumia mashine za kielektroniki (*Electronic Fiscal Devices - EFD*) katika kutoa risiti za ankara za kodi badala ya kutumia vitabu.

Utaratibu huu ulianza kutumika katika nchi za Italia, Bulgaria, Serbia, Rwanda na Ethiopia. Nchi nyingine ambazo zinatumia utaratibu huo ni Kenya na Malawi. Mashine hizo husaidia katika kusimamia kodi kwa kutolea risiti na ankara za kodi na kutunza kumbukumbu sahihi za mfanyabiashara kwa muda wa zaidi ya miaka mitano. Walengwa wa kutumia mashine hizi ni wafanyabiashara wakubwa wenye mitaji ya kati ya shilingi milioni 14 namilioni 40. Mfano ni wamiliki wa maduka ya vipuri, mawakili, maduka ya jumla, wafanyabiashara wakubwa wa mbao, migahawa mikubwa, maduka ya simu na vipuri vyake, baa za vinywaji baridi, studio za picha, wauzaji wa pikipiki na maduka makubwa ya nguo. Kwa nchi nzima walilengwa wafanyabiashara laki mbili tu kati ya wafanyabiashara zaidi ya milioni moja na nusu. Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikilalamikiwa juu ya bei kubwa ya ununuzi wa mashine za *EFD*, mchakato wa ununuzi wa *EFD*, walengwa wa *EFD* na gharama za matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya *TRA* gharama za mashine hizo zinajumuisha mambo yafuatayo; gharama za ubadilishaji wa fedha, yaani *exchange rate*, kodi ya ushuru wa forodha, gharama za usambazaji na gharama za uendeshaji wa biashara. Yote haya yanafikisha gharama za mashine kuwa kati ya Shilingi za Kitanzania 600,000 na 778,377.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumaliza tatizo hilo, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

lundwe tume huru ya kuchunguza uhalali wa bei ya vifaa hivi ili haki iweze kutendeka na kwamba, endapo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)] itabainika kuwa kulikuwa na udanganyifu wa bei, wahusika wote walioshiriki katika mchakato wa manunuzi wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi Na. 7 ya Mwaka 2011. Aidha, Serikali iondoe kodi kwenye vifaa hivyo na Tume hiyo ipendekeze bei mpya kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa fedha za *Commodity Import Support* bado hazijarejeshwa zote. Fedha hizo ambazo wafanyabiashara walikopa kutoka Mfuko wa Kuwezesha Uagizaji Bidhaa kutoka nje ya Nchi zilizotolewa na Denmark, Japan, Norway, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza na Uswisi.

Fedha hizo ambazo zilikusudiwa kununulia malighafi za viwanda, vyombo vya usafiri wa barabara na vifaa vya kilimo na ujenzi kati ya mwaka 1980 na 2000, hazikutumika ilivyotakiwa. Hivyo basi, wale wote ambao hawajazirejesha, Serikali iwaagize wafanye hivyo na wale ambao watahinda hatua stahiki zichukuliwe haraka iwezekanavyo. Hali ya ukusanyaji wa madeni hayo hairidhishi kabisa. Kwa mfano; taarifa ya madeni yaliyokusanywa hadi kufikia Mwezi Juni, 2013 ni kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka wa Fedha wa 2008/2009 jumla ya Sh. 1,982,692,223.98 zilikusanywa; 2009/2010 jumla ya Sh. 1,497,168,690.30 zilikusanywa; 2010/2011 jumla ya Sh. 718,92,994.92 zilikusanywa; 2011/2012 jumla ya Sh. 520,657,190.78 zilikusanywa na mwaka wa Fedha wa 2012/2013 jumla ya Sh. 19,172,000.00 zilikusanywa. Kamati inaiomba Serikali kuzidisha juhudi za ukusanyaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Kamati imelipa uzito mkubwa ni ukuaji wa Sekta ya Bima nchini. Kamati ilikutana na Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Bima Nchini inayojulikana kama *TIRA* na Shirika la Bima la Taifa (*National Insurance Company - NIC*) ili kupata taarifa ya changamoto mbalimbali ambazo Sekta hii inazikabili katika kuchangia kwenye Pato la Taifa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kulifanyia marekebisho Shirika la Bima nchini ambalo lilikuwa limekufa na sasa linaonesha dalili za kufufuka. Aidha, Kamati ingependa kuona Serikali inaingilia kati katika kushughulikia matatizo sugu ambayo yanalikabili Shirika hilo. Matatizo yaliyoainishwa katika taarifa ya utendaji iliyowasilishwa mbele ya Kamati ni pamoja na migogoro ya kesi za nyumba za Bima zilizouzwa ambayo ni ya muda mrefu. Nyumba hizo ziliuzwa kwa wanunuzi mbalimbali, hata hivyo, baadhi ya wapangaji waliamua kwenda Mahakamani wakipinga kuhama kutoka kwenye nyumba hizo. Watu walionunua nyumba hizo wanaendelea kulitoza riba Shirika la Bima kwa kutowakabidhi nyumba hizo kwa mujibu wa masharti ya mikataba ya ununuzi ilivyosainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu kutoka Mamlaka ya Bima Nchini zinaonesha kuwa, mwaka 2012 mchango wa sekta hiyo ulikuwa sawa na asilimia 0.9. Takwimu hizo pia zinaonesha kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 idadi ya makampuni yaliyoandikishwa kufanya biashara hiyo hapa nchini yalikuwa 29. Katika hayo, makampuni 22 yaliandikishwa kufanya biashara za Bima ya kawaida pekee, wakati makampuni matatu yanafanya Bima za kawaida na za maisha. Pia Mamlaka ya Bima nchini ilisajili madalali (*Insurance Brokers*) 84, Mawakala wa Bima (*Insurance Agents* 453) na Wakadiriaji Hasara (*Loss Adjuster and Assessors*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hakuna Sera ya Bima ambayo ingeongoza mageuzi ya Bima yafanyike katika viwango vinavyotakiwa. Utafiti unaonesha kuwa Serikali ikichukua hatua madhubuti Sekta ya Bima inaweza ikachangia kwenye Pato la Taifa kati ya 3% hadi 5%. Hatua ambazo zinashauriwa na Kamati ni pamoja na kuanza kutekeleza mpango wa kuratibu shughuli za Bima kwa kutumia *TEHAMA* ili kuongeza mapato ya Bima ambayo yanapotea kwa kiasi kikubwa kutokana na matumizi ya bima bandia hapa nchini na watu wengi kutopenda kukata bima za magari kwa mujibu wa Sheria.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupanua wigo kwa watu wenye kipato cha chini, Serikali inashauriwa kuandaa upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi walio wengi. Utafiti uliofanywa na Mamlaka za Bima Nchini umebaini kiwango cha matumizi ya huduma za bima bado ni kidogo, ambapo ni asilimia 19 tu ya Watanzania ndiyo wanaoutumia huduma hizo. Vilevile, utafiti huo umebaini kwamba, uhitaji wa huduma ndogo ndogo za bima ni mkubwa na upatikanaji wa huduma hizo utasaidia katika juhudi za Serikali za kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati sasa ambapo mali za Serikali hususan magari na nyumba zinapaswa zivekewe bima ili ziwe katika mfumo wa kisasa. Mali za Serikali zikiwa na bima itasaidia kupunguza hasara ambayo Serikali inapata baada ya magari yake mengi kuibiwa na kuharibika kutokana na ajali zinazotokea mara kwa mara. Majanga ya kuungua kwa nyumba za Serikali yamekuwa yakiongezeka katika siku za hivi karibuni kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, fidia za malipo kwa wahanga wa ajali za magari ya Serikali zimekuwa hazina utaratibu maalum. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha kuwa ufahamu wa wananchi katika mambo ya bima ni mdogo sana. Suala hili limesababisha wananchi wengi kulichukulia suala hili kama anasa zaidi kuliko kuwa mkombozi wao katika kupambana na majanga makubwa ambayo yanaweza kuwasababishia umaskini. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua madhubuti katika kuuelimisha Umma wa Watanzania juu ya faida za bima katika kukabiliana na majanga.

Aidha, Serikali inashauriwa kujadiliana na Vyuho Vikuu mbalimbali hapa nchini ili viweze kutoa mafunzo ya bima kwa ngazi mbalimbali pamoja na kozi za *Acturial Science* ili kuongeza Wataalam wa Bima nchini ambao watakuwa chachu katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Bima inaleta mchango mkubwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakipongeza Chuo cha Usimamizi wa Fedha kwa kuendesha mafunzo ya bima nchini kwa muda mrefu. Kozi hizi pia zilikuwa zikitolewa na Chuo cha Bima, Jijini Dar es Salaam kabla Serikali haijakabidhi majengo yake kwenye Taasisi nyingine ya Serikali. Kamati inashauri Mamlaka ya Bima Nchini ianzishe Chuo chake ili kuziba mapengo ya wataalam yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Takwimu ya Taifa imepewa majukumu ya kuendesha na kusimamia shughuli zote kitakwimu nchini kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu, Sura ya 35. Aidha, kuna Bodi ya Ushauri ya Ofisi ya Takwimu ambayo jukumu lake kubwa ni kumshauri Waziri wa Fedha kuhusu masuala ya kisera na kimkakati katika kuendesha shughuli hii. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua za kuboresha ofisi hii katika siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Takwimu ya Taifa ilikuwa ikiendeshwa katika jengo bovu Sana. Kwa sasa hali imekuwa bora kwani pamoja na mambo mengine, tovuti yao imesheheni takwimu bora ambazo zimekuwa msaada katika maendeleo. Pamoja na mafanikio hayo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inakabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi Makao Makuu na katika Ofisi mikoani. Kamati inashauri ofisi hii ipatiwe wafanyakazi wa kutosha hususan baada ya Muswada wa Sheria ya Takwimu 2013 kupitishwa katika hatua zote. Endapo Sheria mpya ya Takwimu itapata baraka zote zinazotakiwa, ofisi hii itaboreka zaidi na kuwa huru pamoja na kuwa na kasma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee sasa suala la mashirika yaliyobinafsishwa. Tangu Sera ya Ubinafsishaji ianze kutekelezwa na Serikali mwaka 1993, jumla ya mashirika 274 yamebinafsishwa. Kati ya mashirika hayo; 95 yapo katika Sekta ya Kilimo, 94 Sekta ya Viwanda, 23 Miundombinu, 34 Maliasili na Utalii, 15 Sekta ya Nishati na Madini na 13 kutoka sekta nyingine. Hadi kufikia Desemba, 2012 jumla ya mashirika 28 yalikuwa katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji na *New Africa Hotel* na *National Bank of Commerce* yamo katika kundi hili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya *Consolidated Holding Company (CHC)*, hadi kufikia Desemba, 2012 kulikuwa na mashirika au vitengo 12 ambayo yalikuwa katika hatua mbalimbali za urekebishaji. Kwa mfano, *National Insurance Corporation (NIC)*, *General Tyre East Africa Limited* na *Tanzania Posts Cooperation (TPC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *Consolidated Holding Company (CHC)* ambalo lilijulikana kama *NBC Holding Corporation* ni taasisi ambayo ilipewa mamlaka kisheria na Bunge kuchukua majukumu ya mashirika yote yaliyofikia ukomo wake kama vile *PSRC*, *LART*, *ATHCO* na *SIMU 200 LTD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mashirika yaliyobinafsishwa, ni mashirika machache (yasiyofika 10) ndiyo yanauza hisa zake katika Soko la Mitaji nchini. Tatizo hili limesababisha wananchi wengi washindwe kumiliki mashirika yaliyokuwa chini ya Umma na hivyo kusababisha uchumi mkubwa kumilikiwa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika yote yaliyobinafsishwa yangeuza baadhi ya hisa zao katika soko la mtaji yangesaidia katika kuongeza umiliki wa wananchi katika uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kukirekebisha kiwanda cha kuzalisha Matairi cha *General Tyre East Africa* ambacho kilikuwa tegemeo la wengi, Kamati inashauri Serikali ifanye kila iwezekanalo kuhakikisha kiwanda hicho cha matairi ambacho kilikuwa kinafanya vizuri kabla ya kubinafsishwa, kiweze kuzalisha matairi zaidi na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika kuagiza matairi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa michezo ya kubahatisha nchini. Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini *Tanzania Gambling Board* ni chombo kilichoundwa kisheria mwaka 2003 ili kusimamia michezo ya bahati nasibu nchini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Chombo hiki kimeweka utaratibu wa kukuza sekta hii kwa kusimamia utaratibu unaolinda wanaochezesha na wachezaji wa mchezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya bahati nasibu ya kubahatisha imeendelea kuleta mafanikio makubwa hapa nchini. Idadi ya watu wanaojihusisha na mchezo huo imekuwa ikiongezeka siku hadi siku na fedha zinazotumika kuchezea mchezo huo pia zimekuwa zikiongezeka kwa kasi. Kwa mfano; zaidi ya shilingi bilioni 460 ziko katika mzunguko wa bahati nasibu. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 20 la fedha ambazo zilitumiwa katika mwaka uliopita. Mchango wa kodi kwa mwaka 2011 ulikuwa ni shilingi bilioni 16, sawa na Dola za Marekani milioni 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa katika mchezo wa bahati nasibu imekuwa uingizaji wa mitambo ambayo imetengenezwa kwa lengo la kuwapatia wachezeshaji fedha nyingi kuliko kanuni za mchezo huo zinavyotaka. Changamoto nyingine ni michezo inayochezesha na Makampuni ya Simu ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kuwatumia ujumbe wa kushinda au bado nafasi kadhaa za kushinda bila hata ya mteja kushiriki kwa hiari katika michezo hiyo kupitia simu. Ujumbe wa mara kwa mara umekuwa kero kwa watumiaji wa simu ambao hawajashiriki wenyewe kwa hiari.

Kamati inashauri vyombo vinavyohusika kama vile TCRA na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini kukaa pamoja na kuona jinsi vitakavyoondoa kero hii ya kutumiwa ujumbe wa bahati nasibu pasipo kushiriki kwa hiari. Bado Kamati ina imani na michezo hii katika kuongeza zaidi mchango wake katika ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi GEPP. Sekta ya Hifadhi ya Jamii inaendelea kukua kwa kasi. Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini (GEPP) umefanikiwa kusajili wanachama 18,050 katika mpango wa hiari wa kujiwekea akiba ya uzeeni. Mfuko huo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
umetoa fursa kwa wananchi na watu wote walio katika sekta isiyo rasmi kujiwekea akiba ya uzeeni katika Mfuko huo ambapo mpango huo unawapa nafasi wanachama kutuma michango yao kwa njia ya mitandao ya simu.

Katika mpango huo, akiba za wanachama zimefikia fedha za Tanzania zaidi ya shilingi bilioni tatu ikiwa ni kiashiria kuwa wananchi wamekuwa na mwitikio mzuri wa kujiunga na Mfuko huo. Lengo na matarajio ya Mfuko ifikapo mwaka 2014 ni kusajili wanachama 33,226 ili kufanya Mfuko huo kukua kadiri ya malengo uliojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iunganishwe ili gharama za uendeshaji zipungue. Aidha, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ipewe msukumo wa kutosha ili kuongeza wanachama wengi kutoka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara: Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa za utendaji wa Shirika la Viwango Nchini (TBS), Mamlaka ya EPZA, Shirika la Taifa la Maendeleo, Wakala wa Usajili wa Biashara Nchini (BRELA) na Kituo cha Biashara cha Dubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu matumizi ya bidhaa zenye ubora nchini. Shirika la Viwango Nchini ndilo limepewa mamlaka kisheria katika ukaguzi wa bidhaa ili kuangalia ubora. Tatizo la bidhaa zinazolingia nchini kutokaguliwa au kukaguliwa kwa kiwango kisichofaa bado limeendelea kukua siku hadi siku. Kwa kutambua ukubwa wa tatizo hilo, Kamati yangu ilifanya ziara katika nchi za Japan, China na Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai) ili kuona ukaguzi wa bidhaa zinazokuja Tanzania unavyofanyika kutoka nchi hizo. Wajumbe wa Kamati walifanya ziara za mafunzo katika nchi hizo ili kujifunza namna ukaguzi wa bidhaa unavyofanyika kwa kuzingatia Sheria yetu ya sasa ya *Pre-shipment Verification of Conformity Standard* ambayo ilitungwa miaka minne iliyopita.

Katika ziara ya nchini Japan, Wajumbe walipata fursa ya kutathmini uwezo wa Makampuni yanayokagua

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)] magari yanayoingia Tanzania na utekelezaji wa Sheria ya Ukaguzi kwa ujumla. Baadhi ya Kampuni ambazo tulizitembelea ni pamoja na Kampuni ya *Japan Auto Appraisal Insitute* ambayo kwa kipindi cha miaka mitano imekagua magari yanayoingia Tanzania kama inavyooneshwa kwenye mabano: mwaka 2008 (13,290), mwaka 2009(13,837), mwaka 2010 (10,580), mwaka 2011 (7,182) na mwaka 2012 (7,0307). Kampuni hiyo pia inakagua magari yanayoenda nchi za Mauritius, Sri Lanka, Kenya na nchi nyingine duniani.

Kampuni nyingine ambayo Kamati ilipata fursa ya kuikagua ni *East Africa AutoMobile Services Company LTD* ambayo inakagua magari zaidi ya 1200 kwa mwezi kuanzia mwaka 2011. Kampuni hii pia inakagua magari ya nchi za Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai), Kamati ilifanya ziara na kuzitembelea Kampuni za *SGS* na *Intertek* ambazo zinakagua mizigo mbalimbali inayosafirishwa kuja Tanzania kwa ajili ya matumizi. Katika ziara hii, Wajumbe walibadilishana mawazo na wafanyakazi wa kampuni hizo kujua ni kwa nini tatizo la bidhaa zilizo chini ya kiwango bado zinaendelea kufurika katika soko la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa Kampuni ya *SGS* ina uwezo isipokuwa Kampuni ya *Intertek* haina uwezo kwa vile mpaka sasa kuna ushahidi wa makontena kadhaa yaliyobeba *oil* za magari ambazo baada ya kukaguliwa na *TBS* zilibainaika kuwa hazina viwango licha ya kuthibitishwa na Kampuni hiyo kuwa zinakidhi viwango vya ubora kwa ajili ya matumizi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengine tuliyogundua kwa upande wa ukaguzi wa magari kutoka Japan ni pamoja na wenye meli na waagizaji wa magari kutobanwa vya kutosha ili wasipakie magari ambayo hayajakaguliwa. Suala lingine ni uchache wa Wafanyakazi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA) kutoka Shirika la Viwango Nchini (TBS), jambo linalosababisha shirika hilo lisiweze kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo Kamati yetu ilibaini ni Sheria ya Ukaguzi kutumika sehemu moja ya Muungano, yaani Bara na kutotumika katika upande mwingine wa Muungano wa Tanzania, yaani Tanzania Visiwani. Suala hili limesababisha bidhaa zisizo na ubora kupenyezwa kupitia Bandari ya Zanzibar na kuingia Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine tatizo la kufurika kwa soko la bidhaa zisizo na ubora linachangiwa na wafanyabiashara wengi wadogo kununua bidhaa mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali na kukwepa kuzikagua bidhaa hizo kwa kisingizio cha gharama kubwa za ukaguzi. Sheria inataka mizigo yote ikaguliwe bila kujali wingi. Aidha, ada ya ukaguzi kwa mizigo midogo ni kubwa na haizingatii wingi na thamani ya mzigo. Matatizo yote hayo yamesababisha kupungua kwa mizigo kutoka nje ya nchi na wafanyabiashara kutoka Malawi, Zambia na nchi nyinginezo ambao walikuwa wanaitumia Tanzania hasa katika Soko la Kariakoo wamehamia Kenya ili kukwepa gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo Kamati ilibaini ni mkanganyiko wa kuhesabu umri wa gari. Wakati TBS wanatumia mwaka wa kusajili gari ndipo wanahesabu umri wa gari, kwa upande wa TRA wanatumia mwaka wa kuzalishwa gari, yaani *manufactured date* hata kama lilikuwa halitumiki baada ya kutoka kiwandani. Suala hili limeleta utata mkubwa baina ya Taasisi hizo mbili za Serikali na kuleta usumbufu kati ya wateja, waagizaji wa magari, wauzaji, TBS na TRA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri magari yote yakaguliwe ipasavyo kabla hayajaingizwa hapa nchini na ni jukumu la TBS kuhakikisha kuwa meli zote zinazopakia magari yanayoletwa Tanzania, zihakikishe yanakaguliwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
kabla hayajapakiwa na Serikali irekebishe kasoro ndogondogo zilizojitokeza mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waagizaji na watumiaji wote wa magari waelimishwe umuhimu wa kukagua magari kabla hayajafika hapa nchini, kwani imeonekana katika ziara yetu kuwa waagizaji, wasambazaji na wengi wa watumiaji wamekuwa wakiendelea kuagiza magari yenye bei nafuu ambayo yamekataliwa na wakaguzi ili yaingizwe nchini kwa ajili ya matumizi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara yetu ya Japan tumegundua kuna uwezakano mkubwa wa mionzi iliyovuja na inayoendelea kuvuja Japan baada ya tetemeko la ardhi ikaleta madhara makubwa kwa watumiaji wa magari ambayo yameathirika na mionzi ya nyuklia ambayo ni hatari kwa binadamu na viumbe wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzuia Tanzania isiwe shimo la taka la magari mabovu na madhara yanayotokana na hali hiyo, Serikali inashauriwa isitegemee wakaguzi walioko nje pekee, bali iweke utaratibu wa kufanya *post shipment verification* ili kuona kwamba bidhaa na magari yote yamekaguliwa kama Sheria inavyotaka. Aidha, Serikali zote za Muungano zikae ili ziwe na mkakati wa pamoja wa kuzuia bidhaa zisizo na ubora kuingia nchini. Hatua hiyo itasaidia kuzuia bidhaa zisizo na ubora zisipenyezwe kupitia Bandari ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango Nchini lishirikiane na Mamlaka ya Mapato nchini ili kuondoa utata uliopo wa kuhesabu umri wa gari mara linapotengenezwa kiwandani au linaposajiliwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya matumizi. Utata huu umekuwa ukileta usumbufu mkubwa baina ya waagizaji, wanunuzi, wakaguzi na Mamlaka ya Mapato juu ya kodi inayostahili kulipwa kutokana na toleo la gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uchache wa wafanyakazi katika kusimamia Sheria ya Ukaguzi linaweza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
kutatuliwa kwa kutumia mfumo wa *Public Private Partnership (PPP)*, ambao utahusisha sekta binafsi katika kusimamia jukumu hilo. Matumizi ya mfumo huo yatasaidia kuokoa gharama kubwa ambazo zingetumika katika kuajiri wafanyakazi wengi wa kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), limepewa majukumu ya kusimamia viwanda vya msingi nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi. Tunaipongeza Serikali kwa kulipa kipaumbele suala la viwanda katika Mpango wa Maendeleo wa 2011/2012 - 2015/2016, ambao unatambua mapinduzi ya viwanda kuwa ni chachu kubwa ya kukuza uchumi wetu kwa kasi ifikapo mwaka 2025. Ni imani ya Kamati yangu kuwa kama Serikali itatekeleza ipasavyo mpango huo, uchumi utakua na umaskini utapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hivi sasa hali ya maendeleo ya viwanda nchini bado siyo ya kuridhisha. Mchumi anayejulikana kimataifa na mtunzi bora wa vitabu kutoka Chuo Kikuu cha *Cambridge*, Ha-Joon Chang katika kitabu chake kipya ameelezea mengi kuhusu umuhimu wa viwanda katika uchumi. Naomba kunukuu sehemu ndogo ya kitabu chake: *"History has repeatedly shown that the single most important thing that distinguishes rich countries from poor ones is basically their higher capabilities in manufacturing, where productivity is generally higher, and, most importantly, where productivity tends to (although does not always) grow faster than in agriculture and services."* (Chang, 2007:213).

Kwa tafsiri, historia imekuwa inajirudia kwamba nchi zote zilizoendelea ni zile zilizopiga hatua kubwa katika viwanda vya uzalishaji.

Tanzania licha ya kutambua umuhimu wa kuwa na mapinduzi ya viwanda, ripoti ya ushindani wa viwanda nchini, *Tanzania Industrial Competitiveness Report* ya mwaka (2012) inaonesha kuwa Tanzania ipo nyuma katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuzalisha bidhaa kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
ajili ya kuuza nje. Ripoti hiyo inatoa takwimu kwamba katika kipindi cha mwaka 2000 na 2010 mchango wa sekta ya uzalishaji katika Pato la Taifa kutoka viwandani umekua kwa wastani wa asilimia 9.5 ambacho ni kiwango cha chini ukilinganisha na nchi nyingine katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Watanzania katika kushiriki mapinduzi ya viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa, yaani *Tanzania Development Vision 2025*, ambayo inataka uchumi wa Tanzania kuongozwa na uchumi wa Sekta ya Viwanda na Biashara, kuhimili ushindani wa masoko ya ndani na nje ya nchi, inakabiliwa na changamoto zifuatazo:- mwitikio mdogo wa sekta binafsi katika kuinua kasi ya mageuzi ya mifumo ya uchumi, viwanda, miundombinu, teknolojia, ujasiriamali na maendeleo ya rasilimali.

Changamoto nyingine ni wananchi wengi wazalendo kusukumwa nje ya mkondo wa uendeshaji wa uchumi rasmi na biashara ya kimataifa na matumizi ya rasilimali muhimu kwa maendeleo endelevu ya nchi kumilikiwa na wageni na hivyo kuvunwa na kusafirishwa katika hali ghafi ambayo inainyima nchi na wananchi ajira na mapato yatokanayo na ongezeko la thamani katika matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma na ule wa kuzalisha chuma wa Liganga imechukua muda mrefu kutekelezwa licha ya faida zake kubwa kama zilivyoelezwa na wataalam mbalimbali. Ni nia ya Kamati kuhakikisha miradi hiyo inakamilika mapema ili kuweza kuleta chachu ya maendeleo nchini. Kamati ilipokea taarifa kutoka *NDC* kuwa Mradi wa Mchuchuma utakamilika mwaka 2016 na mradi wa kuzalisha chuma wa Liganga utakamilika mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine wa makaa ya mawe upo Ngaka katika Mkoa wa Ruvuma. Mradi huu ukikamilika utazalisha tani 2.5 za makaa ya mawe kwa mwaka na kufua umeme wa Megawati 400 ambao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
utaunganishwa katika Gridi ya Taifa na kusababisha gharama za umeme kushuka kwa kiwango kikubwa. Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya *NDC*, jumla ya ajira zipatazo 3,250 zinategemewa kutolewa pindi mradi utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inapenda kuishauri Serikali iendeleo kuwekeza zaidi katika miradi hii na kuipa msukumo wa kutosha katika utekelezaji wake ili iweze kukamilika mapema iwezekanavyo. Kwa sasa miundombinu ya barabara kuelekea kwenye miradi hiyo bado hairidhishi na tatizo hili limekuwa likiwakatisha tamaa wawekezaji. Aidha, mradi wa umeme wa upepo ambao *NDC* ni mbia, bado unasuasua kwani kasi yake hairidhishi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kusikia kutoka kwa wafanyabiashara na wenye viwanda hapa nchini kuwa mazingira ya kuuza bidhaa zilizozalishwa ndani ya nchi ni magumu sana. Kwa mujibu wa taarifa hizo, ni rahisi kuagiza bidhaa kutoka nje kuliko kuzalisha ndani ya nchi. Hii imetokana na sera ya kulinda viwanda kutofanikiwa hapa Tanzania. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha tatizo hili linatatuliwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu za *Economic Processing Zone (EPZ)* na *Special Economic Zone (SEZ)* zilianzishwa kwa ajili ya kukuza mauzo yetu nje ya nchi na kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Katika eneo hili Kamati hairidhishwi na mgao unaofanywa na Serikali hususan katika Programu za *EPZ*. Tatizo hili limesababisha kutokamilika kwa mipango kwa wakati.

Kwa mfano, malipo kwa watakapoathirika na bomoabomoa ili kujenga *Tanzania China Logistic Centre* Kurasini kwa zaidi ya miaka mitatu sasa bado hayajatolewa yote licha ya Serikali kufahamu umuhimu wa kujenga kituo hicho ambacho marafiki zetu wa China wapo tayari kukijenga kwa gharama zao baada ya Serikali ya Tanzania kukamilisha malipo kwa wale wote ambao maeneo yao yatachukuliwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Serikali inafahamu vizuri umuhimu huo wa kufanya maamuzi mapema kwani mradi huo unagombewa na nchi nyingine za Afrika ikiwemo Nigeria ambayo imeonesha utayari wa kuwakaribisha Wachina kuingia ubia nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fidia ya jumla ya shilingi bilioni 46.6 yanatakiwa kwa ajili ya kuwalipa fidia wakazi wa eneo la Bagamoyo *SEZ* ambao hawajalipwa tangu mwaka 2008. Kwa msingi huo, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha hizo haraka iwezekanavyo ili tusiwavunje moyo wawekezaji katika azma ya kuanza kutekeleza miradi yao ambayo itasaidia kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Aidha, malipo hayo kwa wananchi ni muhimu kwa ajili ya maisha yao kwani wamekuwa wakisubiri toka mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zinahitajika katika kukamilisha Miradi ya *EPZ* ni ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyokwisha fanyiwa uthamini na maeneo yaliyokwishapata waendelezaji kama Bagamoyo (*EPZA*) shilingi bilioni 46.66, Bagamoyo (*CMHI*) shilingi bilioni, *Kurasini Logistics Centre* shilingi bilioni 49.168; Tanga, shilingi bilioni 4.2; Songea, shilingi bilioni 4.2 na Kigoma, shilingi bilioni 1.5. Jumla ni shilingi bilioni 207.728.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Programu za *EPZ* na *SEZ* zinatoa majibu kwa hoja kubwa za kimsingi katika nchi yetu kama vile kuiinua nchi kiviwanda (*industrialisation*), kuongeza mauzo nje (*export promotion*), kuongeza kipato (*income generation*) na kuongeza ajira (*employment creation*). Kutokana na umuhimu huo, Kamati inashauri kuwa ni vyema *EPZA* ikatengewa fedha za kutosha ili kutekeleza programu hizo ambazo zitaleta *multiplier effects* katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara Dubai ili kujifunza mambo mbalimbali kama vile ukaguzi wa magari, uendeshaji wa maduka ya kubadilishia fedha pamoja na kutembelea Kituo cha Biashara cha Dubai. Tanzania ina ofisi katika kituo hicho kikubwa cha biashara duniani.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
Changamoto zilizopo ni bidhaa za Tanzania kutokidhi viwango vilivyowekwa kimataifa na Tanzania kushindwa kufanya maamuzi yanayohusu biashara na uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kujadili Taarifa ya Utendaji wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Dodoma. Kamati ilibaini kuwa Chuo hicho kinakabiliwa na uhaba wa vyumba vya mihadhara na *TEHAMA*, maktaba ndogo isiyokidhi mahitaji pamoja na kukosekana kwa huduma ya Zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza matatizo ya uhaba wa miundombinu ya madarasa, ofisi na maktaba, Kamati inashauri Serikali iwapatie jengo la hifadhi ya chakula kwani halitumiki kwa kipindi cha zaidi ya miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo hilo ambalo lipo karibu sana na Chuo hicho pamoja na Ofisi za Bunge, halifai kutumika kwa ajili ya kuhifadha chakula kwa kuwa lipo karibu sana na makazi ya watu na ofisi mbalimbali, hali ambayo itasababisha gharama kubwa katika kutokomeza wadudu ambao watakuwa tishio kwa majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo hili likikabidhiwa kwa Chuo hicho litakuwa na uwezo wa kupunguza kabisa msongamano mkubwa wa wanafunzi katika chuo hicho. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imetekeleza ahadi yake ya mara kwa mara kuhusu matumizi ya jengo hilo.

Katika mahafali ya wahitimu wa Chuo hicho mwaka huu, mgeni rasmi ambaye alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliahidi kushughulikia kilio cha *CBE*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa za utendaji za Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezeshaji na Uwekezaji) ambazo ni Kituo cha Uwekezaji Nchini kinachojulikana kama *Tanzania Investment Centre (TIC)* na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Na. 26 ya mwaka 1997 kwa lengo la kuendeleza, kuratibu na kuwezesha uwekezaji nchini. *TIC* ina jukumu la kuhamasisha uwekezaji na masuala yanayohusiana na uwekezaji ili uwekezaji uweze kuwa na manufaa kwa Watanzania kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2012 Watanzania wameweza kuona umuhimu wa kuwekeza na wameweza kuchangamkia fursa katika sekta mbalimbali. Katika kipindi hicho zaidi ya miradi 869 yenye thamani ya mitaji ya Dola za Marekani milioni 11,420 iliweza kusajiliwa na inategemewa kuzalisha ajira zaidi ya 174,412. Idadi hii ya miradi ni kubwa kuwahi kusajiliwa na kituo.

Miradi ya Watanzania iliweza kuongoza kwani *TIC* ilisajili miradi 469 ya wazawa ambayo ni asilimia 54 ya miradi yote iliyosajiliwa. Sekta tano zilizoongoza katika kusajiliwa ni utalii, usafirishaji, uzalishaji viwandani, majengo ya biashara na kilimo. Sekta ya Utalii iliongoza kwa kusajili miradi 144, usafirishaji miradi 92, uzalishaji viwandani miradi 86, majengo ya biashara miradi 78 na kilimo miradi 28. Katika usajili wa miradi hiyo, wawekezaji wa nje waliweza kusajili miradi 205 ambayo ni asilimia 23.5, kiwango ambacho ni chini ya nusu ya kiwango cha usajili wa miradi ya wawekezaji wa ndani. Miradi ya ubia kati ya wageni na Watanzania ilikuwa ni 195 ambayo ni asilimia 22.5. *TIC* katika jitihada zake za kuongeza faida za uwekezaji katika uchumi wa Tanzania pia ilifanya shughuli ya kuwawezesha wawekezaji kupata vibali vyote vinavyohitajika chini ya *One Stop Centre* na utoaji wa huduma kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilianzishwa rasmi Novemba, 2005 baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi mwaka 2004. Licha ya Baraza hili kuwepo kwa zaidi ya miaka minane, bado Watanzania

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)
wako nyuma katika kushiriki kikamilifu katika kumiliki uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matatizo ambayo yanawakumba wananchi katika kushiriki na kumiliki uchumi wa nchi yao ni pamoja na ukosefu wa mitaji, kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba, kuwepo kwa vizuizi vinavyosababisha benki za biashara kusita kutoa mikopo na ardhi haijatumika vizuri katika kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi na kutatua changamoto za ardhi kutotumika kama chombo cha kuweka chachu ya uwekezaji pamoja na kufanya tathmini ya utendaji wa kazi wa Baraza na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kujiipanga upya katika kuhakikisha umiliki wa uchumi kwa wananchi wengi unakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa, Baraza liliidhinishwa bajeti ya shilingi bilioni 17.16 ambayo ni asilimia 4.5 ya fedha zilizoombwa. Aidha, fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni 13.40 ambazo ni asilimia 78.01 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuliwezesha Baraza kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Sera na Sheria ya Uwezesaji. Katika sehemu ya mapato na matumizi, Baraza limekuwa likitengewa fedha kidogo ikilinganishwa na zilizoombwa.

Pia sehemu ya fedha zilizoidhinishwa hazifiki kwenye Baraza kwa wakati ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa. Hivi sasa Mfuko wa Baraza una mtaji wa shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya kuwezesha wananchi. Katika jitihada za kuongeza mtaji huo, Kamati inashauri Serikali kupeleka mabilioni ya JK katika mfuko wa Baraza. Kwa taarifa ambazo Kamati imezipata, marejesho ya mabilioni ya JK yamefikia asilimia 82 kwa sasa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Mradi wa *Tanzania China Logistics Centre* ni Mkutano wa *Sino-Africa Cooperation* uliofanyika Jijini Cairo mwaka 2009 ambapo Serikali ya China ilionesha nia ya kujenga, kuendeleza na kuendesha vituo vikubwa vya biashara katika nchi nne za Afrika. Kutokana na mahusiano mazuri kati ya Serikali ya Tanzania na China, Serikali ya China iliichagua Tanzania kati ya nchi nne za Afrika kuwa ya kwanza ambayo mradi wa aina hii utaanzishwa. Mradi huu utajengwa, kuendelezwa na kuendeshwa kwa ubia (*PPP*) kati ya Serikali ya Tanzania na China, ambapo Serikali ya China itawakilishwa na Kampuni ya *Yiwu Pan-Africa International Investment Corporation* na Tanzania ikiwakilishwa na Mamlaka ya *EPZ (EPZA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mradi huu lina ukubwa wa ekari 61.2 ambalo limetengwa katika Kata ya Kurasini, Jijini Dar es Salaam na linahusisha Mitaa ya Shimo la Udongo, Mivinjeni na Kiungani inayojumuisha idadi ya kaya 1020. Kwa mujibu wa taarifa ya uthamini (*Valuation Report*) kutoka kwa Mthamini Mkuu wa Serikali *Vol. 1 – 5*, jumla ya gharama ya fidia ni shilingi 94,168,314,600 na jumla ya kaya zilizothirika na mradi ni 1020. Hadi kufikia tarehe 25 Oktoba, 2013 mamlaka ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 45.55 ambapo kati ya hizo shilingi milioni 550 zilitumika katika uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya fidia imelipwa mwezi Agosti, 2013 ambapo watu 278 walilipwa kiasi cha shilingi bilioni 25 na mamlaka kufanikiwa kutwaa eneo la ekari 19.7 ambazo zinahusisha sehemu ya eneo la vitongoji vya Mivinjeni na Kiungani.

Aidha, mwezi Novemba, 2013 mamlaka ilikamilisha ulipaji wa fidia kwa awamu ya pili iliyohusisha shilingi bilioni 20 ambapo watu 194 walilipwa fidia na kuweza kupata eneo la ekari 5.9. Fidia ilifikia jumla ya shilingi bilioni 45 na idadi ya watu waliofidiwa kufikia 472 kati ya watu 1020 na jumla ya eneo lililokwishafidiwa kufikia ekari 25.6 kati ya ekari 61.2.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo bado halijalipwa fidia ni ekari 35.6 ambalo litagharimu kiasi cha Sh. 49,168,314,600/=. Aidha, mpaka kufikia mwezi Januari, 2014 kwa mujibu wa Sheria za Ardhi, fedha yote isipolipwa ndani ya miezi sita itatozwa riba ya asilimia sita ambayo itaendelea kuongezeka kila baada ya mwaka. Hadi kufikia Januari, 2014 riba itakuwa ni Sh. 2,950,098,876/= na hivyo kusababisha deni lote kufikia kiasi cha Sh. 52,118,413,476/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ambazo zinaweza kujitokeza kwa kutokulipa kwa wakati ni pamoja na kusababisha ongezeko la kiasi kitakachotakiwa kulipwa kutokana na riba ambapo hadi kufikia Januari, 2014 riba itakuwa shilingi bilioni 2.9, jambo ambalo linaweza kusababisha wawekezaji wafikie hatua ya kukata tamaa kutokana na ucheleweshaji wa upatikanaji wa eneo na kufikiria kuwekeza katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari nyingine ni pamoja na kuongezeka kwa malalamiko kutoka kwa wananchi na kukosekana kwa ajira tarajiwa 25,000 zitakazotokana na Mradi huu, pamoja na kupoteza mapato ya Serikali ambayo yangetokana na kodi ambazo zingepatikana katika ajira zitakazotokana na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikipoteza mradi huu itakuwa imepoteza fursa ya uwekezaji wa mtaji wa takribani Dola za Kimarekani milioni 400 na hatimaye kupoteza ujuzi ambao ungepatikana kutokana na teknolojia ambayo ingetumika katika eneo la mradi. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha kulipa fidia iliyobaki ili kuepuka hasara na usumbufu utakaojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni Eneo Maalum la Uwekezaji la Bagamoyo (*Bagamoyo SEZ*), ambalo lina ukubwa wa takribani hekta 9,000 na linahusisha Vijiji vya Zinga, Kondo, Mlingotini, Pande na Kiromo. Aidha, eneo hili limejumuisha mashamba ya *NAFCO* ya Kitopeni, Kidagoni na Pimbini, shamba la Marealle na Shamba la Matunda (*Matunda Farm*). Eneo hili litaendelezwa katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
mfumo wa mji wa viwanda na biashara na uendelezaji wake utahusisha pia uendelezaji wa bandari mpya ya Mbegani.

Aidha, kunatarajiwa kuwa na reli ya kuunganisha eneo hilo na Reli ya Kati na Kituo cha Ruvu. Ndani ya eneo la *Bagamoyo SEZ* kutajengwa eneo la viwanda vya *EPZ* na *SEZ*, eneo huru la biashara litakalokuwa *trade hub* kwa nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika, sehemu za utalii (*tourist parks*), eneo huru la teknolojia (*technological park*), *logistic hub* pamoja na maeneo ya makazi na shughuli nyingine za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ya uthamini kwa eneo linalokadiriwa kufikia hekta 5,742.52 ambalo sehemu kubwa ni mashamba yanayomilikiwa na watu na Taasisi mbalimbali binafsi imekamilika. Jumla ya watu 2,180 wamefanyiwa uthamini tangu mwaka 2008 na fedha iliyokuwa inahitajika kwa ajili ya kulipa fidia mwaka 2012 ni shilingi bilioni 60.

Hadi kufikia sasa, fidia iliyolipwa ni shilingi bilioni 16.9, watu waliolipwa ni 821 na eneo lililotwaliwa ni hekta 1,630. Katika mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Serikali ilitenga na kuzuia (*ring fenced*) jumla ya shilingi bilioni 50.2 kwa ajili ya fidia ya eneo hili. Hata hivyo, fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 10.9 na shilingi bilioni 39.3 hazikuletwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha.

Kutokana na ongezeko la riba, jumla ya shilingi bilioni 46.66 zinahitajika ili kukamilisha malipo ya fidia kwa eneo lililokwishafanyiwa uthamini ambalo linajumuisha watu au kaya 1359. Malipo hayo ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 3.56 kama riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari mbazo zinaweza kujitokeza kwa kutolipa fidia kwa wakati ni kama ifuatavyo:-

Kusababisha ongezeko la kiasi kitakachotakiwa kulipwa kutokana na riba ambapo kuanzia Oktoba, 2012 hadi kufikia Oktoba, 2014 kiasi cha riba kimefikia shilingi bilioni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

3.56. Pia itasababisha wawekezaji kufikia hatua ya kujitoa katika mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyeiti, aidha, eneo la hekta 1700 lililotolewa kwa *China Merchants* kwa ajili ya kujenga viwanda ambalo halijalipiwa fidia kwani halikufanyiwa uthamini katika awamu ya kwanza; gharama za kuwahamisha wakazi wa eneo husika na kuwapa makazi mapya zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 101. Fedha za mradi huu zinatakiwa kabla ya tarehe ya kukabidhi eneo kwa waendelezaji kwa mujibu wa mkataba ambayo ni Machi 20, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi wa Bagamoyo ambao wamesubiri malipo hayo tangu mwaka 2008, kukosekana kwa ajira 200,000 tarajiwa zitakazotokana na mradi huu na wananchi wengi wameanza kuwa masikini zaidi kwa kuwa wamepokonywa haki yao ya kumiliki ardhi bila msaada wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengine ni kupoteza pato la Serikali ambalo lingetokana na kodi ambazo zingepatikana katika ajira zilizopo katika mradi huu, kupoteza ujuzi ambao ungepatikana kutokana na teknolojia ambayo ingetumika katika eneo la mradi na kupoteza fursa ya uwekezaji katika mtaji ambao ungewekezwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaliomba Bunge litoe azimio la kuitaka Serikali kulipa fidia kwa wahusika kabla ya Desemba 31, 2013 ili kuwezesha utekelezaji wa miradi hii ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la viongozi wa Taasisi kukaimu kwa muda mrefu, zaidi ya miezi sita ambayo ndiyo kikomo kulingana na utaratibu wa utumishi wa Umma. Aidha, tunashukuru matatizo kama hayo yamekwisha katika Chuo cha Elimu ya Biashara -CBE na TANTRADE na tayari

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
wamepata viongozi wa kudumu. Bado tatizo hili lipo katika Wakala wa Usajili wa Makampuni unaoujulikana kama *BRELA* ambapo nafasi imekuwa ikikaimiwa kwa zaidi ya miezi 13.

Pia bado kuna tatizo hili *Tanzania Bureau of Standard*. Tatizo hili la kukaimu linasababisha maamuzi ya Taasisi hizo kuchukua muda mrefu na kutojiamini kwa wanaoshikilia nafasi hizo kwa kuwa wanakosa *instruments* za kufanyia kazi. Kamati ingependa kuona Serikali inayashughulikia mapema mambo hayo. Aidha, Taasisi ambazo Bodi zake zimemaliza muda wake ni dhahiri Serikali inajua kama Wajumbe wa Bodi watamaliza muda wake na hili siyo jambo la dharura, hivyo Kamati inashauri wateuliwe kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwaandae Watanzania na miundombinu itakayowawezesha kumiliki uchumi wa gesi. Maandalizi ya uchumi wa gesi yawe makubwa hususan katika kumwandaa Mtanzania katika miaka ijayo kuwa gesi iliyogunduliwa Kusini mwa Tanzania itakuwa nguzo kubwa katika uchumi wetu kama ilivyo katika nchi ya Urusi ambapo uchumi wake kwa kiasi kikubwa unategemea kuuza gesi ndani na nje ya nchi.

Maandalizi yanayotakiwa ni pamoja na matumizi bora ya gesi, wataalam wa kutosha, mitaala ya kufundishia katika vyuo vyetu pamoja na maandalizi ya miundombinu katika majengo mbalimbali yanayokusudiwa kujengwa. Aidha, Serikali iandae utaratibu wa jinsi ya kupunguza majanga yanayotokana na gesi kwa kutumia mfumo wa bima na mifumo mingine inayokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wa nchi zenye vituo vya kufanya tafiti za mafuta na gesi duniani kama Houston, Aberdeen, Singapore, Papua New Guinea umeonesha kuwa nchi hizi hutenga maeneo maalum kando ya bahari kwa minajili ya *freeport zones* ambapo hukodishwa na makampuni yanayotoa huduma kwa watafiti wa mafuta na gesi hususan katika kuweka vituo maalum vya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
usambazaji wa vifaa vya huduma za utafiti. Hivyo basi, Mamlaka ya Bandari, Shirika la Maendeleo ya Petrolini nchini, Mamlaka ya Mapato na Uongozi wa Mkoa wa Mtwara na kampuni zinazohusika na tafiti za mafuta na gesi watekeleze mpango huo mapema kama walivyokubaliana hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua madhubuti inazochukua kuhakikisha kuwa inaweka miundombinu bora ya umeme kama vile Mradi wa Songosongo na Mchuchuma, bado wawekezaji wengi wanalalamika kuhusu upatikanaji wa umeme wa kutosha wa viwanda vyao.

Kamati ilipata fursa ya kutembelea viwanda vya saruji, vinywaji na vinginevyo na wamiliki wa viwanda hivyo walitoa kilio chao mbele ya Kamati juu ya tatizo sugu la umeme usiozingatia ratiba na wakati mwingine kuleta madhara makubwa kwenye mashine za kuzalishia bidhaa. Tatizo la umeme limesababisha kutumia majenereta ambayo yanatumia gharama kubwa na kusababisha hasara kwa kampuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Serikali kutokamilisha miradi mikubwa ya umeme kama vile Mradi wa Ngaka na Mchuchuma imeanza kutafsiriwa vingine na wananchi kwa kuhusisha na masilahi binafsi. Ni muda muafaka sasa kwa Serikali kuhakikisha miradi hiyo iliyochukua muda mrefu inakamilishwa mapema iwezekanavyo ili kushusha umeme kwa kiasi kikubwa na kupunguza kuagiza mafuta kwa ajili ya mitambo ya jenereta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwa na migongano ya utekelezaji wa shughuli za Serikali baina ya Taasisi za Serikali katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Tatizo hili limekuwa kikwazo kikubwa katika kuleta maendeleo ya haraka hapa nchini na kutimiza mipango mbalimbali ya maendeleo kama vile Kasi Mpya, Nguvu Mpya, Ari Mpya, Mpango wa Matokeo Makubwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA) Sasa (*Big Results Now*), Kilimo Kwanza na kadhalika. Mfano mkubwa ni mgongano uliopo baina ya Mamlaka ya Mapato Nchini na Mamlaka ya Bandari Tanzania juu ya mifumo mipya ya utoaji wa mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza ukusanyaji wa mapato, Kamati inaishauri Serikali kufanya mageuzi makubwa katika matumizi ya *TEHAMA* hususan katika kuhakikisha kuwa wanaweka mfumo wa kielektroniki katika kukagua magari ambayo hayajalipa leseni na bima ambapo Askari wa Usalama Barabarani watapatiwa vyombo vya kielektroniki katika kutekeleza Sheria za Usalama Barabarani. Utaratibu huu ukitumika ipasavyo utaliingiza Taifa zaidi ya mara mbili ya makusanyo yanayokosekana sasa kutokana na tozo za ada na bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuongeza mapato liende sanjari na hatua ya kubana matumizi ya Serikali hususan katika kupunguza ununuzi wa magari ya kifahari na hatua nyinginezo za kutumia *public private sector partnership*, utaratibu ambao unatumika vizuri na kuonesha mafanikio makubwa katika nchi za Brazili, Singapore na Malaysia. Sheria inayotumika sasa katika manunuzi imelalamikiwa kuwa imekuwa chanzo cha kuongezeka kwa gharama za manunuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iangalie uwezekano wa kuhimiza mablenki yaweze kufungua matawi yao kila Wilaya ambako pia kuna wananchi wengi wenye uhitaji wa huduma za kiblenki. Aidha, suala hilo liende sambamba na ufunguzi wa mablenki ya kilimo, benki ya vijana na wanawake katika ngazi ya kila Mkoa kwa kuanzia ili kufikisha huduma hizo karibu sana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iwezeshe Taasisi ya *Bancorp Ltd.* kuwa bBenki kamili ya biashara kwa kuwa hajjaweza kutimiza sharti la Benki Kuu la kuwa na kiwango cha chini cha Shilingi bilioni 15.0. Kwa sasa Taasisi hii ina mtaji wa Shilingi bilioni 7.8. Hivyo basi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]
Serikali iwekeze kiasi cha shilingi bilioni 7.2 ili iweze kufikisha shilingi bilioni 15 zinazohitajika iweze kupata leseni ya kuwa Benki ya Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Tanzania imekuwa ikilalamikiwa na wadau wa maendeleo kuwa inachelewa kufanya maamuzi ya kufanya mambo. Hii imetokana na kuwa na milolongo ya taratibu na masharti ambayo yamekuwa kero na kuchelewesha kufanyika kwa maamuzi.

Kamati ilipata malalamiko kutoka Kituo cha Biashara cha Dubai kuwa jitihada zao za kutangaza biashara za Tanzania kwa kiasi kikubwa zinakwamishwa na kuchelewesha kwa maamuzi yanayosubiriwa kutoka Taasisi mbalimbali za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kanuni (*regulations*) kuchelewa kuandaliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali na kusababisha Sheria zilizopitishwa na Bunge kuchelewa kutekelezwa. Kwa mfano, Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 hadi leo haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Naomba nitoe shukrani zangu kwako wewe mwenyewe kwa kuendelea kuendesha Bunge kwa umakini mkubwa ukishirikiana na Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika - Mheshimiwa Job Ndugai na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wote wa Wizara tatu ambazo Kamati inazisimimia. Naomba kwa heshima na taadhima niwatambue kwa kuwataja majina; Mheshimiwa William Mgimwa - Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda - Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Mary Nagu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji).

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA)]

Wengine ni Mheshimiwa Saada Mkuya Salum na Mheshimiwa Janet Mbene ambao ni Manaibu Mawaziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Gregory Teu - Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Dkt. Silvanus Likwelile - Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha pamoja na Manaibu wake wote wawili. Shukrani nyingine ziwaendee Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Ndugu F. Turuka - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mwisho, shukrani ziwaendee Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Viwanda na Biashara pamoja na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hizo. Napenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano waliotupa wakati tukitekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha Taarifa ya Kamati kwa kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah. Aidha, nawapongeza kwa dhati Makatibu wa Kamati; Ndugu Brown G. Mwangoka, Ndugu Angela Shekifu na Msaidizi wa Kamati Ndugu Paulina Mavunde.

Mwisho kabisa, nawatakia Watanzania wote kheri ya Krisimasi na Mwaka Mpya wa 2014. *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atujalie wote tufike salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha, naomba kutoa hoja (*Makofi*)

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, nakushukuru. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi. (*Makofi*)

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi. Kwanza kabisa, naomba nimpe pole Mheshimiwa William Mgimwa, Waziri wa Fedha na Diwani mwenzangu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa; Mungu amjalie aweze kupona haraka na aweze kuungana nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Masuala ya Ukimwi, niwasilishe taarifa ya utekelezaji wa shughuli ambazo tumezifanya katika kipindi cha Machi hadi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI uliowateua kwa mamlaka ulionayo na kwa Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013 ni hawa wafuatao na napenda kuwatambua kwa kuwataja majina:-

Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o - Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Chiku Alfah Abwao, Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali Omar, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Dkt. Engelbert F. Ndungulile, Mheshimiwa Maria Ibesi Hewa, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa Ignatus Aloyce Malocha, Mheshimiwa Selemani Saidi Bungara, Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, Mheshimiwa Ahmed Ally Salim, Mheshimiwa Sara Msafiri Ali, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Maulida Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Anna MaryStella John Mallack na Mheshimiwa Mwanamrishi Taratibu Abama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Masuala ya UKIMWI ina jukumu la kushughulikia mambo yafuatayo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]

(i) Kuratibu Masuala yanayohusu Ukimwi katika sekta zote;

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu Ukimwi na udhibiti wa dawa za kulevya;

(iii) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa za kulevya; na

(iii) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Desemba, 2012 hadi Desemba, 2013 Kamati ilishughulikia mambo mbalimbali ambayo naomba kuwasilisha kwa njia ya ushauri na mapendekezo na hatimaye Bunge lako Tukufu liweze kuyapokea, kuyajadili na kupata uamuzi wa Bunge kwa ajili ya utekelezaji bora wa Serikali. Mambo hayo ni pamoja na bajeti kwa ajili ya kutekeleza afua za Ukimwi; matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya VVU/Ukimwi; upungufu wa sheria ya VVU/ Ukimwi; Ukimwi kwenye Sekta ya Uvuvi; Ukimwi kwenye Sekta za Madini, Gesi na Mafuta; utekelezaji wa Waraka wa Rais Namba 2 wa Mwaka 2006; kufuatilia utekelezaji wa Kamati za Kudhibiti Ukimwi ngazi za Wilaya, Kata, Vijiji na Vitongoji; mchango wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwenye Masuala ya Ukimwi; mahusiano ya ukatili wa kijinsia na Ukimwi; Baraza la Watu wanaoishi na VVU/Ukimwi; Chama cha Wabunge cha Kupambana na Ukimwi; na udhibiti wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti kwa ajili ya kutekeleza afua za Ukimwi. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kumekuwa na kupungua kwa rasilimali fedha kwa kiwango cha asilimia tisa kutoka mwaka 2006/2007, ingawa wahisani wameonesha nia ya kuendelea kutoa msaada kwa sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahisani wakubwa wa shughuli za Ukimwi ni Serikali ya Marekani na Mfuko wa Dunia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)
wa Magonjwa ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria. Wahisani hawa huchangia kiasi cha asilimia 90 ya fedha za Ukimwi, ambapo mchango wa Serikali ni asilimia kumi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*), watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi wanatakiwa kuanza kutumia dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi wanapokuwa wamefikisha *CD4* 500 badala ya *CD4* 300 kama ilivyo sasa. Hii maana yake ni kuwa, wahitaji wa dawa wataongezeka hivyo kuongeza bajeti ya fedha za Ukimwi. Ili kukabiliana na tatizo la utegemezi wa fedha za Ukimwi kutoka kwa wadau wa maendeleo, Sera ya Taifa ya Ukimwi iliyoinduliwa mwaka 2001, inaelekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Ukimwi. Kuanzishwa kwa Mfuko huu kutasaidia kupunguza utegemezi wa wahisani kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takribani miaka kumi na moja sasa tangu kuzinduliwa kwa Sera hiyo bila kuanzishwa kwa Mfuko wa Ukimwi na kwa miaka mitatu mfululizo sasa Kamati inapotaka maelezo kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, Serikali imekuwa ikitoa majibu mepesi kuwa andiko limeshakamilika na kuwasilishwa kwenye Kikao cha Baraza la Mawaziri na Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kuanzishwa kwa Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Ukimwi. Pamoja na kwamba, bado wadau wa maendeleo wana nia ya kuendelea kusaidia afua za Ukimwi, Kamati inaitaka Serikali kutoa majibu kwa nini kumekuwa na kigugumizi kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Kudhibiti Ukimwi? Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha marekebishi ya mabadiliko ya sheria hii mapema iwezekanavyo ili Mfuko wa Ukimwi uweze kuanzishwa katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Ili kuweza kukabiliana na changamoto ya ongezeko la wahitaji wa dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (*ARV's*) kutokana na ongezeko la idadi ya *CD4*, ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
vyema Serikali ikawa na mkakati wa kuanzisha viwanda vya ndani vya kuzalisha ARV's, kwani Serikali hutumia gharama kubwa kuagiza dawa hizo nje ya nchi, ambapo zaidi ya asilimia 90 ya dawa hizo hugharamiwa na fedha za nchi wahisani.

Kamati inaishauri Serikali kuziagiza Halmashauri zote nchini kutenga fedha kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza afua za Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu matumizi ya fedha za Ukimwi kwenye maeneo mbalimbali kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 ilibani upungufu wa fedha za kupambana na Ukimwi. Baadhi ya upungufu huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za *Global Fund* zinazohusu Ukimwi ambazo hazikutumika hadi kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha 2011/2012 zilikuwa Sh. 3,351,960,875/=. (ii) Kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Tume ya Kudhibiti Ukimwi ilipokea kiasi cha Sh. 2,917,608,827/= kwa ajili ya usimamizi wa kazi za Ukimwi. Kiasi cha Sh. 222,250,895/= ambazo ni sawa na asilimia 7.6 hazikutumika. (iii) Fedha kwa ajili ya Halmashauri mbalimbali kupambana na Ukimwi ambazo hazikutumika hadi mwishoni mwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 zilikuwa Sh. 1,545,629,529/=. (iv) Fedha za Mkakati wa Kupambana na Ukimwi (*NMSF*) zinazosimamiwa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi kwa ajili ya utekelezaji na usimamizi wa kazi za Tume ya Kudhibiti Ukimwi hazikutolewa na Hazina. Kiasi hicho kilibaki kwenye akaunti ya Hazina bila maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo wa Kamati kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Matumizi ya Fedha za Ukimwi. Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali hazitolewi kwa wakati. Aidha, pale zinapotolewa kwa wakati uzembe wa baadhi ya watendaji hukwamisha utekelezaji wa afua za Ukimwi ambapo fedha nyingi hubaki katika akaunti bila kutumika kama zilivyokusudiwa katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
mwaka wa fedha husika. Kuchelewa huku kunafanya malengo mbalimbali kutofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndiyo yenye jukumu la kuratibu Programu ya Fedha za Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Ukimwi (NMSF). Utekelezaji wa Programu hizi unafanyika kupitia Sekretarieti za Mikoa pamoja na Halmashauri zote Tanzania Bara. M h e s h i m i w a Mwenyekiti, upo Mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wa namna ya utumiaji na ugawaji wa fedha za Ukimwi kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufuatilia utekelezaji wa utumiaji na ugawaji wa fedha za Ukimwi kwenye Halmashauri mbalimbali nchini, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya Mikoa na Halmashauri mbalimbali za Miji, Wilaya na Vijiji. Katika ziara hizo, Kamati iliweza kubaini yafuatayo:-

(i) Kamati imebaini kwamba Kamati za Ukimwi katika ngazi zote zipo ila hazifanyi kazi ipasavyo na kuna upungufu mkubwa wa fedha ngazi za chini.

(ii) Baadhi ya waratibu wa Mikoa na Wilaya ambao wana wajibu wa kuzijengea uwezo Kamati za Ukimwi za Halmashauri, Kata, Vitongoji na Vijiji hawatekelezi wajibu wao, hali iliyopelekea Kamati hizi kutokutana na kufanya vikao kama utaratibu unavyoelekeza.

(iii) Ukosefu wa utashi wa kisiasa wa kushughulikia masuala ya Ukimwi. Kwa mfano, Mwongozo wa kudhibiti Ukimwi ngazi ya Halmashauri, unamtaja Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri kuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti Ukimwi katika Halmashauri husika. Muundo huu unakwamisha utendaji kazi wa Kamati hizi.

(iv) Baadhi ya Mikoa na Halmashauri hazina mkakati wa Halmashauri wa kupambana na Ukimwi.
(v) Hakuna uelewa wa kutosha kuhusu mfumo wa utoaji

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)
taarifa za afya zisizo za kitabibu (TOMSHA) katika
Halmashauri nyingi.

(vi) Hakuna uwiano wa thamani ya fedha (*value for money*) kwenye miradi ya kuwasaidia watu wanaoishi na VVU/Ukimwi.

(vii) Kuna uhaba mkubwa wa kondomu kwenye baadhi ya maeneo hasa vijijini ambapo kuna baadhi ya sehemu kondomu iliyotumika hufuliwa na kuanikwa na kisha hutumika tena na sehemu nyingine wananchi huuziwa paketi moja ya kondomu kwa Sh. 1,000/= badala ya Sh. 200/= hadi Sh. 500/=.

(viii) Ushirikishwaji hafifu wa wadau wa afua za Ukimwi katika ngazi ya Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu na changamoto zitokanazo na utumiaji na ugawaji wa Fedha za Ukimwi kwenye Halmashauri mbalimbali nchini, Kamati inashauri yafuatayo:-(i) Muundo wa Halmashauri unaomtaka Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ukimwi ya Halmashauri ubadilishwe ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji. Kamati inashauri nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Udhhibiti Ukimwi ngazi ya Halmashauri isitokane na nafasi aliyonayo bali Mwenyekiti achaguliwe miongoni mwa Wajumbe kutokana na utashi wa kisiasa alionao katika kupambana na Ukimwi. (ii) Kuwepo kwa Mwongozo utakaozitaka Halmashauri zote nchini kuwa na Mpango na Mkakati wa Kupambana na Ukimwi katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya Utafiti wa Viashiria vya VVU/Ukimwi kwa Mwaka 2011/2012 uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonesha kwa ujumla kiwango cha maambukizi ya Ukimwi Kitaifa kimepungua kutoka asilimia 5.7 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 5.1 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kiwango cha maambukizi kimkoa kinaongozwa na Mkoa wa Njombe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
ambao una kiwango cha juu cha maambukizi cha asilimia 14.8, ukifuatiwa na Mkoa wa Iringa wenye asilimia 9.1 ikilinganishwa na wastani wa Taifa ambao ni asilimia 5.1 kwa mujibu wa takwimu za viashiria vya VVU/Ukimwi (DHS 2012). Aidha, utafiti huu umeonesha kiwango cha maambukizi ni kikubwa miongoni mwa wanawake kwa 6.2% ikilinganishwa na wanaume ambao ni 3.8%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea Mkoa wa Njombe ilifurahishwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo na Taasisi zisizokuwa za kiserikali ikiwemo kufanya tohara kwa wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi, mkoa peke yake hautuweza kumaliza tatizo hili; hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuwa na mpango mahususi wenye matokeo makubwa na siyo *business as usual* na badala yake kuanza mikakati ya *business unusual* ili kufikia lengo la maambukizi sifuri ifikapo 2015. Hii ni pamoja na Mikoa mingine yenye maambukizi makubwa kama Iringa, Mbeya na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema taarifa hizi za utafiti wa viashiria vya VVU/ Ukimwi zikasambazwa na kufafanuliwa kwa jamii ili jamii iweze kufahamu ukubwa wa tatizo la Ukimwi na jinsi ya kukabiliana nalo.

Wanawake ambao ni kundi maalum katika jamii wana maambukizi ya kiwango cha juu ukilinganisha na wanaume, hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuandaa programu maalum zitakazolenga kushughulikia masuala ya Ukimwi kwa wanawake au wasichana na vijana na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilishughulikia masuala yanayohusu Ukimwi katika Sekta ya Uvuvi. Sekta ya Uvuvi huchangia Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 1.4 Kamati ilipofanya ziara Mkoa wa Mara, Wilaya ya Butiama katika Vijiji vya Busekela na Bukima, ilielezwa kuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)
wakati wa msimu wa giza kila mwezi dagaa wengi huvuliwa. Kijiji cha Busekela pekee hupokea takribani wafanyabiashara 3,000 - 5,000 kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi zikiwemo nchi za Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Watu wa Kongo. Aidha, taarifa za Mkoa zilithibitisha kwamba, maambukizi ya VVU/Ukimwi Mkoani Mara huchangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia Sekta hii, Kamati imebaini kwamba:-

(i) Shughuli za uvuvi ni shughuli za msimu ambapo watu mbalimbali hukutana kipindi ambacho dagaa au samaki wanapatikana kwa wingi. Mwingiliano huu unahatarisha afya za wenyeji, wageni na wavuvi na hivyo kupelekea magonjwa ya mlipuko na ongezeko la kasi ya maambukizi ya Ukimwi.

(ii) Hakuna juhudi za makusudi zilizochukuliwa na Serikali ili kuhakikisha wavuvi, wenyeji na wageni wanaokwenda maeneo ya uvuvi kununua na kuvua samaki au dagaa wanapata huduma za afya zikiwemo huduma za upimaji wa VVU/Ukimwi.

(iii) Hakuna mkakati maalum ulioandaliwa na Serikali wa kushughulikia tatizo la maambukizi ya Ukimwi kwenye maeneo ya Uvuvi.

(iv) Kijiji cha Busekela kilichopo Halmashauri ya Butiama hakina Zahanati ya kuwahudumia wenyeji wa kijiji hicho na wageni wanaokuja kuvua na kununua dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Ukimwi kwenye Sekta ya Uvuvi: Kutokana na umuhimu wa uvuvi katika nchi yetu, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kamati inaupongeza Mkoa wa Mara kwa kuwa na mkakati wa Mkoa wa Kupambana na Ukimwi. Hata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
hivyo, juhudi hizi hazitafanikiwa kwa kuuachia mkoa peke yake. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuusaidia Mkoa huu pamoja na mikoa yote inayozunguka Ziwa Victoria pamoja na mikoa mingine yenye shughuli za uvuvi.

(ii) Kamati inapenda kufahamu kuna programu gani za masuala ya Ukimwi zilizoanzishwa au kuandaliwa kwenye maeneo ya Mkoa wa Mara na vijiji vyote vinavyojishughulisha na uvuvi.

(iii) Kamati inaishauri Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, TAMISEMI na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, zishirikiane katika kusaidia na kuanzisha Programu Maalum za Ukimwi kwenye maeneo yote ya uvuvi ya kando kando ya Ziwa Victoria.

(iv) Serikali isaidie Serikali za Vijiji vya Busekela na Bukima kuwa na Mkakati wa Kupambana na Ukimwi sehemu za uvuvi.

(v) Waratibu wa kudhibiti Ukimwi wa Mikoa watekeleze wajibu wao kwa kufuatilia Halmashauri na Serikali za Vijiji ili kuweza kufahamu changamoto zinazowakabili katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Aidha, Tume ya Kudhibiti Ukimwi iwajengee uwezo Wenyeviti wa Serikali za Vijiji.

(vi) Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, isaidie kujenga kituo cha afya na kupeleka wataalam wa afya katika Kijiji cha Busekela, ambacho hupokea wageni takribani 3000 - 5000 kutoka nchi za Rwanda, Burundi, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo wakati wa msimu wa kuvua dagaa au samaki kila mwezi kwani hakina huduma ya Zahanati ya Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukimwi kwenye Sekta ya Madini. Sekta ya Madini ni moja ya Sekta zinazojumuisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
mkusanyiko na mwingiliano mkubwa wa watu kutoka sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Afrika Kusini utafiti unaonesha kuwa, Sekta ya Madini ndiyo inayoongoza kwa wafanyakazi wake kuambukizwa na kuishi na Virusi vya Ukimwi. Katika nchi ya Zambia asilimia 18 ya wafanyakazi wa Migodi ya Shaba wanaishi na Virusi vya Ukimwi. Vilevile nchi ya Botswana ambayo inazalisha almasi kwa wingi, theluthi moja ya wafanyakazi wa migodi ya almasi wanaishi na Virusi vya Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania hakuna takwimu sahihi kuhusu hali ya maambukizi ya Ukimwi kwenye maeneo ya migodi ingawa utafiti uliofanywa na *African Medical and Research Foundion (AMREF)* katika Mji wa Geita na maeneo yanayozunguka Mgodi wa Ashanti zinaonesha kuwa, asilimia 16 ya wanaume na asilimia 18 ya wanawake wa eneo hilo wanaishi na VVU/Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa migodini huishi maisha ya kuhamahama ambayo huvuruga utaratibu wa kuishi kifamilia. Wengi wao huishi kambini kwenye mahema na hawana nafasi ya kujumuika na jamii zingine kwenye masuala ya kijamii na kimichezo. Hali hii hupelekea wengi wao kuanzisha mahusiano mapya ya kimapenzi miongoni mwa watumishi wenzao na wanajamii wanaoishi jirani na migodi, mahusiano ambayo huchochea maambukizi mapya ya VVU/Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia Sekta ya Madini, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Kazi ya utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta imeanza na inategemea kuajiri watu wengi zaidi hususan vijana na hakuna maandalizi yoyote yaliyofanywa na Serikali kuhakikisha vijana ambao wamesomeshwa kwa gharama kubwa afya zao zitalindwa ili waendeele kulitumikia Taifa.
(Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]

(ii) Tangu kuanza kwa shughuli za uzalishaji madini kwenye migodi, uzalishaji gesi na mafuta, hakuna mpango mkakati wa kupambana na Ukimwi ulioandaliwa kwenye maeneo hayo pamoja na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo.

(iii) Kamati ilipokutana na Wizara kuhusu kujadili masuala ya Ukimwi kwenye Sekta ya Madini, ilibaini kwamba watendaji wa Wizara hawafahamu kama nchi nyingi duniani zenye shughuli za migodi watumishi wake wanaongoza kwa maambukizi ya VVU na vifo vitokanavyo na Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kunufaika na Sekta ya Madini, mafuta na gesi, inahitajika kuwepo na mipango makini na usimamizi thabiti katika nyanja zote. Kwa upande wa masuala ya Ukimwi, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Wizara ya Nishati na Madini ifanye utafiti kujua nchi nyingine zinazozalisha mafuta, gesi na uchimbaji wa madini zimetumia mikakati gani katika kupambana na maambukizi ya Ukimwi migodini na kwenye uzalishaji wa gesi na mafuta.

(ii) Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iandae mpango mkakati wa kupambana na Ukimwi kwenye maeneo ya uzalishaji gesi, mafuta na migodi. Mpango huo uhusishe maeneo yote ya vijiji vinavyozunguka migodi ambapo mabomba ya mafuta na gesi yatapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhusiano uliopo baina ya ukatili wa kijinsia na Ukimwi. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa ukatili wa kijinsia (*Gender Based Violence - GBV*) ni chanzo cha maambukizi ya VVU/Ukimwi. Ukatili wa kijinsia unajumuisha unyanyasaji wa kimwili, kiuchumi na kisaikolojia. Kwa mfano, madhara ya vitendo vya mila potofu kama vile ndoa za utotoni na ubakaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto ya ukatili wa kijinsia ni vyema Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
ikaboresha na kushirikisha programu za mafunzo ya kada mbalimbali zinazotolewa kwa wafanyakazi wa huduma ya afya, Polisi na viongozi wa jamii ili kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini ikiwa huduma hizi zitaunganishwa pamoja na kurekebisha kanuni za kibaguzi, sheria na sera zinazohusiana na haki za mali pamoja mila kandamizi kama ukeketaji, zitasaidia kupunguza ukatili huu wa kijinsia na hatimaye kupunguza maambukizi mapya ya VVU/Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi kwa kuanzisha Dawati la Jinsia kwenye vituo vyote vya polisi ambalo kazi yake kubwa ni kusikiliza malalamiko na kupokea taarifa kuhusiana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mahusiano yaliyopo kati ya ukatili wa kijinsia na Ukimwi. Ili kupunguza maambukizi mapya ya VVU/Ukimwi Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kamati inaitaka Serikali kuwaelimisha wananchi kuhusu shughuli na umuhimu wa dawati la jinsia lililoanzishwa na Jeshi la Polisi. Aidha, Kamati inatoa wito kwa wananchi kutumia madawati hayo ya jinsia yaliyoanzishwa katika maeneo yao.

(ii) Kuanzishwa kwa vituo vya kuwahudumia wahanga wa ukatili wa kijinsia ili vitumike kuwahifadhi wahanga hao kwa muda ili waweze kupata msaada wa kisheria na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madereva wa magari ya masafa marefu ni kundi lingine linalochangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maambukizi ya virusi vya Ukimwi hapa nchini. Madereva wa masafa marefu wanakabiliwa na changamoto ya kuwa mbali na familia zao kwa kipindi kirefu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kudhibiti Ukimwi kwa kushirikiana na Asasi ya IOM na Chama cha Madereva wa Masafa Marefu, inatoa ushauri wa namna ya kujikinga na maambukizi ya Ukimwi kwa madereva wakati wanapokuwa safarini. Tume ya Kudhibiti Ukimwi imeweza kujenga vituo vya kupumzika madereva vijulikanavyo kama *One Stop Border Posts* ambavyo hutumiwa na madereva kupumzika, kupata ushauri na kupima afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea kituo cha kupumzika madereva wa masafa marefu kilichopo eneo la Mdaula, Wilaya ya Bagamoyo na Makambako. Katika ziara hiyo Kamati iliweza kubaini yafuatayo:-

(i) Kituo cha Mdaula kimejengwa mbali na walengwa ambao ni madereva wa masafa marefu. Madereva wengi huegesha magari yao eneo la Chalinze, wakati kituo kimejengwa ambako hakuna eneo kubwa la kuegesha magari. Huu ni upotevu wa fedha na rasilimali za umma.

(ii) Kituo kimejengwa eneo la makaburini na hakuna uzio wa kutenganisha eneo la kituo na eneo la makaburi, hali ambayo inaongeza unyanyapaa, hofu na kutengwa.

(iii) Kituo kinakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi kama vitendanishi (*reagents*).

(iv) Wataalamu wa kituo hawana uwezo wa kutosha kutoa maelezo kuhusu Ukimwi, kinga na ushauri nasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vituo hivi viweze kuleta tija na kupunguza maambukizi mapya ya VVU/Ukimwi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kituo kilichojengwa eneo la Mdaula, karibu na makaburi kwa ajili ya madereva kupumzika na kupata huduma za ushauri nasaha, kihamishwe kutoka mahali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
hapo. Aidha, Tume ya Kudhibiti Ukimwi ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kupata eneo lingine sehemu ya Chalinze.

(ii) Kamati pia ilibaini kuwa gharama zilizotumika kujenga kituo hicho hazilingani na hali halisi ya kituo (*value for money*).

(iii) Watumishi wa vituo hivyo wajengewe uwezo ili kuondoa hofu ya kuzungumzia mambo yanayohusu VVU/ Ukimwi.

(iv) Muundo wa vituo vya kupumzika madereva wa masafa marefu viwe na ramani ya aina moja; kwa mfano, Kituo cha Makambako ni mfano mzuri wa kuigwa. Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Waraka wa Rais Na. 2 (2006) unaotoa mwongozo wa namna ya kuwahudumia Watumishi wa Umma wanaoishi na Virusi vya Ukimwi. Waraka huo unatoa mwongozo wa namna waajiri wanavyopaswa kuwahudumia Watumishi wa UMma wanaoishi na Virusi vya Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ili kufuatilia utekelezaji wa Waraka huo. Katika vikao hivyo Kamati ilibaini kwamba:-

(i) Kamati za Ukimwi mahala pa kazi zipo ingawa baadhi ya Kamati hizo hazikutani kufanya vikao kama mwongozo wa Kudhibiti Ukimwi mahala pa kazi unavyoelekeza.

(ii) Hakuna kiwango maalum cha fedha kilichotengwa na Serikali kwa ajili ya kuwahudumia watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi. Posho ya kujikimu hutolewa kwa jinsi mwajiri atakavyoona inafaa.

(iii) Ukosefu wa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]

(iv) Hakuna uelewa wa kutosha kwa watumishi kuhusu Waraka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Waraka wa Rais Namba 2 (2006) kuhusu namna ya kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU/Ukimwi. Ili kuweza kuendana na mabadiliko ya Ugonjwa wa Ukimwi, miongozo mbalimbali ya ndani, kanda na kimataifa na mabadiliko ya sayansi kuhusu Ukimwi, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i)Yafanyike marekebisho ya Sera ya Ukimwi.
(ii)Kuimarisha uwezo wa Kamati za Ukimwi.

(iii)Kuwepo na kiwango cha chini kitakachotamkwa na Serikali kwa ajili ya kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU/Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kukutana na baadhi ya mifuko ya hifadhi za jamii ikiwemo *NSSF*, *PPF* na *LAPF* na kupokea taarifa ya jinsi mifuko hii inavyoratibu na kusimamia masuala mbalimbali yanayohusu Ukimwi kwa wafanyakazi na wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza *PPF* kwa kuwa na programu ya kusomesha watoto yatima ambao wazazi wao walikuwa wanachama wa mfuko kabla ya kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inapenda kutoa pongezi kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *NSSF* kwa kuwa na programu ya huduma za bima ya matibabu kwa wanachama wote bila ya kubagua ambapo watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi wanafaidika pia na huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii kubuni utaratibu mzuri ambao utasaidia wanachama wake na hivyo kusaidia juhudi za Serikali kuwahudumia watoto yatima na wanaoishi na Virusi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI) vya Ukimwi. Aidha, Kamati inawashauri Wananchi kujiunga na Mifuko ya Hifadhi za Jamii ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Bima ya Afya ili kupata matibabu kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF); kuna uhusiano wa karibu kati ya Ukimwi na umaskini. Ukimwi unaleta umaskini katika kaya kwani rasilimali za familia zinatumika katika kuuguza na kuongeza mzigo mkubwa wa watoto yatima na walio katika mazingira magumu. Umaskini pia unasababisha kuongezeka kwa maambukizi ya Ukimwi kwa kuwa jamii inajilingiza katika tabia hatari hasa kwa vijana na hususan watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzindua TASAF Awamu ya Tatu, ambayo ina programu zinazolenga kusaidia kaya maskini kwa kutoa fedha moja kwa moja, *cash transfer*. Hivyo, Kamati inashauri huduma hii isambazwe kwenye maeneo mengi kwani ina manufaa makubwa kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi kutengewa ruzuku itakayosaidia Baraza kuweza kujiendesha kwani limekuwa likiendesha shughuli zake kwa kutegemea fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi na wanaotumia dawa wanakabiliwa na lishe duni. Kamati inapongeza juhudi za Serikali za kuanzisha programu ya lishe ikiwa ni pamoja na kuhamasisha viwanda kuweka virutubishi kwenye unga na mafuta ya kupikia. Kamati inashauri elimu kuhusu lishe bora iendelee kutolewa katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na kuhamasisha viwanda vidogo vidogo kuongeza virutubishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia maambukizi sifuri, unyanyapaa sifuri na vifo sifuri vitokanavyo na Ukimwi ifikapo 2015 kama ilivyoazimiwa na Umoja wa Mataifa, Kamati inashauri Sheria ya Ukimwi ya Mwaka 2008 ifanyiwe marekebisho ili kuondoa unyanyapaa na ubaguzi kwa watu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]
wanaoishi na Virusi vya Ukimwi na familia zao. Kamati inashauri Sheria hii ifanyiwe marekebisho kwa kuviondoa vipengele vinavyochochea unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi. Vipengele hivyo ni:-

Kipengele namba 47 kinachohusu adhabu kwa mtu anayeambukiza Virusi vya Ukimwi kwa makusudi kinachosomeka; *"Any person who intentionally transmits HIV to another person, commits an offence and on conviction shall be liable to imprisonment to a term of not less than five years and not exceeding ten years."* Kipengele hiki kiondolewe kwani ni vigumu kubaini kama mtu amemwambukiza mwenzie kwa makusudi. Aidha, sheria hii pia inamuimiza mwanamke anayeishi na Virusi vya Ukimwi ambaye anaweza kumwambukiza mtoto wake tumboni au wakati wa kunyonyesha (PMTC).

Kipengele Na. 21 (a) kinachosema: *"Mtu yeyote mara anapopima na kugundulika kuwa anaishi na Virusi vya Ukimwi anatakiwa kumwambia mwenzi wake mara moja kuhusu hali yake; Any person who has knowledge of being infected with HIV after being tested shall immediately inform his spouse or sexual partner of the fact."* Kifungu hiki kinanyanyapaa watu wengi wanaokuwa wa kwanza kupima na kukutwa na Virusi vya Ukimwi hasa wanawake na wenzi wao kuwalaumu kuwa wao ndiyo walioleta janga hili katika mahusiano yao na kusababisha ukatili wa kijinsia na kuondoa usiri. Kamati inaona kama huu ni ukiukwaji wa Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakipongeza Chama cha Wabunge cha Kupambana na Ukimwi (TAPAC), kwa kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge kuhusu Ukimwi. Mafunzo hayo ya siku mbili yalishirikisha pia Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kutoka Ofisi ya Bunge pamoja na Makatibu wote wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapongeza utashi wako kwa kutenga muda kwa ajili ya Wabunge na Watendaji

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)
wa Ofisi ya Bunge kujadili masuala ya Ukimwi. Kamati inapendekeza kwamba, kwa sababu elimu ya Ukimwi mahala pa kazi katika taasisi hii inahusu Wabunge na Watumishi, ni vyema Bunge liongeze bajeti kwa ajili ya mkutano wa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi inalo jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Serikali kuhusu Sera na Mipango ya udhibiti wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati iliweza kukutana na taasisi na vyombo mbalimbali vyenye mamlaka ya kushughulikia masuala yanayohusu dawa za kulevya. Vyombo na taasisi hizo ni pamoja na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Kikosi Kazi cha Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ina jukumu la kusimamia mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kupunguza upatikanaji, matumizi na madhara. Tume imekuwa ikifanya kazi ya kubaini na kuharibu mashamba ya bangi, kuzuia uvunaji wa mirungi, kuanzisha shughuli mbadala za kiuchumi pamoja na kuzuia biashara haramu ya dawa za kulevya kwa kuteketeza dawa zilizokamatwa na kuzuia uchepushwaji wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevya na kuzuia utengenezaji haramu wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Serikali katika kupambana na dawa za kulevya kwani kasi ya ukamataji wa dawa hizo imeongezeka, kuteketezwa kwa kiasi kikubwa cha mashamba ya bangi, kutambua na kudhibiti njia mbalimbali zinazotumika kupitisha na kusafirisha dawa ya kulevya. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokutana na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya iliweza kubaini changamoto zifuatazo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]

(i) Tume haina mamlaka ya kisheria ya kufanya uchunguzi, ukamataji na upekuzi katika kesi zinazohusu dawa za kulevya. Mamlaka hayo vimepewa vyombo vingine vya dola kama Polisi, Uhamiaji na Idara ya Ushuru na Forodha.

(ii) Adhabu za kisheria zilizoainishwa katika Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya ni ndogo ukilinganisha na ukubwa wa makosa. Hali hii imepelekea kuendelea kushamiri kwa biashara ya dawa za kulevya.

(iii) Sheria iliyopo haibainishi wazi kuhusu utaratibu mzuri wa kuwalinda watoa taarifa za siri kuhusiana na biashara ya dawa za kulevya.

(iv) Sheria iliyopo inatumia thamani ya dawa za kulevya kama kigezo cha kutoa dhamana na adhabu na hivyo kuleta ushawishi kwa watu wengine kujingiza katika biashara hiyo.

(v) Tume haina bajeti ya kutosha kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(vi) Kushamiri kwa kilimo cha bangi pamoja na kilimo hicho kufanyika katika maeneo yasiyofikika kiurahusi.

(vii) Uhaba wa fedha za kufanyia kazi.

(viii) Ukubwa wa mipaka ya nchi.

(ix) Ukosefu wa nguvu ya kisheria kuweza kushughulikia wahalifu.

(x) Ukosefu wa motisha kwa wafanyakazi wa kikosi kazi.

(xi) Ucheleweshwaji wa kesi zinazohusu dawa za kulevya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu ya Serikali una jukumu la kutoa ushahidi wa kitaalam (*expert witness*) kwenye kesi za jinai zinazohusiana na dawa za kulevya, vielelezo vya makosa ya jinai na kutoa ushahidi wa kitaalam kwenye mamlaka husika kama Jeshi la Polisi na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Katika ziara hiyo Kamati iliweza kufahamu kazi nzuri zinazofanywa na Wakala hususan shughuli za uchunguzi wa vielelezo vya dawa za kulevya na vinasaba. Hata hivyo, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (i) Uchakavu mkubwa wa majengo.
- (ii) Ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu yake.
- (iii) Uhaba wa watumishi wakiwemo wataalamu wa kutumia mitambo ya kisasa ya kutambua dawa za kulevya.
- (iv) Ukosefu wa mapato ya Wakala kutoka Taasisi za Serikali zinazopata huduma ya Wakala.
- (v) Maslahi duni ya Watumishi wa Wakala ukilinganisha na ugumu wa kazi wanazofanya.
- (vi) Usalama mdogo wa wataalam wakati wa kutoa ushahidi kwenye vyombo vya sheria.
- (vii) Madhara ya kiafya kwa wataalam wakati wa kufanya uchunguzi na wakati wa kutoa ushahidi kwa kuwa hutakiwa kuhakiki vielelezo mahakamani.
- (viii) Mahitaji makubwa ya huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)]

(ix) Uhaba wa wataalam na miundombinu ya kuwezesha utoaji wa huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

(x) Kushamiri kwa kilimo cha bangi pamoja na kilimo hicho kufanyika katika maeneo yasiyofikika kiurahusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu vita dhidi ya mapambano ya dawa za kulevya.

(i) Serikali iharakishe mchakato wa kutungwa kwa Sheria mpya ya kuzuia na kupambana na dawa za kulevya.

(ii) Serikali iharakishe mchakato wa kuunda chombo maalum kitakachoshughulikia masuala ya dawa za kulevya.

(iii) Serikali ianzishe mahakama maalum kwa ajili ya kushughulikia makosa ya dawa za kulevya.

(iv) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa mamlaka zote na taasisi zinazoshughulikia masuala ya dawa za kulevya.

(v) Kusomesha na kuajiri wataalam wa kutosha kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.
(vi) Kamati inaitaka Serikali kuharakisha upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya.

(vii) Tatizo la dawa za kulevya litangazwe kuwa janga la taifa ili kuleta hamasa kwa Wananchi kushiriki katika mapambano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matibabu ya *Methadone* kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha huduma ya *methadone* kwa waathirika wa dawa za kulevya. *Methodone* ni dawa inayosaidia watumiaji wa dawa za kulevya kuacha kutumia dawa hizo bila kupata madhara. Huduma hii kwa sasa inapatikana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)
Mwananyamala. Aidha, Kamati inaipongeza Manispaa ya Temeke kwa kushirikiana na Shirika la Madaktari wa Ulimwengu (*Medicine Du Monde – MDM*) kuanzisha huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU/Ukimwi kwa wanaojidunga sindano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kutumia fursa hii kuwahakikishia Watanzania kwamba, tiba ya dawa ya *methodone* ni salama na haina lengo la kuhamasisha matumizi ya dawa za kulevya kama inavyosemekana miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kuwa huduma hii inakuwa endelevu. Vilevile Kamati inaishauri Serikali kuanzisha huduma hii katika hospitali zote za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kuwajengea uwezo kwa kuwapa mafunzo na mitaji itakayowawezesha waathirika wa dawa za kulevya kuweza kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa kujitolea kuwa mlezi kwa walioacha kutumia dawa za kulevya. Hatua hii inasaidia kupunguza unyanyapaa kwa walioacha kutumia dawa na kuwafanya wengine wajitokeze kupata matibabu ili kupunguza maambukizi mapya ya Ukimwi. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha programu ya *Methodone* pamoja na huduma kwa wanaojidunga sindano na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza na mfano wa kuigwa Barani Afrika. Hatua hii inaonesha utashi wa hali ya juu wa kisiasa (*political will*), jambo ambalo limepelekea Mataifa mbalimbali kuja kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, kwa kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na ushirikiano. Aidha, kwa namna ya pekee, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutoa shukrani za dhiti

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI)
kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwenye ofisi yako Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) - Mheshimiwa William V. Lukuvi na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuipatia Kamati ushirikiano mkubwa wakati wote wa kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashillah pamoja na Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Abdallah Hancha na msaidizi wao Ndugu Halima Laizer, kwa ushirikiano walioipatia Kamati kuratibu shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kuyakubali Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. SARA MSAFIRI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa asubuhi hii, tutaanza na Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Misanga na Mheshimiwa Mrema.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza ya kuchangia. Kabla ya kuchangia, kwa mujibu wa Mwenyekiti aliposoma hii Taarifa ni kwamba, Taarifa hii ya Uchumi, Viwanda na Biashara inasimamia Taasisi jumla ya 57. Sasa ni dhahiri kwamba, kuchangiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA]

leo asubuhi na tukamalizia leo siku moja, hatutaitendea haki Kamati hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Kamati za Hesabu za Serikali, Kamati ya LAAC na Kamati ya Bajeti ilichukua muda wa siku nne toka tarehe 6, 7, 10 na 11, tunachangia kwa sababu ya umuhimu wa Taarifa ya Kamati zile. Tukiangalia ratiba yetu Kamati ya Miundombinu na Nishati na Madini pia imepewa siku mbili. Sasa hii ya Viwanda, Uchumi na Biashara ambayo ndiyo *backbone* ya uchumi wa nchi na maendeleo ya nchi, inapewa siku moja au nusu siku. Sasa *okay*, yakimwagika hayazoeleki, lakini hebu tujifunze kwamba mara nyingine jambo hili tulifikirie kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiti na Kamati ya Uongozi waone umuhimu wa Kamati hii ambayo inasimamia Wizara tatu na Taasisi 57. Hilo lilikuwa la kwanza na lililoharibika, litengenezwe kwa mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika taarifa hii ya Kamati, imezungumzwa kuhusu utitiri wa mabenki, kwamba, tuna mabenki 51 hapa nchini lakini ni benki mbili tu ambazo zinaonekana angalau vijijini au sehemu mbali ya Dar es Salaam ambao ni *CRDB* na *NMB* na zilizobakia zote zimejikusanya katika Mji Mkuu Dar es Salaam. Hata huo Mji Mkuu tunaosema Mji Mkuu wa Kiserikali unaojulikana Dodoma, zaidi ya benki 40 na kitu hazipo hapa.

Kwa hiyo, hapa kuna udhaifu fulani na tunajua hawa wamekuja kutafuta fedha ndiyo wawekezaji wenyewe, lakini sasa angalau nchi iwe na mipango kwamba hizi benki mtawanyo uwe vipi na benki 51 si nyingi mno? Mbona yako mataifa makubwa hayana utitiri wa mabenki huo? Au hawa wamekuta udhaifu gani hapa Tanzania kwamba hapa ndiyo shamba la bibi wanapokuja kuchota! Pamoja na wingi wa hayo mabenki, bado riba ni kubwa mno. Sasa ni jambo ambalo linashangaza. Kulikoni? (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA]

BoT kweli inaishauri Serikali ipasavyo, ukiacha hayo mabenki ambayo yanashughulikia mambo ya fedha, leo yamejichomoza pia makampuni ya simu yanashughulika na mambo ya fedha kwa kiasi fulani; *Tigo Pesa, M-Pesa, Z-Pesa, Air Tel Money*. Kwa hiyo, utakuta mbali ya biashara yao ya mawasiliano, lakini kwa upande mwingine ni kama Benki pia hizi sasa hivi.

Kwa hiyo, hatuzungumzii 51 tunazungumzia 55 na zaidi, lakini kuna tatizo katika haya Makampuni ya simu yanayoshughulikia biashara ya pesa. Hivi Benki Kuu wanashindwa nini hadi leo kusimamia haya Makampuni ya Simu kwamba leo kuna utumaji wa fedha tu hapa hapa tena mwingine unaweza ukatuma hadi laki tano, wengine mpaka milioni, lakini unatuma huna *receipt*. Wewe unayetuma huna *receipt*, anayepokea hapewi *receipt*. Kuna nambari tu pale ya Wakala. Hivi wangapi wanajua nambari ya Wakala? Tena hiyo nambari ukienda hapo kwa Wakala, inafichwa ile namba. Wangapi watakuwa wajanja wakajua umetuma pesa kwenye Wakala namba fulani fulani? Wangapi watakojua na kwa nini utume fedha mahali na halafu hakuna *receipt* yoyote? Huu udhaifu uondoke na hata hao *TRA* wanaosimamia kodi, hawa hawana hata hizo mashine za elektroniki; kitu gani kitawajulisha kwamba fedha ngapi zimetumwa na mimi niliyetuma fedha pale, mtakuwa na ushahidi gani kwamba nimetuma hizo fedha, mbali ya huo upotevu unaopotea? Suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa, kwa takwimu za zamani tunaambiwa limeongezeka kwa asilimia 15.2, hizo ni takwimu za Serikali kutoka trilioni 18 mwaka 2011 mwezi Desemba, mpaka trilioni 21 mwaka 2012, Desemba. Hili deni linaongezeka siku hadi siku. Leo nadokezwa kwamba tayari liko trilioni 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kipengele kikubwa ninachoshangaa, swali hili limeshaulizwa mara ngapi hapa Bungeni, lakini jibu la Serikali ndiyo nashindwa kulifahamu kwa akili yangu. Labda leo Serikali ije na jibu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA]

litakalokuwa zuri zaidi. Wabunge tukiuliza: Kwa nini deni la Serikali linaongezeka siku hadi siku na namna gani njia gani zitakazosababisha deni la Serikali lipungue? Majibu, kwa kweli yanasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninukuu majibu ya Serikali, hebu sikiliza. "Serikali inaendelea na utekelezaji na mkakati wa kusimamia Deni la Taifa ikiwa ni pamoja na kukopa katika vyanzo nafuu." Kwa hiyo, hiyo moja kwamba Deni la Taifa kulipunguza ni kuendelea kukopa katika vyanzo nafuu. Hiyo ndiyo njia moja ya Serikali katika kupunguza Deni la Taifa. "Aidha, Serikali ipo katika mchakato wa kuanzisha idara ya madeni ambayo pamoja na mambo mengine, itakuwa na jukumu la kujenga uwezo wa kufanya upembuzi yakinifu." Kuanzisha Idara ya Madeni.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Dah!
MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyaa, hiyo ni kengele ya pili. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, lakini dakika kumi pia hazitoshi.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrema na Mheshimiwa Mpina ajiandae.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya pili. Kwanza, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa taarifa yake nzuri, mambo ni mengi, muda ni mfupi, ameshindwa kumaliza, kama alivyosema, *Hansard* izingatie yote aliyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, naunga mkono yote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

yale ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisisitize masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini tunayo sera ambayo inatu-*encourage* kujenga viwanda, kufufua viwanda na kadhalika. Kwa kuwa muda ni mchache, niende moja kwa moja; ni jambo la kusikitisha kwamba, viwanda vilivyopo hapa nchini havilindwi kiasi kwamba, watu wanaanza kujuliza, hivi kuna haja ya kujenga viwanda vipya hapa nchini au tuendelee na utaratibu wa kuagiza bidhaa kutoka nje? Maana inaonekana sasa kuagiza bidhaa kutoka nje ni rahisi, ni afadhali kuliko kuwa na viwanda hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, umesikia malalamiko mengi; viwanda vya sementi vinalalamika kwamba sementi iko nyingi lakini inayoingizwa kutoka nje kwa urahisi na wakati mwingine hata kodi inayotakiwa kulipwa hailipwi. Sementi kutoka Pakistan inaingia bila kuzingatia taratibu na matokeo yake inauzwa kiurahisi tu. Sasa hawa ambao tumewapa nafasi ya ku-*invest* viwanda vya sementi hivi, wanajikuta wana mzigo ambao hausaidii. Viwanda vya sukari wanalalamika, sukari inaongezwa kiholela, Bodi yetu ya Sukari ile inatoa vibali kiholela, watu wanaingiza sukari tu. (*Makofi*)

Hivi sasa mafuta ya kula yanaingizwa kiholela tu, yapo mengi tu hapa wakati kuna alizeti, kuna pamba, kuna nini, mafuta yako mengi tu. Sasa mtu unajuliza, kuna haja gani ya kuvutia wawekezaji waje wa-*invest* viwanda hapa wakati hatuna utamaduni, hakuna sera nzuri ya kuwalinda au kulinda viwanda vyetu? Hii ni athari kubwa. Inasemekana, sijui, kwamba wakubwa humu ndani wamo kwenye vita kama hii ndiyo maana haichukuliwi hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni yangu kwamba kama tunataka tunufaike, lazima tuangalie tukataze kabisa kuingiza bidhaa wakati bidhaa hizi zinapatikana katika nchi yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

Hayati Mzee Nyerere miaka ile ya 1970 alipojenga vile viwanda, vingi tu; vya nguo na nini; wewe uliona viwanda vilivyokuwa vinafanya kazi, nguo zilikuwa zinapatikana. Wakati ule akina mama hawa kama hajapata Khanga ya Urafiki au MWATEX, hajafurahi bado. Leo nani anajali habari ya Khanga ya Urafiki? Nani anajali Khanga ya MWATEX? Watu wanakimbilia India, vinaingia, vitu vyenyewe havina thamani, anavaa siku mbili vimekwisha. Lakini kwa sababu sijui kuna masilahi gani, naiomba sana Serikali, kama tuko *serious* kuwakaribisha wawekezaji waje wawekeze, ni lazima tuwe na utaratibu wa kulinda viwanda vyetu. Vinginevyo, tuachane na dhana ya uwongo ya kwamba tunakaribisha wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia Kampuni ya India ya Bajaj walikuwa waje kuwekeza hapa, lakini inasemekana nao sasa wameshaanza kukata tamaa, kwa sababu wanaona ni afadhali waleta bajaj kutoka India watapata faida kuliko kuja kujenga kiwanda hapa Tanzania.

Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba, lazima Serikali ijiangalie upya namna ya kulinda viwanda vya ndani ya nchi. Nimetoa mfano wa sukari, sementi na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali ya CCM imebuni vitu vingi vya kumsaidia mwananchi kumwondolea umaskini wa kipato, lakini pia kumpa maisha mazuri. Tumetunga sheria hapa zinaitwa *Mortgage Financing* na *Lease Financing*, zote hizi zimetungwa ili zivasaidie wananchi.

Wote tunajua, kujenga nyumba kwa kijana ambaye ameanza kazi jana kutoka Chuo Kikuu siyo kazi rahisi na ndiyo maana baadhi yao, wachache maskini ya Mungu inabidi waingie katika njia nyingine za haraka haraka ili waweze kujipatia nyumba. Kama kweli hii *Mortgage Financing*, *Lease Financing* ingekuwa inafanya kazi sawasawa hata ingepunguza tamaa ya baadhi ya vijana wetu ambao wanataka wapate nyumba lakini uwezo wa kupata nyumba ni ghali. Wangepitia mikopo hii, wakapata.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

Lakini mpaka leo hii sheria imetungwa haijatekelezwa vizuri. Ukiuliza sababu unaambiwa eti bado hatujapata mkopo, tumeomba mkopo sijui *World Bank*, tumeomba mkopo sijui wapi na wapi. Hivi tulitunga sheria kwa kumtegemea *World Bank* aje atusaidie kutekeleza?

Mimi nadhani kama sheria ingekuja hapa ikasema kwamba sheria hii mkitunga lakini *subject* ya kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia, nadhani tungekataa, tusingelikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kama Serikali ya CCM inafanya kwa nia safi kutunga sheria, sera na nini za kuwezesha wananchi, kuwapunguzia umaskini na kuwawezesha kukaa vizuri kama ujenzi wa nyumba, halafu haitekelezwi, ni kiini macho na kuwahadaa wananchi. Siyo jambo zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo hii ambayo inakopwa kwenye mabanki ambayo sijui yameteuliwa machache sijui, mpaka leo bado ni asilimia 20, asilimia 19, asilimia 21 na kadhalika. Nani atakopa mkopo wa kujenga nyumba asilimia 20, 21? Wakati inatungwa sheria hii tuliambiwa kwamba mkipitisha sheria hii mambo ya mikopo ya kujenga nyumba itakuwa chini ya asilimia kumi, kumi na moja, kumi na mbili. Lakini mpaka leo ni *20 percent, 21 percent*; nani atamudu? Wewe unakufa una-*save interest* tu kabla hujaanza hata ile *amount* yenyewe ambayo inatakiwa. Kwa hiyo, hili nalo ni jambo la kuhadaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu tunalo Baraza la Uwezeshaji, linatakiwa lisaidie kuondoa kipato cha umaskini kwa wananchi kwa kutoa mikopo mbalimbali. Ipo mifuko 12, kwanza, ni mingi sana. Nimehesabu mifuko ile ipo *about twelve*, ni mingi sana, tuipunguze.

Vilevile hizo fedha ambazo zinatolewa kwa Baraza la Uwezeshaji ni duni. Waliomba Shilingi bilioni 385, wamepewa Shilingi bilioni mbili; hivi wafanyeje? Mtakuja kuwalaumu kwamba hawafanyi kazi sawasawa? Mtu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

anaomba Shilingi bilioni 385, unampa Shilingi bilioni mbili, halafu umtegemee afanye kazi yake sawasawa? Siyo sawa!

Sasa kama kweli tunaanzisha kitu na tuna nia ya kuwasaidia watu, tutekeleze basi yale makusudio ambayo yamefanya tuanzishe hicho kitu. Vinginevyo, tuache, tuchague vitu vichache ambavyo tuna uwezo navyo, tuvitekeleze. Tusilundike mambo mengi kwa majina tu ili tuonekane kama tuna hiki, tuna hiki na hiki, wakati kumbe hakuna jambo lolote ambalo linaweza likafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Baraza hili la uwezeshaji na Mifuko mingine hii inakopesha *SACCOS* zetu na *VICOBA* asilimia 11. Sasa asilimia 11 wenyewe *SACCOS* wanakopesha asilimia 15, wengine 16. Kwanza, hakuna *uniformity*. Ningeomba kabisa hapa kwamba, mamlaka inayohusika kama ni Baraza litoe maelekezo *interest* iwe kiasi fulani, siyo kumwachia kila *SACCOS*, kila *VICOBA* kufanya anavyoona yeye inafaa. (*Makofi*)

Vilevile bado hata asilimia 11 ni nyingi. Ni maombi yangu kwamba ili kusaidia kweli *VICOBA* na *SACCOS*, *interest* inayotolewa na mifuko hii pamoja na Baraza la Uwezeshaji iwe chini ya asilimia 10 ili na wao wakiweka kidogo, angalau wanakuwa na asilimia 11, 12, unamsaidia yule mwananchi. Sasa unamtoza mtu asilimia 15!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaonea huruma sana akina mama ambao wamejiunga na *Pride*. Katika Mfuko unaosumbua akina mama hawa ni *Pride*. Kila wiki wapeleke, wakati mwingine wengine wanaingia gizani, wewe Mbunge sasa unajazia. Sasa mimi nadhani wanadhaliishwa akina mama hawa. Tuwaonee huruma. Kama tumeanzisha vyombo hivi kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, tuwe *serious* kuona kweli vitu hivi vinawasaidia wananchi. Kwa hiyo, *Pride* ni chombo kimojawapo ningeomba Serikali ikipigie macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni habari ya *dollarization*. Nchi yetu ni nchi ambayo ina matatizo. Ninyi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

nyote mnasafiri hapa. Ukifika tu *Airport* kazi ya kwanza ni kubadilisha dola, unaingia kwenye pesa zao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Muda umekwisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Missanga, nakushukuru. Ni kengele ya pili.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini haya mengine yazingatiwe. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mrema, atafuatiwa na Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Khatib Said Haji ajiandae.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema niliyokusudia kuyasema, naomba kwanza nimshukuru sana Mtukufu Rais, nimshukuru Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Bunge na Mawaziri waliopo hapa ndani pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliosindikiza mwili wa Marehemu Anselm Lyatonga Mrema, mdogo wangu, mpaka Kilaracha Marangu Moshi, wakahakikisha amezikwa kwa heshima zote zinazostahili. Ninasema ahsante sana ndugu zangu.

La pili, naomba niwashukuru sana wananchi wa Vunjo ambao walikuwa wananiombea wakati niko India nilipokuwa mgonjwa. Wakati wengine wanachekelea Jimbo lile liwe wazi, lakini nilikata rufaa kwa Mwenyezi Mungu na nasema hafi mtu hapa! Kwanza nimalize kipindi changu vizuri na Mungu aniongezee muda, niwaambie watu hawa wanaopitapita, nitagombea tena mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ningeomba nielekeze hili la kwanza kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Mimi nashindwa kuelewa ni kitu gani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA]

huwa wanafanya. Ninayo barua hapa ya Serikali ya tarehe 12 Agosti, 2013 ambayo ameandikiwa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda na barua hii ameandika Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ni vizuri ili tuweze kuisaidia Wizara hii na hasa Kamati hii inayounganisha Wizara hizi mbili; ya Ardhi pamoja na ile ya Viwanda. Inasema: "Uhakiki wa miliki ya ardhi na matumizi kwa ardhi kabla ya utoaji wa leseni. Tarehe 29 mpaka 30 Julai, 2013 nilifanya ziara ya kikazi Wilaya ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro.

Katika ziara hiyo nilitembelea kiwanda cha *Kilimanjaro Wines and Spirit* kilicho kwenye Mji Mdogo wa Himo. Madhumuni ya kutembelea kiwanda hicho yalikuwa ni kupata ukweli juu ya malalamiko yaliyowasilishwa na Mbunge wa Vunjo, Dkt. Augustine Mrema kuwa, kiwanda hicho kimejengwa kinyume na masharti ya hati miliki. Katika ukaguzi huo nilibaini mambo yafuatayo:-

Eneo lililojengwa kiwanda hicho lilitengwa kwa ajili ya matumizi ya *camp site* kwenye Mipango Miji. Hata hivyo, hati miliki ilitolewa kwa ajili ya biashara na makazi. Badala ya *camp site*, kimejengwa kiwanda cha vinywaji vikali bila kupata kibali cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Kiwanda hicho kinamilikiwa kwa ubia baina ya Watanzania na Wakenya, kwa uwiano wa asilimia 50. Kimesajiliwa na Wizara yako na kupewa leseni ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la kiwanda hicho limejengwa bila kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri ya Moshi, ambayo ndiyo Mamlaka ya Upangaji, bila kujali athari za kimazingira. Lngine lipo Pingamizi la wananchi wa Himo, wapatao 148 wanaopinga ujenzi wa Kiwanda katika eneo hilo.

Kwa maelezo haya, Wazari anaambiwa utaona kuwa ujenzi wa kiwanda hicho umekiuka Sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya Mwaka 1999, Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007 na Sheria za Mamlaka za Miji Na. 8 ya Mwaka 1982, Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA]

na Sheria ya Hifadhi ya Mazingira Na. 20 ya 2002. Hivyo, hakikustahili kupewa leseni kama ilivyofanywa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kitendo hicho kimesababisha usumbufu kwa wananchi wa Mji Mdogo wa Himo hususan wanaoishi karibu na eneo la kiwanda, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na Wizara zinazosimamia Sera na Sheria zinazotajwa hapo juu.

Hatua ya kutambua na kutoa vibali kwa kiwanda hicho ni kuunga mkono uvunjaji wa Sheria uliofanywa na mmiliki wa kiwanda hicho. Hii itaweka mfano mbaya kwa wananchi wengine wanaosababisha sheria za nchi kupuuzwa. Vilevile hatua hiyo inafanya Serikali ionekane kutokuwa na mshikamno katika usimamizi wa Sera na Sheria za nchi.

Mheshimiwia Mwenyekiti, nimeamua kulileta hili kwa sababu inaonekana kuna *contradiction* kati ya Wizara ya Viwanda na Masoko na Wizara ya Ardhi. Wizara ya Ardhi inaeleza Sheria zake zinatakiwa ziwe namna gani, lakini Viwanda na Biashara wanafanya vitu vingine. Naomba msaada, kwa sababu wananchi wale hawata kubali, wamekasirika na mimi nitakuwa sijatenda haki nikiwaona wale wananchi wanaamua kujichukulia sheria mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naomba Wizara nyingine iliyopo hapa Bungeni, ni kuhusu *KNCU*. Mambo yanayofanyika kule siyo mazuri. Nimejaribu kuomba msaada wa Wizara hii ya Kilimo, lakini sijapata majibu.

Mheshimiwa Waziri pamoja na kukitaja Chama cha *KNCU*, kwenye taarifa yako ya Bajeti na kuona ya kwamba kuna Taarifa ya Wakaguzi (*Evaluation Report*) kutokana na *Cooperate Audit and Supervision, Cooperation* inayosema kama ifuatavyo; yaani Ripoti ya Ukaguzi wa *KNCU* inasema kwamba, *KNCU* imepata hasara ya Sh. 3,483,000,000/= huku ikiwa na madeni yenye thamani ya Sh. 4,028,000,000/= na madeni ya Benki Sh. 846,000,000/=. Sasa hii ni Ripoti ya Ukaguzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba na nimeandika barua kwa Mheshimiwa Waziri, hawa watu walioifikisha *KNCU* pale wanachukuliwa hatua gani? Hawajibu. Hamtujibu sisi Wabunge. Sasa mnataka sisi tufanye nini? Au mnataka na mimi niungane na wenzangu niseme kuna baadhi ya Mawaziri hapa ni mizigo kwamba mwondolewe? Au niungane na wengine wale wanaofikiria labda kuna rushwa inayotembea katika nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii Ripoti ya Ukaguzi, nimemletea Mheshimiwa Waziri, nisaidie, *KNCU* inakufa. Wananchi wangu kahawa yao inakopwa kwa Sh. 150/= kwa kilo. Sasa nimkimbilie nani? Kwa hiyo, haya mawili...

*(Hapa kengekel illia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mrema, nakushukuru. Ni kengele ya pili.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja kama haya yatajibiwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said na Mheshimiwa Genzabuke ajiandae.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza mapato ya Serikali; hapa Bungeni, Serikali ilitueleza kunako mwezi Juni, wakati tunapitisha Bajeti ya Serikali kwamba, Sheria ya VAT ya Mwaka 1997 itafanyiwa marekebisho kuhusu namna ya kupunguza misamaha ya kodi na tukaambiwa kwamba Sheria hiyo ingeletwa hapa Bungeni mapema kabisa. Sasa naona tunaelekea kwenye Bunge la Bajeti, Sheria hii mpaka sasa haijaletwa. Wala Sheria nyingine zote zinazohusu kupunguza mismaha ya kodi haijaletwa, na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

muda siyo mrefu tunaenda kwenye Bunge la Bajeti bila haya yote kufanyika.

Sasa tunapata mgogoro mkubwa kwamba tunapozungumza hatuna mapato, Serikali haina mapato, lakini bado jitihada zetu hatuzioneshi katika suala hili na kuhakikisha misamaha ya kodi tunaipunguza kwa kurekebisha sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Bunge lako, naomba uiambie Serikali kwamba Bunge hili lisiingie katika Bunge la Bajeti kama hautaletewa mkakati wa Serikali wa kupunguza misamaha ya kodi ikiwa ni pamoja na kuleta marekebisho ya sheria ambayo yako hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niliongea hata kipindi kile ni suala la Uhamishaji wa Gharama (*Transfer Pricing*) kwamba, hili ni miongoni mwa mazoezi yanayofanywa na Makampuni makubwa hasa yenye Makampuni Tanzania hapa nchini, kutorosha fedha nyingi sana nje ya nchi kupitia katika Sekta ya Madini, Sekta ya Simu, Viwanda, pamoja na Mabenki. Tukasema, mpaka sasa hivi kwa mujibu wa Sheria ya Mapato (*The Income Tax of 2004*), kifungu cha 33(1)(2) kinazungumza suala la *Transfer Pricing*, lakini hakuna *guidelines* pamoja na *regulations* za usimamizi wa suala hili la *Transfer Pricing*.

Taasisi ya TRA wao walishamaliza kutengeneza hizi *Regulations* na *Guidelines* zipo kwa Waziri wa Fedha. Leo ni zaidi ya miezi minane zipo mezani kwa Waziri wa Fedha, lakini hazijawa *indorsed* na hazijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na hatujui sababu, kwa nini hazitangazwi kwenye Gazeti la Serikali? Sasa Waziri atakapokuwa anachangia, atuambie kwa nini hizi kanuni hazitangazwi, licha ya hasara kubwa ambayo Taifa linaingia hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na muda wetu ulivyo mfupi huu wa dakika kumi, nizungumzie suala la matumizi ya Dola za Kimarekani. Kwa kweli inasikitisha sana, *The Banking and Financial Institution Act, 2006* ipo wazi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

sana katika suala la matumizi ya fedha za kigeni hapa nchini. Tumekuwa tukisema muda wote, wasimamizi wa zoezi hili ni Benki Kuu, wanaosimamia suala la matumizi ya fedha hapa nchini, lakini tumeendelea kuona fedha za kigeni zinatumiwa sambamba na *Tanzanian Shillings*. Licha ya Wabunge wote kulalamika, licha ya wananchi wote kulalamika, lakini hatuoni mabadiliko yakifanyika. Huwa tunajuliza tatizo ni nini? Sheria ipo wazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Hoteli zote zina-*quote* kwa Dola bila sababu zozote zile za msingi na wanalipwa Dola. Hakuna nchi yoyote hapa Afrika na sehemu nyingine ambayo inafanya mambo ya kitoto kama sisi. Ukienda *South Africa*, kwa namna yoyote huwezi ukaipata Dola bila maelezo ya kutosha kwa nini unataka Dola. Hotelini hawawezi kupokea, hata iwe kwenye Duka la namna gani hawawezi kupokea Dola. Dola unaipata *Bureau De Change* na Benki. Ni maeneo mawili tu. Lakini hapa kwetu zinauzwa kama karanga.

Ukienda kununua Dola hata leo, huombwi *Passport* ya kusafiria, huombwi *ticket*, wala kitambulisho, yaani mnauziana kama karanga! hakuna nchi ya namna hiyo. Huku tunazungumza kuporomoka kwa Shilingi ya Tanzania, lakini huku tunafanya mambo ambayo hayafanani na sisi. (*Makofi*)

Sasa najjuliza, hivi ni kweli Gavana wa Benki Kuu yeye hajui kwamba biashara hizo zinafanyika na Sheria anayoisimamia hajui? Tatizo ni nini? Kwa nini hatuchukui hatua za mara moja tu? Waziri alisema suala la kwanza ni *Dollarization*. Kaka yangu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mgimwa ni mgonjwa, nimwombe sana Mungu amponye, apate afya njema. Alisema la kwanza ni *Dollarization*. Akasema hii hatutakubali! Sasa najjuliza, haya maduka ni ya akina nani hao wakubwa kiasi kwamba hata Serikali imeelemewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba, kama Benki Kuu wameshindwa kusimamia, basi tutafute chombo kingine

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

au tufanye kila linalowezekana kuwafanya Benki Kuu waweze kusimamia. Lakini kama Benki Kuu wameshindwa kusimamia na Waziri wa Fedha naye ameshindwa kusimamia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji na uwezesaji kiuchumi. Katika eneo hili Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza suala la riba kubwa za Kibenki. Kuna maamuzi yaliyofanywa na Benki mwaka 2013 kwenye Bajeti, ukurasa wa 33 ukusoma walisema wameamua kupandisha riba ya mikopo ambayo wanatoa katika Taasisi za Fedha, wakapandisha kutoka asilimia 7.58 hadi asilimia 12.5, kwa Taasisi za Fedha, kwa kisingizio cha kwamba eti wanapunguza mfumko wa bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa tunalalamika na tunasema Benki Kuu, fanyeni kila linalowezekana kwa ajili ya kupunguza Riba za Mabenki. Lakini Benki Kuu ndiyo huyo huyo ambaye anachochea kupanda kwa riba katika Taasisi za Fedha. Sasa ongezeko la asilimia tano katika Tasisi za Fedha; hizi Taasisi za Fedha unataka zifanye nini? Asilimia tano zimeongezeka. Ni lazima kwa vyovyote vile Taasisi za Fedha zitatoza kwa gharama kubwa, kama unatozwa asilimia 12.58 lazima itakuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuzipa Benki hizi mtaji. Tuliambia *TIB* kuwapa Shilingi bilioni 500, kwa muda wa miaka mitano, leo hii tumebakiza Bajeti mbili tu, lakini Benki yetu, *Tanzania Investment Bank* mpaka sasa hivi tumeipelekea Shilingi bilioni 100 tu. Tulitakiwa tuwe tumepeleka Shilingi bilioni 300, lakini mpaka sasa tumepeleka Shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo ambayo nayo inasuasua kuanzishwa, nasikia sasa hivi imeanzishwa, lakini Benki nyingine kama vile *Tanzania Postal Bank*, pamoja na *Twiga Bank Corp*, zote nazo zina mgogoro mkubwa wa kuongezewa mtaji wake ili ziweze kuwa Benki za Biashara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza, ni kwa nini kila tunalopanga hapa tunashindwa kutekeleza? Tulisema ili Watanzania waweze kupata fedha za kuwekeza wao wenyewe, tutengeneze Taifa ambalo litakuwa na wazawa wenye kuwekeza na kwamba Benki yao ni hiyo *Tanzania Investment Bank*. Leo ni Shilingi billioni 100, tatizo liko wapi? Makusanyo yetu kwa mwaka 2012 tulifikia asilimia 98, karibia asilimia 100 kabisa, kwa nini hatukupeleka fedha hizo na sasa kwa nini hatujapeleka fedha hizo? (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Genzabuke.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, ninapenda kutoa pole kwa Mwanakamati mwenzetu, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mungu amjalie apate nafuu ili tuweze kushirikiana naye katika kulijenga Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kuwapa pole CCM, kwa msiba mkubwa uliowapata kule Mwanza, kwa kufiwa na Mwenyekiti wao Mstaafu - Mheshimiwa Clement Mabina. Upoe sana, Bwana ametoa na Bwana ametwaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanzia kutoa mchango wangu katika ukurasa wa 22 wa Hotuba hii. Napenda ni-*declare* kwamba, nami ni Mjumbe wa Kamati hii ya Uchumi, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 22, Ibara ya 2.4.3, hapa Kamati inaelezea kuhusiana na Mipango ya *EPZ*. Nataka nijikite katika sehemu inayohusu Mradi wa *Tanzania and China Logistics*. Ni masikitiko yangu sana kuwa umuhimu wa Mradi huu, ambao ungelisaidia Taifa letu kutoa ajira kwa vijana 25,000 wa Tanzania, Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

imekuwa ikisuasua kulipa fidia kwa wakazi wa Kurasani. Jambo ambalo linapelekea pesa zinazobidi kulipwa kuzidi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali katika Mradi huu Tanzania ilitakiwa na inatakiwa ilipe fidia ili iweke eneo lile wazi ili wale Wafadhili wa Kichina waweze kuutekeleza na ilitakiwa kulipwa Shilingi bilioni 60. Katika kipindi cha miaka miwili, kutokana na kusuasua kwa Serikali kukamilisha kuwalipa wananchi wale, imepelekea deni lile lifikie Shilingi bilioni 94.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hasara na inaonekana kutokuwa tayari kwa Serikali katika kukamilisha yale mambo muhimu ambayo yako mbele yetu. Katika Sekta ya Viwanda siku zote tumekuwa tukisema na Serikali imekuwa ikilijua hilo kwamba, Viwanda ndiyo vitaliondoa Taifa hili hapa lilipo na kulisogeza mbele. Inapotokea Wafadhali kama hawa wapo tayari kuisaidia nchi katika jambo muhimu kama hili, ambapo Serikali imetakiwa kutoa eneo wazi, Mradi ambao kuna nchi jirani wanaumezea mate, lakini kwa huruma tu ya kuonekana Tanzania wapatiwe Mradi huu, Serikali mpaka sasa imeupatia Mradi huu jumla ya Shilingi bilioini 45, na kadiri muda unavyozidi kwenda ndivyo deni hili linavyozidi kukua.

Ninaiomba Serikali, kwa kujua kabisa umuhimu wa jambo hili, iweze kutenga fedha za kuwalipa. Pamoja na kuwasababishia wananchi wale matatizo makubwa ya kwamba hawawezi kuendeleza chochote na wapo katika hali ya kutokujielewa, bado Serikali inaendelea kupoteza pesa kwa kukidhi haja na *interest* inayotokana na kuchelewa kuwalipa wananchi wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nasikia Serikali imetoa pendekezo la kuwaambiwa wale Wafadhili kwamba, hiki kiasi kidogo ambacho tumelipa muanze Mradi katika eneo hili. Haya ni mambo ya kitoto. Wenzetu Mradi ule utatoa zaidi ya Shilingi bilioni 400, lakini sisi tunaposuasua

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

kufidia Shilingi bilioni 90, hii linatuletea shida. Naomba Wizara ilianganalie hili kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nigusie ukurasa wa 17, ambapo imezunguziwa suala la *TBS*. Nikiri ni kweli tulikwenda safari ya Dubai na Kamati na tulikagua Makampuni yanayokagua bidhaa. Nataka nimpongeze sana Mwenyekiti wetu na Wajumbe wenzangu kwa kullona hili kwamba, katika Makampuni tuliyoyakagua pale, Kampuni ya *Inter-Tech* haina sifa ya kuendelea kuwa Wakala wa *TBS*, wa kuweza kusimamia na kukagua mizigo inayokuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa vigezo kabisa. Kuna shehena ya *oil* ya magari iliyokamatwa Dar es Salaam na *TBS*, hii ikionekana ina *certificate* zote ambazo Kampuni hii imethibitisha kwamba, bidhaa zile zina ubora wa viwango. Jambo ambalo zilipokaguliwa kwa umakini zilionekana hazina ubora wa viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo taarifa kwamba *TBS* ilifanya Ukaguzi wa kushtukiza Dubai, kukagua baadhi ya *containers* ambazo tayari zilikuwa zimeshapakia mizigo. Miongoni mwa makontena yaliyokamatwa ni ambayo tayari yana *certificate* ya Kampuni hii ya *Inter-Tech*, yakionesha yamekagua bidhaa na zipo tayari kupakiwa na kuja nchini. Matokeo yake bidhaa hizo zilionekana hazina viwango hivyo. Mimi ninajiliza; hivi Mheshimiwa Waziri unangojea nini usiwashauri *TBS* ikaachana na Wakala huyu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kampuni ambayo tayari inaonekana matokeo ya ukaguzi wake hayaridhishi na hayana kabisa; kusema kweli tuseme wazi kwamba, hawakagui mizigo bali wanatoa *certificate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari tunazozipata kubwa sana za kuingiza bidhaa ambazo hazina ubora, wanaoumia zaidi ni wananchi masikini. Leo hii ukiingiza bidhaa za umeme, waya na *bulb*, ambazo hazikidhi viwango,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

wanaoumia ni wanyonge wanaonunua bidhaa hizo na baada ya muda mfupi vifaa vile vimekufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoingiza bidhaa za aina ya vyakula ambazo hazina viwango, tunaoumia ni sisi wote. Leo hii vitambi holela vimeongezeka. Ni matokeo ya kula vyakula ambavyo havikaguliwi. Vyakula hivyo vinaingia na kupitishwa, Watanzania wanakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Kampuni hii ya *Inter-Tech*, anayeogopwa ni nani? Kwa nini *TBS* imegundua udhaifu huu na haichukui hatua? Mnangojea nini? Mheshimiwa Waziri, nashukuru sana kwamba wewe sio miongoni mwa wale Mawaziri mizigo, lakini kuendelea kulifumbia macho hili, kuna hatari ya kuja kuwa Waziri kiroba. Naomba sana uchukue hatua, hii ni kwa faida ya wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ombi langu kwa Serikali. *TBS*, majukumu iliyonayo ni makubwa ya kuhakikisha bidhaa zinazolingia nchini mwetu zinakaguliwa na ukubwa wa nchi yetu unaleweka, lakini hadi sasa kuna tatizo kubwa pale la wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mamlaka zinazohusika zichukue hatua kama kweli tumedhamiria kuifanya nchi yetu isiwe soko la bidhaa hafifu. Tunaomba Mamlaka inayohusika ichukue juhudi za kuifanya *TBS* iwe na wafanyakazi wanaokidhi kutekelza majukumu yao ili tuondokane na nchi yetu kugeuzwa dampo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikitoa ombi mara nyingi na kwa bahati nzuri sana Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda ni Kamati ambazo zipo chini yetu, tunazisisimamia. Nimekuwa nikitoa ombi kutokana na malalamiko ya Watanzania wengi wanaoagiza magari yaliyotumika kutoka nje. *TRA* kukadiria bei kwa mujibu wa vigezo walivyoviweka bado tunasema ni tatizo na linaendelea kuwaumiza Watanzania wengi. Nimesema hili kwa sababu *TRA* wanaangalia mwaka lilipotengenezwa gari

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

lakini hawaangalii matokeo ya minada inavyokwenda katika nchi hizo.

Nilikuwa nimetoa pendekezo hapa na kusema kwamba, kwa sababu *TBC* ndiyo Mawakala wa kusimamia ubora wa viwango, ni kwa nini *TBC* asiwe Wakala wa kuthibitisha pia bei za magari wanayonunua Watanzania katika nchi zile? Hii ingeondoa kabisa tatizo. Hili ni ombi nalitoa.

Kama haiwezekani hilo, ni kwa nini *TRA* isiweke Mawakala angalau katika nchi zile tatu ambazo zinaleta magari Tanzania; nchi kama Japan, Dubai na Uingereza ili wakathibitisha bei za magari na kuondokana na dhuluma inayofanyika?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib, nakushukuru!

MHE. KHATIB: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Genzabuke na ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kafumu!

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Humu ndani tumekuwa tukiwaita Mawaziri ni mabomu, ni mizigo, ni mizinga na maneno mengine mengi. Mara nyingi tumekuwa tukikaa humu ndani wakati wa bajeti tunapitisha pesa kifungu kwa kifungu, tunafurahi na tunashangilia kwamba bajeti yetu imekwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema kwamba, Mawaziri wakati mwingine pesa hizi tunazozifikisha humu ndani pengine haziwafikii ndiyo maana utendaji wao unakuwa mgumu. Sasa nina swali moja tu, nataka nijue kwamba pesa hizi ambazo tunakuwa tunazipitisha hapa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE]

Bungeni, tatizo lipo TRA, Hazina au tatizo lipo BoT? Je, ni wapi ambapo pesa hizi zinavuja? (Makofi)

Kwa hiyo, mimi nataka nijue tu kwamba, pesa hizi zinakwenda wapi ili tuondokane na lawama ambazo tunalaumiana kila mara. Mara nyingi tumekuwa tukisikia kwamba, TRA wamekusanya pesa wamevuka lengo, lakini sasa pesa haziendi kwenye maeneo husika. Kwa hiyo, nataka pesa zote zinapokusanywa zipelekwe kwenye maeneo husika, zikajenge barabara na zikatengeneze reli ili mizigo iweze kusafiri kutoka kwenye maeneo husika kupelekwa sokoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipitisha kwenye bajeti pesa za barabara ya Kigoma – Nyakanazi, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa barabara hiyo bado ni kikwazo kikubwa. Kwa hiyo, naishauri Serikali tufanye haraka ili ahadi tulizoziahidi ziweze kutekelezeka kwa kutengeneza Reli ya Kati ili mizigo iweze kufika maeneo husika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu uwekezaji na uwezeshaji. Mara nyingi tumekuwa tukimsikia Mheshimiwa Mama Nagu anaimba uwekezaji na uwezeshaji. Wananchi wetu huko vijijini hawaelewi maana ya uwekezaji na uwezeshwaji. Mara nyingi wanajua uwezeshwaji ni kuwawezesha kipesa. Mimi nafikiri pamoja na juhudi ambazo tayari zimeshafanywa na Serikali, waendeleo kupelekewa elimu ya kuelewa maana ya uwekezaji na uwezeshwaji. Wanapewa elimu lakini bado elimu hii inatakiwa ipelekwe kwa kasi zaidi ili watambue fursa walizonazo na hatimaye waweze kukuza uchumi wao kwa kupitia fursa zinazowazunguka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu Benki ya TIB. Naomba Benki hiyo mtandao wake ufike katika kila Wilaya ili wananchi waweze kukopeshwa vifaa vya kilimo kupitia kwenye benki hiyo. Serikali kwa kuwasogezea karibu Benki

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE]

ya *TIB* wananchi wataweza kutumia fursa hiyo kwa kutumia Benki hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiuliza swali Bungeni tarehe 13 nilisema kwamba Benki nyingi zipo mjini na wanaonufaika sana ni wale ambao wameanzisha Vikundi vya *SACCOS* na *VICOBA* ambao wanaishi mjini kwa sababu Benki zipo karibu yao na hata leo asubuhi nilisimama kutaka kuuliza swali kwamba Benki zote zipo mjini hata Benki ya Wanawake ipo mjini. Nilikuwa nataka kuomba Benki hiyo nayo ipelekwe vijijini.

Sasa basi, naomba mwongezee Bbnki ambazo zina 100% na Serikali kama Benki ya *Twiga Bank* na Benki ya Posta, mzunguzee mtaji ili ziweze kufikisha lengo la shilingi milioni 15 kusudi *BoT* waweze kuwapa kibali hatimaye ziweze kuwa benki kamili za biashara. Kwa kuwa benki hizo zimeonesha ni jinsi gani zinajali kuwakopesha wanawake na vijana kupitia *VICOBA*, zikiongezewa mtaji zikawa benki za biashara zitaweza kufanya vizuri na wananchi wataweza kunufaika kupitia benki hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niendeleo kusisitiza kwamba, tuendeleo kufanya kazi kwa pamoja, tuendeleo kuihoji Serikali kwa utaratibu, kwa upendo na bila kuitana mizigo, tukiendeleo kutatua matatizo madogo madogo ambayo yanatukabili. Kwa sababu tukikaa humu ndani tukarushiana lawama, hatutaweza kufanya shughuli za maendeleo bali hata wale ambao ni Viongozi wetu tunakwenda kuwakatisha tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu viwanda vyetu vya ndani ambavyo vimekuwa vinazalisha lakini vinashindwa kufanya ushindani kutokana na bidhaa zinazotoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari inazalishwa katika viwanda vyetu na vijana wengi wameajiriwa katika viwanda hivyo. Naomba basi, pamoja na kwamba nafahamu ni biashara huria, kila mmoja anastahili kufanya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE]

biashara, lakini watu ambao wanatoa bidhaa kutoka nje kama sukari, mafuta na sementi walipe ushuru ili waweze kushindana na soko letu la ndani ili vijana wetu wasikose kazi kwa sababu wanatishiwa sasa kuachishwa kazi wale ambao wanafanya kazi katika viwanda vya Mtibwa na hata *Kagera Sugar*; kuna hatari ya kuja kuachishwa kazi wakati tatizo la ajira nchini ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana na sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kafumu, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter na Mheshimiwa Pindi Chana atamalizia katika kipindi cha mchana.

MHE. DKT. PETER D. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Kamati hii, wameleta Ripoti nzuri ambayo inatuwezesha na sisi kuchangia kwa maana ya kuwasaidia kutoa maoni yetu ili Serikali iweze kufanya vizuri zaidi katika Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia jambo moja tu linalohusu viwanda. Viwanda ni *engine* ya kukua kwa uchumi wa nchi yoyote. Nchi zilizoendelea kama Marekani na nchi za Ulaya, zilivyotoka kwenye Vita ya Kwanza na ya Pili ya Dunia zilielekeza nguvu zake zote katika kukuza viwanda kwa ajili ya kukuza uchumi wake. Wakati huo mchango wa viwanda katika uchumi huo ulikuwa chini ya 20% na ukakua mpaka ukafika zaidi ya 45% au 50%, mchango wa viwanda kwenye *GDP*. (*Makofi*)

Baada ya hapo, uchumi ulipokua Sekta ya *Services* au Huduma ikawa kubwa zaidi. Kwa hiyo, hizo nchi mchango wa viwanda ukateremka ukaenda mpaka 19%

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. PETER D. KAFUMU]

hata chini yake, lakini walianza na viwanda kwanza.
(Makofi)

Kwa hiyo, sisi nchi yetu ya Tanzania tulianza vizuri sana wakati ule wa Marehemu Baba wa Taifa, tulielekeza nguvu kwenye kufufua na kujenga viwanda kwa kusaidiwa na kwa kutoa fedha zetu wenyewe. Wakati dunia inabadilika kwamba twende kwenye uchumi huria, tukashauriwa na mataifa kwamba tubinafsishe viwanda vyetu ili viweze kukua, lakini bahati mbaya kubinafsisha ndiyo kulifanya kuu viwanda kwa sababu wale tuliowapa viwanda vyetu wakavitelekeza wakatumia kukopa, wakaviacha vinakufa na wengine wakahamisha hata mitambo. (Makofi)

MJUMBE FULANI: Kwelli!

MHE. DKT. PETER D. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama China sasa, mchango wake wa viwanda kwenye *GDP* yake ni zaidi ya 45% na *service industry* ni 49% hivi. Nchi zote za namna hii zinazoendelea sasa kama Saudi Arabia na Venezuela, mchango wa viwanda ni mkubwa zaidi kuliko mchango wa *services* na kuliko michango mingine. (Makofi)

Kwa hiyo, na sisi tunatakiwa twende huko, Serikali inatakiwa itengeneze mkakati maalum wa kufufua viwanda. *Industrialisation* ni kitu muhimu kweli, lakini sisi tunaacha tu, viwanda vimekufa tunaona ni kitu cha kawaida. Siyo jambo jema sana. (Makofi)

Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba, tutengeneze mkakati maalum wa kufufua viwanda. Wizara ya Viwanda na Biashara mna kazi kubwa. Viwanda vipo vingi, hata huwezi kuvitaja. Viwanda kama vya ngozi, *ginnery*, vya kuchambua pamba na hata viwanda vidogo vya Mang'ula vyote vimeondoka. Tunatakiwa tuvifufue.

Naiomba Serikali kwakweli itazame jambo hili kwa jicho tofauti kwa sababu tusipo-*industrialise* tutaachwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. PETER D. KAFUMU]

nyuma wakati wote. Tutazungumza mambo mengi lakini uchumi unaotokana na viwanda ndiyo unaotufufua. Tukishafufuka, sasa tunaweza kuendeleza mambo mengine. Sasa hivi tuna 25% mchango wa viwanda kwenye GDP Tanzania, tunatakiwa twende mpaka ifike 50% kwanza halafu baadaye tunaweza kurudi nyuma baada ya *services* na vitu vingine vikakua zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Kiwanda cha Kuchambua Pamba kule kwetu kilikuwa kinaitwa *Manonga Ginnery*. Ndugu zangu na kaka zangu Wasukuma wanajua *Manonga Ginnery* ndiyo kiwanda kikubwa cha kwanza baada ya Uhuru. Watu wote walikuwa wanakuja kuchambua Pamba kule Manonga Chomachankola. Kiwanda hicho ukifika sasa hivi kimekufa, kinasikitisha. Alipewa sijui nani, simfahamu. Lakini naiomba Serikali kama mtaweza, chukueni hicho kiwanda mturudishie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mweyekiti, Igembensabo, Chama cha Ushirika, Nzega, Igunga na hata Tabora kina uwezo. Hebu tupeni hicho kiwanda sisi tukiendeleze. Tutatafuta mbia na tutakifufua. Ukifika huko sasa hivi utashangaa, kiwanda kikubwa. Wakati wa uchaguzi nakumbuka tulikwenda hapo kupiga kampeni, wananchi wakasema jamani, Dkt. Kafumu unaona kiwanda chetu hiki? Wale wapiga kampeni akina *Doctor* walifanya kampeni kubwa sana na tukaahidi tutakifufua katika kipindi changu cha Ubunge.

Naiomba Serikali, tafadhalini sana, hebu tusaidieni ili mimi Ubunge wangu uweze kuendelea mwaka 2015 nipate kirahisi, vinginevyo tunawadanganya wananchi. Hatuwezi kuendelea tusipokuwa na viwanda. (*Makofi*) Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipenda kusema hayo na napenda kurudia, naiomba Serikali itengeneze mkakati maalum kwa ajili ya kufufua viwanda vyetu, viwanda vyote kabisa ninyi ni mashahidi ili Serikali yetu na ili uchumi wetu uweze kuendelea pamoja na mambo mengine. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunisikiliza.

MBUNGE FULANI: Unga mkono hoja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DKT. PETER D. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kafumu na sasa namwita Mheshimiwa Assumpter Mshama na Mheshimiwa Pindi Chana ajandae.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika masuala mawili yaliyopo mbele yetu, yaani uchumi na viwanda pamoja na masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea uchumi, unaongelea ni namna gani unaweza ukatumia maliasili au rasilimali zetu kwa uhakika na usanifu ili kupata matokeo mazuri ya hali ya watu husika.

Unapokuwa unasema uchumi umekua, uchumi huo unatakiwa uonekane katika hali ya watu wako. Sasa mimi naomba sana kwanza hili suala la kwamba uchumi wa Tanzania umekua, kama hauonekani kwa watu wako, huna haja ya kusema uchumi umekua. Kwa hiyo, naomba sana tuwekeze nguvu zetu sana kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongelea uchumi wa Tanzania au viwanda, huwezi kuachana na kilimo. Japo siyo Wizara ya Kilimo, lakini unapoongelea kiwanda cha sukari, unaoongelea kilimo, unapoongelea kiwanda cha pamba, unaongelea kilimo, upoongelea kiwanda cha koroshom unaongelea kilimo na unapoongelea viwanda vya matundam unaongelea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kilitokea katika Bunge la Bajeti, Wabunge wengi tulikimbilia kuona namna gani tunavyoweza kupata matrekta. Baada ya muda mfupi tu, matrekta yametoweka, watu wengine tumeshakusanya fedha kutoka katika Wilaya zetu, lakini tumeshindwa kupata matrekta na zana za kilimo hazipatikani kwa wakati unaotakiwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

Kwa hiyo, Tanzania, uti wa mgongo wa Taifa letu kwa uchumi unaangalia sana kilimo. Kwa nini Serikali imefuta utaratibu wa kupata matrekta? Maana juzi nilikwenda JKT, wanasema usituulize sisi, labda uiulize Serikali? Mimi naomba tuongeze matrekta kama ilivyokuwa kipindi kilichopita ili wananchi waweze kulima kilimo cha kisasa na baadaye tuweze kuona matokeo katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia viwanda vingi vilitaifishwa, lakini wale waliovichukua kama wenzangu walivyosema, watu walichukulia mikopo na walipomaliza kuchukua mikopo wakavitelekeza wakafanya vitu vingine.

Sasa naiomba Serikali inaonaje, kila aliyechukua kiwanda alikuwa ameandika *writeup* ya kwamba atakapochukua kiwanda, atafanya moja, mbili na tatu. Kwa nini Serikali isiwatake watu hao kutuonesha yale waliyoyaahidi kama yamefika na kama hayajafika, kwa nini tusikitaifishe tena hicho kiwanda basi tukawapa wale ambao wanaweza wakafanya mambo ambayo yamekusudiwa kufanywa katika viwanda hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kwa uchungu sana namna ambavyo tunashindwa kuwalinda watu ambao wamewekeza katika viwanda vyetu.

Juzi tu katika mchango wangu, narudia kwa sababu ni jambo ambalo linaniuma, kwa kuongezea tu; kiwanda chetu cha Sukari Kagera kimefanya mambo mengi na makubwa, mashamba, kimekopesha wananchi kulima.

Tuna *outgrowers* zaidi ya 100, lakini juzi ameshindwa kuwalipa kwa sababu ya namna ambavyo sukari inaingia nchini kwa mgongo wa nyuma. Sasa kama tuna sera ya kulinda viwanda vya ndani, halafu tunakuwa hatutekelezi sera hiyo, hivi tunategemea kweli hao watu waliowekeza kwenye viwanda waendeleo kuwa na nguvu ya kuwekeza kwenye viwanda?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

Jambo lingine ni kwamba, juzi ameshindwa kulipa *outgrowers* katika Jimbo langu la Nkenge; kisa, hana pesa. Sukari ipo kiwandani, na hata akipewa miwa hawezi kuwalipa. Inakuwa ni kama kukopeshwa, kama wakati ule wa kahawa. Sasa naiomba Serikali ije na mkakati maalum wa kufufua ile sera ya kulinda viwanda vyetu vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni umeshasikia mtu anatamani kufungua kiwanda kingine cha sukari? Tunapungukiwa zaidi ya tani 100 kwa mwaka ndiyo maana tunaingiza sukari. Lakini wawekezaji hawashindwi kujenga viwanda vingine. Wanashindwa kwa sababu hawana uwezo au hawana namna ya kuzuia au kudhibiti wale wanaoingiza sukari kwa mgongo wa nyuma. Matokeo yake sukari inadoda viwandani na wao wanashindwa kulipa mikopo na matokeo yake mwezi huu tarehe 30 kiwanda cha *Kagera sugar* kitapunguza watu 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vijana 3,000 wakitoka wakarudi Kijijini pale Misenyi tutawaweka wapi, kama sio wizi, udokozi na unyang'anyi utakaokwenda kuvamia Wilaya ya Misenyi? Mimi naomba wakati tunahitimisha hili suala la viwanda, Mheshimiwa Waziri aje kutueleza, anafanya nini kuhusu tatizo la uingizaji kiholela wa sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo linaloeleweka kabisa; una uwezo wa kusema tunahitaji sukari, lakini jukumu la sukari tuwapatie walio na jukumu la kutuingiza sukari kuliko kumpa mtu mwingine, sitaki kuwataja majina, lakini saa ikifika tutawataja ili waache kuchezea nchi hii, tuweze kufanya vitu katika utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niliwauliza watu wa *TRA* tukiwa tunaongea kwenye Kamati, nikauliza kwamba, hii sukari inayoingia kiholela tatizo ni nini? Wakasema wanaingiza kama sukari ya *brown*. Lakini na sisi tunashangaa, kama mtu wa *TRA* anashangaa kuona sukari inaingia nchini na haelewi, nani tumwulize habari ya kuingiza vitu holela nchini? Kwa hiyo, naomba sana, ili kunusuru Jimbo langu la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

Nkenge, tuje na tamko la nini kinafanyika kudhibiti uingizaji holela wa sukari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua, kuna viwanda vingi vya viatu vilichukuliwa pale. Hebu twende leo Bora tuangalie kama tutakuta kuna viatu vinatengenezwa. Twende Morogoro tuangalie, ni nini kinafanyika katika viwanda vile? Lakini ukiangalia *writeup* ilipochukuliwa, walisema wataendeleza kitu kinachoendelea pale. Kwa hiyo, naomba viwanda vyote vikaguliwe. Kila mtu ambaye alichukuwa Kiwanda na akasema atazalisha kitu fulani twende kufanya ukaguzi: Je, ndicho kitu kinachoendelea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi itachezewa mpaka lini? Watu wengine wameita shamba la bibi. Ukitaka mahali pa dezo pa kuwekeza, nenda Tanzania. Mimi nadhani umefika wakati wa kusimamia sheria na watu wawe waoga. Unaingiza tani na tani za sukari, wewe huna mtu uliyemwajiri wa sukari, huna mkopo wowote unaohusu sukari, lakini hakuna mtu anayekugusa kwa sababu una nguvu ya fedha. Kwa hiyo, nguvu ya fedha tunaomba isitumike, bali nguvu ya haki ndiyo itumike na watu wote watendewe haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu kila siku hapa alikuwa anaongelea sera ya kulinda viwanda vyetu vya ndani. Imekuwaje leo viwanda vyetu vya ndani hatuvillindi wakati tunategemea viajiri vijana wengi wanaozurura Mitaani? Mfano wakiondoa vijana 3,000, Mtibwa vijana 4,000 ni nini kinatokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno langu la mwisho, watu wameongelea habari za Benki, benki nyingi zinatoa misaada Mjini. Hivi watu wengine ambao wako kule vijijini, tuna mpango gani wa kuona wapi hii keki tunagawana wote kwa usawa? Ukienda kutafuta watu wa Misenyi waliopata mkopo, utashangaa. Vijana wanataka kulima, hawawezi kupata mkopo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Nakushuru Mheshimiwa Assumpter kwa mchango wako mzuri.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Pindi Chana.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kupongeza taarifa za Kamati za Wenyevidi wawili waliosoma, Wanyalukolo wenzangu kutoka Mkoa wa Iringa wamesoma vizuri sana taarifa za Kamati zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuzungumzia suala zima la viwanda. Ni kweli kabisa katika nchi yetu tunahitaji viwanda na ni lazima tujiulize kila mwaka baada ya kupitisha bajeti kwamba tumetoka viwanda vingapi kwenda viwanda vingapi? Kwa hiyo, tuwe na *graph* na *statistics*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa napata bahati sana ya kutumwa na Chama na Serikali kwenda nchi mbalimbali. Kwa hiyo, ni miongoni mwa watu wanaosafiri sana kutokana na kutumwa tumwa.

Sasa nchi nyingine wenzetu sasa hivi wanatengeneza magari, wanatengeneza vifaa vya kwenda kwenye Mars na Jupiter kutoka kwenye *Earth* lakini sisi bado tuko hatua za mwanzo. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara, lakini nadhani wakati wenzetu wanatembea sisi tunapaswa kukimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malighafi tunazo za kutosha kwa mfano chuma kule Ludewa Mchuchuma na Liganga, lakini viwanda bado vinaanzishwa kwa kusuasua. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo ningepomba sana tukazane. Kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA]

Kampuni ya Kichina iko pale inaanza kutoa uzalishaji lakini bado hatua zinakwenda polepole sana kule Mchuchuma na Liganga. Lakini sambamba na hayo, wakati mwingine tunachukua ardhi kwa ajili ya uwekezaji kwa wananchi. Ardhi hii tunapoichukua tunachelewa sana kuwafidia wananchi wetu.

Kwa hiyo, lazima ifike wakati tunapojenga viwanda kwa kutumia *Public Private Partnership* wakishirikiana na sekta binafsi, tujitahidi sana kuwafidia wananchi kwa viwango vinavyotakiwa. Maeneo mengine wanafidiwa kama ndiyo watu walikuwa wanaishi, wanajengewa nyumba na kadhalika. Hivi ni vitu vya msingi sana. Kwa hiyo, ningeomba sana suala la fidia pale tunapochukua ardhi za wananchi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanja mbalimbali na viwanda kwa kweli liangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa mbalimbali katika nchi yetu ni Mikoa ya Kilimo Kwanza, kwa mfano Mkoa wa Iringa na Njombe ni maeneo ambayo tunazalisha sana kilimo. Kule tunazalisha viazi, mahindi na mbogamboga. Lakini pamoja na kuzalisha, bila viwanda kama taarifa ya Mwenyekiti ilivyosema, kwa kweli bado tutakuwa tunasusua.

Lazima tuwe na viwanda vya kutengeneza malighafi hizi kuwa bidhaa zinazoeleweka, kwa mfano taarifa ya Mwenyekiti wa Ukimwi, amesema hata dawa mbalimbali lazima ziwe zinapatikana Tanzania, kwa mfano, madawa ya ARV. Sasa madawa haya yanahitaji viwanda, vitu kama mbolea. Leo hii Tanzania tunatumia sana mbolea katika Kilimo Kwanza. Lakini viwanda hivi vya mbolea hakika bado viko vichache sana, havikidhi haja, tunaagiza mbolea toka nje. Ni pesa nyingi sana ambazo tumekuwa tukizitumia.

Sambamba na hilo, ni vitendea kazi kwa mfano majembe. Tunawashukuru sana *SIDO* wanatengeneza majembe ya kukokotoa, majembe ya kutumia wanyama, majembe ya aina mbalimbali lakini bado hata jembe la mkono lenyewe bado wakati mwingine tunaagiza nje. Ni kweli kuna matrekta na kadhalika, lakini matrekta yale wakati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA]

mwingine huwezi kutumia kupalilia. Sisi wakulima wa mahindi, wakati wa palizi kuna palizi mbili na pale unahitaji jembe la mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kupitia Ofisi yangu nimekuwa nikijitahidi sana kutoa ruzuku kwa wananchi vitu kama majembe ya mkono. Wakati Serikali inatoa mbolea, mimi Ofisi yangu huwa natoa majembe ya mkono kwa ajili ya wananchi. Nimekuwa nahangaika sana kupata makontena ya majembe ya mkono. Mara nyingi sana nakuta majembe haya ya mkono yameandikwa *made in China*, yanatoka nje. Kwa nini Tanzania tusiweze kutengeneza vitendea kazi hivi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima ifike wakati tujitahidi sana masuala ya vitendea kazi, hususan vitendea kazi vya kilimo. Kwa hiyo, ningepomba sana, kwa kuwa nchi yetu ni Kilimo Kwanza, huu sio wakati wa kuagiza vitendea kazi kama majembe, mbolea vinatoka nchi za nje. Ni wakati wa kuwa na uwekezaji wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili suala la kuwa na viwanda vyetu, sasa hivi inafika wakati unamwangukia Mtanzania unakuta mavazi yake kwa mfano asilimia 50 ya mavazi aliyovaa ni *made in* nchi fulani. Unakuta nguo aliyovaa haijatengenezwa Tanzania, saa haijatengenezwa Tanzania, kiatu hakijatengeneza Tanzania, simu anayotumia haijatengenezwa Tanzania, mawani hayajatengenezwa Tanzania. Hivi sasa Tanzania tuna viwanda gani? Kwa hiyo, wakati ufike sasa tuwe na viwanda vya kutosha kutengeneza hata vitu vidogo vidogo. Naomba sana tutoe ridhaa kwa wawekezaji wenye nia njema, mikopo ipatikane vizuri, viwanda viwepo.

Wenzangu wamezungumzia mabenki, nami naomba niseme. Mabenki kwa kweli riba zimekuwa ni kubwa. Ukienda kuweka *fixed deposit* kwenye benki, asilimia unayopata *interest* wewe unayeweka *fixed deposit* unakuta ni ndogo kuliko asilimia ambayo benki inachukua inapotoa mkopo kwa mwananchi. Unakuta akina mama wakienda kukopa, riba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA]

ni asilimia 16. Zikienda Taasisi kubwa kubwa, ni asilimia 16 hiyo hiyo. Jambo hili nimekuwa nikilizungumza sana, masuala ya viwanda na biashara. Biashara sasa hivi lazima mtu awe na uwezo wa kukopa, lakini mabenki gharama zake ni kubwa sana za riba. Hili ni jambo ambalo naomba liangaliwe vizuri.

Sambamba na hilo, ningepomba sana suala la viwanda na biashara mabenki yaweze kukopesha vijana. Kuna nchi kama Zimbabwe, wao waliweka sera kwamba mabenki sasa yakopeshe vijana, kwa maana ajira zimekuwa ni changamoto. Wanaweka utaratibu vijana wanakopa, wanapata bodaboda, wanawekeza kwenye shughuli mbalimbali, wanauza vocha, maisha yanakwenda, tunapunguza ukali wa maisha.

Kwa hiyo, ningepomba sana mabenki yaangalie ni namna gani tunaweza kuwasaidia wananchi, tuisubiri tu mabilioni ya JK ambayo yametusaidia sana kupitia *NMB*. Tuombe sasa mabenki pia yaweze kukopesha vijana maana vijana pia ni zaidi ya asilimia 50 ya idadi ya watu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuna kiwanda pale Iringa kinaitwa *National Milling Corporation*. Hiki kiwanda ni muhimu sana kwa watu wa Iringa Wananjombe. Kwa hiyo, ningepomba hili liangaliwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE: PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Pindi Chana. Sasa naomba namwita Mheshimiwa Pauline.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache. Awali ya yote nawapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini naamini kwamba Serikali itachukua mapendekezo yote na kuyafanya kazi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PAULINE P. GEKUL]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja tu la muhimu sana la kuchangia nalo ni *Electronic Fiscal Device (EFD)*. Hivi karibu wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali kote nchini wametoa malalamiko yao kwa Serikali jinsi hizi mashine zinapatika kwao na kwa bei gani.

Naipongeza sana Kamati ya Biashara kwa kutoa mapendekezo matatu na mimi niyarudie kwamba iundwe Tume huru kuchunguza uhalali wa mashine hizo na mchakato mzima wa ununuzi. Naomba hili Serikali mtakapokuja kujibu msememe mmeridhia hili kwa sababu limegusa wafanyabiashara wote kote nchini.

Pendekezo la pili, wamesema Serikali iondoe kodi kwenye vifaa hivyo. Hizo mashine ambazo wafanyabiashara wamepatiwa, Serikali iondoe kodi. Lakini la tatu, Tume ipendekeze bei mpya kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana kwa asilimia 100 na mapendekezo ya Kamati kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, hizi mashine zinaambatana na matatizo yafuatayo:-

Kwanza bei ni kubwa, wafanyabiashara wameshalisemea. Lakini la pili, *roller* ile ambayo inatumika kutoa risiti moja inauzwa Sh. 10,000/= na inatoa risiti 20 ambazo ni chache sana. Hii inaongeza wigo mkubwa wa mfanyabiashara kuweza kulipa fedha nyingi sana. Ni tatizo kwao, wanalalamika wafanyabiashara wa kwangu wa Mkoa wa Manyara na wale wa pale Babati. Hata sasa wanasema kwamba kwa nini Serikali haijibu hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ukichukua hii mashine huwezi ukamuuzia mtu mwingine inakuwa ya kwako. Mimi leo nina duka la nguo au mama lishe au biashara yoyote, nikishakuwa na ile mashine siruhusiwi kumpa mtu mwingine baada ya biashara yangu kufunga. Wafanyabiashara wanataka kufahamu, kwa nini wanazuiwa, kama siendelei na biashara kwa nini nisimpatie mtu mwingine

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PAULINE P. GEKUL]

hii mashine wakati mimi nimenunua kwa fedha zangu zaidi ya Sh. 800,000/= ? Lakini Sh. 135,000/= kwa ajili ya ukaguzi kwa kila mwaka inachajiwa na *TRA*. Wafanyabiashara wanauliza maswali kwa Serikali, mmeshatuuzia kwa bei kubwa, tunalipa tena, tunanunua *roller*. Lakini pia ukiangalia kila mwaka Sh. 135,000/=, kama hilo halitoshi, wafanyabiashara wanachajiwa zaidi ya Sh. 50,000/= kwa kila matengenezo inapoharibika ile mashine. Hebu angalieni, ni kwa jinsi gani mmemdidimiza huyu mfanyabiashara? Ni kilio cha wafanyabiashara wote kote nchini.

Niwapongeze Wafanyabiashara wa Dar es Salaam na wa Mikoa mingine waliogoma, na wa kwangu wa Mkoa wa Manyara *TRA* leo wanawaambia tarehe 1 tutapambana, lazima mtumie hizi mashine.

Hebu nikuombe Mheshimiwa Waziri, kabla hawa wafanyabiashara hawajaanzisha mgogoro na *TRA*, hebu toeni tamko rasmi kwamba tunaangalia kwa upya na Tume inaundwa na hili zoezi la hizi mashine msimamishe kwa nchi nzima. Kwanini msimamishe Dar es Salaam? Kwanini Wafanyabiashara wangu wa Babati wasisimamishiwe na Mkoa wa Manyara wote? Kwa nini wao waendeleo kutumia hizi mashine?

Kwa hiyo, naiomba Serikali, hili jambo ni la msingi sana na hao wafanyabiashara ndio wanaiwezesha Serikali yetu, ndio wanaolipa kodi kwa asilimia zote. Kwa nini mwalimbikizie malipo yote hayo?

Kingine, pia hata *TRA* haijatoa elimu ile kwa ufanisi zaidi wa kutumia ile mashine. Kwa hiyo, inatoa nafasi ya zile mashine kuharibika, halafu mfanyabiashara analipa zaidi ya Sh. 50,000/=, *TRA* wanachukua 135,000/= kwa ajili ya ukaguzi. Ni mzigo mkubwa sana kwa wafanyabiashara nchi hii. Naomba Serikali kama ni sikivu, jioni mtuambie mmesitisha zoezi hili, sio kwa Mkoa wa Dar es Salaam tu, hata kwa Mkoa wangu wa Manyara na kwa wafanyabiashara wa Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wote wamemalizika. Jioni tutakuwa na wachangiaji sita, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ajiandae kama hayuko humu ndani, basi apewe taarifa kwamba yeye ndiye atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza. Wakimaliza hao, Serikali itakuja kujibu; Mawaziri watano, ambao ni Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Mheshimiwa Saada Mkuya, Mheshimiwa Dkt. Kigoda, Mheshimiwa Dkt. Nagu na Mheshimiwa Lukuvi. Watapata kila mmoja dakika kumi kumi.

Baada ya maneno hayo, nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.54 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lillirudia)

Hapa Naibu Spika, (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa Kigwangalla. Mheshimiwa Kigwangala tafadhali.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niwe mchangiaji kwenye hoja hizi za Kamati mbili zilizofikishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Wenyeviti wenzangu wa Kamati hizi za Ukimwi, Madawa ya Kulevya pamoja na ile Uchumi, Viwanda na Biashara, pamoja na Wajumbe wao kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kipindi chote cha mwaka mmoja uliopita. Lakini zaidi kwa kuandaa Kamati hizi na kwa kuzisoma kwa umakini na umahiri wa hali ya juu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda zaidi nijikite kwenye ile hoja ya Uchumi, Viwanda na Biashara. Kwanza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

ni-*declare interest* kwamba binafsi ni Daktari, lakini ni Daktari ambaye pia nimepitia katika maisha ya ujasiriamali, maisha ya kufanya biashara. Hivi ninavyoongea hapa, namiliki hisa kwenye Kampuni za *MSK Group of Companies*, japokuwa siendeshi shughuli za kampuni hizo kila siku.

Uzoefu wangu katika kufanya biashara hapa Tanzania, nimejifunza mambo mengi sana. Mojawapo kubwa ambalo nimeliona, ni namna ambavyo Serikali inajitahidi siku hadi siku kutengeneza mazingira rafiki zaidi kwa uwekezaji hapa nchini kwetu. Lakini jitihada hizo kwa bahati mbaya sana zimekuwa zikikwamishwa na baadhi ya watendaji ambao aidha wanafanya makusudi kutokurahisisha mchakato wa uwekezaji kufanyika ama kwa nia ya kutaka kupata chochote, ama pengine labda kwa kutokuwa na uelewa mzuri tu wa namna na umuhimu wa kuwasaidia wawekezaji kwenye Taifa letu. (*Makofi*)

Mfano mzuri, ni ugumu ambao unatengenezwa bila sababu za msingi na baadhi ya mamlaka. Kwa mfano, mwingiliano uliopo kati ya Taasisi ya *TIC* na *TRA*; ukisoma sheria na ukipewa maelekezo kwenye Tasisi ya *TIC* kwamba ni namna gani mwekezaji anatakiwa awe *handled*, na kwamba mwekezaji ana *benefits* zipi; halafu mwekezaji akaingia nchini, akapewa *certificate of tax incentives*, akaondoka nayo, akaenda nayo *TRA* na orodha ya vitu ambavyo amesamehewa kisheria kuvilipia kodi, lakini akifika kule *TRA* anakutana na mikingamo na vizingiti. Wanaanza kukata hii, ondoa hii, kata hii, ondoa hii; na mwisho wa siku kunakuwa hakukuwa hata na maana ya mwekezaji huyo kwenda kuomba *tax incentives* kwenye mamlaka zinazohusika.

Kwa hiyo, ningependa kupendekeza hapa kwamba Watendaji wetu nao waendane na nia na kasi ambayo imewekwa na Serikali ya Awamu ya Nne katika harakati za kuhamasisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali.

La pili, ni kwenye eneo la ardhi. Tunasema tuna mamlaka kwa mfano *EPZA*, *TIC*, kuna Mamlaka ya *RUBADA*, wote hawa wanatoa ardhi kwa wawekezaji wanapokuja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

nchini kwetu. Lakini kwa namna ya ajabu sana, nimeshuhudia mtu anaomba ardhi ili awekeze kwa faida ya kuzalisha ajira, lakini pia kwa faida ya kufanya *manufacturing* ndani ya nchi yetu ili tuweze kupunguza bidhaa ambazo tunaingiza kwa kutumia *forex* zetu kutoka nje ya nchi hususan katika nchi za Mashariki ya mbali kama China na kwingine.

Unakuta mtu anacheleweshwa kupata ardhi kwa zaidi hata ya miaka mitatu ama mine, na ardhi yenyewe hii wala hapewi iwe ya kwake milele, anaazimwa tu kuitumia kufanya shughuli ambayo anataka kuifanya kwa mujibu wa sheria yetu ya Ardhi Na. 4 na ile Na. 5. Lakini cha kushangaza, unakuta anacheleweshwa, anazungushwa; huku, kaenda, karudi. Mwisho wa siku mtu anakata tamaa, anakimbilia Kenya ambao wana ardhi ndogo sana. Anapewa ardhi anawekeza, halafu Wakenya wanakuja kuwa baadaye wao ndio wanaongoza kwa kuleta bidhaa ambazo zinatumika katika Taifa letu, kuliko Taifa lolote lile hapa duniani.

Ni jambo la ajabu na ni jambo la aibu kwamba pengine wawekezaji hawa wanaokimbia hapa kwenda Kenya, wangeweza kuwekeza hapa Tanzania, tungezalisha ajira lakini pia tungeweza kupunguza kiasi cha *forex* ambacho tunakitumia kwa ajili ya kununua bidhaa kutoka nje ya nchi. Matokeo yake tunge-*strengthen currency* yetu, lakini pia tungeweza ku-*stabilize* vizuri ile *balance of payment account* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme napenda sana Wabunge wenzangu kuchangia na kusaidia kutupa ushauri sisi Wabunge wa Nzega hususan Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC – Mheshimiwa Mbarouk, alitupa ushauri. Lakini ningependa tu kumjulisha kwamba ile kauli aliyoitoa haikutufurahisha sana sisi Wabunge wa Nzega kwamba eti tumeshindwa kutumia fedha tulizozipata kutokana na ushuru wa huduma, kwamba Kamati yake walifika pale Nzega na wakaona huo upungufu.

Ushauri ule aliutoa pengine bila kujua tu, na nimtaarifu kwamba watu wa Nzega tulishaazimia kuzitumia pesa zile za

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

ushuru wa huduma takriban bilioni 2.3; na kwamba tuna mikakati ya kufanya. Kwa kuwa yale ni mambo ya Nzega, alitakiwa ayaache tu ya Nzega. Asishangae kwa nini zipo kwenye akaunti. Angekuta zimeliwa, tungemwelewa. Lakini kwa kuwa amezikuta ziko kwenye akaunti, na Wabunge wa Nzega – mimi na mwenzangu Mheshimiwa Selemani Zedi, tuko imara na tuko makini, na tunahudhuria vikao. Sijui kama yeye huwa anahudhuria kule kwake, lakini sisi tunajitahidi kweli kuhudhuria vikao vya Halmashauri na tunashiriki kikamilifu kwenye maamuzi yote yanayofanywa na Baraza letu la Madiwani. *(Makofi)*

Sasa tumwombe atuachie ya Nzega wenyewe. Labda tu kwa kumpa taarifa, nimwambie kwamba fedha zile watu wa Nzega wameazimia kwenye Kikao halali cha Baraza la Madiwani kuanzisha Benki ya Watu wa Nzega *(Nzega Commuty Bank)*. Kuanzisha kampuni ambayo tutainunulia mitambo ya kuchimba visima, lakini pia mitambo ya kuchonga barabara ili kuibadilisha Nzega. Nawahakikishia tukikamilisha mikakati pale Nzega, mimi na mwenzangu Mheshimiwa Selemani Zedi tutaendelea kuwa Wabunge milele. Kwa sababu hizi ndiyo kero ambazo zinawaudhi wananchi wetu, na tunazifahamu na tumeanza kuzichukulia hatua. *(Makofi)*

Pia nilishangaa kwa nini hawakujjuliza, tuliwezaje kuzitafuta Shilingi bilioni 2.3 ambazo zilidhulumiwa na wawekezaji hawa kwa zaidi ya miaka 15, na Wabunge wengine walikuwepo? Lakini sisi tumehakikisha katika hii miaka mitatu ya mwanzo tumezipata fedha zile. Sijui kwa nini huyu mtu hakujaribu kujihoji hata kidogo tu, akaweza kufahamu kwamba sisi tuko makini, tuko mahiri na hatushindwi kuzitumia fedha ambazo tumezitatfuta wenyewe. Kwa hiyo, nilipenda kumpa hiyo taarifa huko aliko zimfikie na aendeleo kutuachia Wananzega mambo yetu ya Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme lingine tu kwamba watu wa Nzega tunapenda kuwezesha ili tuweze kutunisha mfuko wetu. Ndiyo maana tumeanza sisi wenyewe mchakato wa kuanzisha Benki ya Jamii ili tuweze kuzikopesha SACCOS

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

zote katika Wilaya ya Nzega hatimaye SACCOSziwakopeshe wananchi kwa wingi. Sasa kwa kuwa sisi wenyewe tumekwishaanzisha harakati hizi za kujenga uwezo wa kiuchumi kwa wananchi wa Nzega, tunaomba Serikali ituunge mkono kupitia ule mfuko wa uwezeshaji ulioko chini ya mama yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, lakini pia kupitia Mfuko wa Vijana na ule Mfuko wa Akina Mama na mwisho wa siku msisahau lile Azimio la kuanzisha ile Benki ambalo lilipitishwa na Bunge hili mwezi wa Aprili kupitia hoja ambayo mimi niliwasilisha hapa Bungeni, ya kukuza ajira kwa Vijana na Kuondoa Umaskini. *(Makofi)*

Basi zile pesa zitakapotengwa na Serikali, msisahau Nzega, kwa sababu Nzega tuko makini na tumejipanga. Ndiyo maana tumeanza sisi wenyewe kuwekeza kwa kuanzisha Benki yetu. Hivyo, natarajia Serikali itaona jitihada zetu na itajipanga kututengea fungu kutuwezeshwa. Maana yake, mbebe ambaye yeye mwenyewe anaweza kukushikilia. Bibi yangu alikuwa anapenda kusema, “ukishikwa shikamana.” Sasa sisi tayari tumeshaanza kushikamana vizuri.

NAIBU SPIKA: Nakuona Mheshimiwa umesimama. Mheshimiewa Kigwangalla, dakika moja.

TAARIFA

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kutumia Kanuni Na. 68 (8), naomba kumpa taarifa msemaji wa sasa hivi kwamba Kamati ya LAAC ni Kamati ambayo imeundwa kwa sheria zote za Bunge, na imepewa majukumu na mamlaka ya kuweza kufanya kazi. Haikubaguliwa kwamba eneo fulani ifanye kazi, eneo lingine lisifanye kazi. Kathibitisha kwamba kweli fedha zipo. Sasa lugha ya kusema kwamba tuwaachie wenyewe watu wa Nzega, hii itakuwa hatukuyatendea haki yale majukumu ambayo wewe Spika umetupa kwa ajili ya kuyatekeleza. Naomba kauli ile ambayo amesema kwamba mambo ya Nzega waachiwe wenyewe wa Nzega, kwa kweli aifute. Kwa sababu taarifa ile ilikuwa ni taarifa ya Kamati ya Bunge. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigwangalla, taarifa hiyo umepewa.

MHE. HAMIS ANDREA KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, hii taarifa ya Mheshimiwa Mbarouk imetolewa, lakini sikubali. Naendelea kusema tu kwamba Mheshimiwa Mbarouk angeuachia wenyewe tu. Kwa sababu kwanza nimeshangaa, yeye kama Mwenyekiti wa LAAC angetakiwa ajue utaratibu wa kufanya kazi wa Halmashauri. *(Makofi)*

Fedha za *own source* kwa utaratibu wa Halmashauri zinaamuliwa kwamba zitumike vipi na watu wenyewe wenye fedha zile. Kwa hiyo, zile fedha za huduma ni *own source* ya Halmashauri ya Nzega. Nasi kwenye Halmashauri ya Nzega, tumeshazifanyia maamuzi ambayo niliyasema hapa.

Sasa uamuzi wetu upo, na upo *documented* kwenye Maazimio ya Baraza. Lakini pia wakati yeye anapita kule Nzega, tayari tulikuwa tumeshapeleka maombi kule TAMISEMI ya kuruhusiwa tuzitumie kama *Supplementary Budget*. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti wa LAAC anapokuwa hajui hata utaratibu wa *Supplementary Budget* wa Halmashauri, inanishangaza sana. Ningetarajia Mwenyekiti huyu awe analijua hili. Asizungumze tu mambo humu ndani ya Bunge kwa faida ya kufurahisha hadhira, wakati hayajui yalivyo na hajui misingi ya anachokisema. Kwa sababu utaratibu wa kuendesha Halmashauri unajulikana. Sisi fedha zile tumeziomba kwa kutumia *Supplementary Budget*, hatuwezi hatuwezi kuzitumia nje ya bajeti.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ni kengele ya pili hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Aaah! *(Kicheko)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU SPIKA: Niseme ni bahati mbaya sana kwamba hawa wanaolumbana, wote wawili ni Wenyeviti wa Kamati za Bunge humu ndani, ambao ni washauri wa Kiti hiki kwa karibu sana kwa kiwango kikubwa. Ningependa mambo haya wakalumbanie kwenye Kamati yao ya Uongozi, waone ni namna gani ya kufanya. Ila tu kwa maana ya Kiti ni kwamba Kamati zina ruhusa ya kufanya mambo ambayo yako ndani ya *portfolio* yao kwa uhuru kabisa bila kuzuiwa na kipingamizi chochote kile. *(Makofi)*

(Hapa Mheshimiwa Wenje alisimama)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wenje!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sana. Kanuni zetu za Bunge zinasema kwamba mjadala ambao ulikwishafungwa hauwezi ukaanza tena humu ndani ya Bunge. Nawe ndio unasababisha vurugu humu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku, *trend* yako siyo nzuri. Wewe ndio unavuruga Bunge kwa kuruhusu mjadala ambao uliokwishafungwa huko nyuma, uanze tena upya na unajua Kanuni za Bunge zinakataza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushauri, haya mambo ya kuzua mijadala ambayo ilikwishafungwa, usiruhusu Wabunge wanafanya na wewe uko kwenye Kiti. Ndiyo inayoanzisha vurugu ndani ya hili Bunge.

NAIBU SPIKA: Nimekuacha uzungumze hadi mwisho. Ni utaratibu wa utovu wa nidhamu mkubwa sana kumshambulia kiongozi wako kirejareja tu. Sasa haya mambo mnayofanya kule *CHADEMA*, mnamshambulia kiongozi wenu Naibu Katibu Mkuu, mnataka kuleta na Bungeni tena. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Cecilia Pareso, endelea.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika mjadala huu wa Taarifa za Kamati. Nami niwapongeze Wenyeviti wa Kamati kwa kuwasilisha taarifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutoa mchango wangu katika suala la Sekta za Benki nchini na Taasisi zinazotoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki zimekuwa zikianzishwa nyingi sana, ni jambo jema. Lakini Benki hizo zinapofika suala la kutoa mikopo, kwa kweli mikopo ile inatolewa kwa riba kubwa sana, kiasi kwamba wananchi wengi ambao wanatamani wapate mikopo, wanashindwa kwa sababu riba zinakuwa kubwa sana.

Taarifa ya Kamati imeonesha hapa kwamba Benki hizo sasa zinafikia karibia asilimia 25 na nyingine ziko hadi asilimia 25 ya mikopo inayotolewa. Kiwango hiki ni kikubwa sana, hivyo hatutaweza kuwasaidia wananchi ili waweze kujikwamua kiuchumi. Lakini kuna hizi Taasisi nyingine, mfano *Bayport*. *Bayport* imekuwa ikilalamikiwa sana. Wananchi wa Jimbo la Karatu, baadhi wanalalamikia Benki hii kutoza riba kubwa sana. Kuna mmoja ambaye amechukua mkopo wa Sh. 2,200,000/= lakini mpaka anarejesha anatakiwa arejeshe Shilingi milioni nane. Ni karibia asilimia 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo haki! Tunataka kujua usimamizi wa hizi Taasisi unakuwaje? Maana huko ni kumnyonya kabisa mwananchi anayekwenda kuchukua mkopo. Mtu anakwenda kuchukua mkopo, ana malengo yake au shida imemsukuma afanye hivyo. Lakini mwisho wa siku wakati anaporejesha huo mkopo, riba inakuwa kubwa sana, yaani kupitiliza. Kwa hiyo, ni vyema Serikali ikasimamia hizi Taasisi. Sheria ipo, miongozo inatolewa, lakini unaweza ukawa na sheria, ukawa na miongozo halafu hakuna kinachofanyika. Kwa hiyo, ni vizuri kufuatilia kwa karibu kuona kwamba jambo hili la riba linaweza kupunguzwa, na wananchi wapata kile ambacho wanastahili. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwenye suala la takwiku za *transaction* zinazofanywa na Makampuni ya Simu. Siku hizi utumaji na upokeaji wa hela pia umehamia kwa kiwango kikubwa sana katika Makampuni ya Simu kupitia simu za mikononi. Lakini hatujawahi kupata takwimu sahihi ni kiasi gani mfano kwa mwaka zinatumika kusafirisha hela kupitia simu. Tunaona ni vyema Serikali ilete takwimu sahihi, ni kiasi gani *transaction* ya simu inafanywa na tujue takwimu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni matumizi ya Dola za Kimarekani. Mheshimiwa Mpina asubuhi alizungumzia vizuri sana kuhusu udhibiti wa *Bureau De Change*. Maduka ya kubadilishia fedha yamekuwa mengi sana nchini. Licha ya kuwa tu mengi, hata vibanda vya simu unaweza ukakuta Dola nazo siku hizi unaweza ukabadilisha, unaweza ukapata Dola. Hakuna udhibiti wa biashara hii. Sijui wakati wa utoaji wa leseni wanaangalia nini! Yaani hakuna udhibiti katika utoaji wa leseni na hakuna udhibiti katika biashara hiyo. Lakini Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 inataka maduka hayo wasizidishie dole elfu kumi. Lakini je, ni kwa kiasi gani Serikali imesimamia sheria hii? Ni vyema Serikali iangalie suala la udhibiti wa maduka haya ya kubadilishia fedha, yaani *Bureau De Change*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia suala la matumizi ya Dola za Kimarekani. Kumekuwa na matumizi makubwa sana ya Dola za Kimarekani. Nilishawahi kuuliza swali hapa Bungeni. Lakini Serikali nyie mnasema tu kwamba sheria inatamka kwamba hela halali ni hela ya Kitanzania. Ndiyo, sheria inasema hivyo, lakini mmefuatilia kuona ni kwa kiasi gani kunakuwa na matumizi ya Dola za Kimarekani? Kiasi ni kikubwa sana. Lakini kunapokuwa na matumizi makubwa saa ya hii Dola, ina maana fedha zetu za Kitanzania zinakuwa hafifu. Kwa hiyo, ni vyema sana kuwepo na udhibiti wa kutosha katika suala la utumiaji wa Dola za Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu deni la Taifa. Kila mara tunaletewa taarifa kwamba deni la Taifa linaongezeka, lakini hatuambiwi kwanza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

mnakopa wapi? Kwa mikataba gani? Kwa kiasi gani? Lakini tunaletewa tu takwimu kwamba deni la Taifa limefikia trilioni 23, mara trilioni 25 lakini taarifa sahihi, kila siku mnatuletea takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Bunge lako sasa lipewe taarifa sahihi za kina tuachane na habari za takwimu kujua kwamba huwa mnakopa wapi? Kwa mikataba gani? Ni kiasi gani mnakopa? Kuliko tu kuona kila siku takwimu, deni la Taifa linaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu suala la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kamati wanaeleza na sisi kama Kambi Rasmi ya Upinzani, mimi kama Naibu Waziri Kivuli wa Kazi na Ajira, mara zote katika mwaka wa fedha tukisoma hotuba yetu tumeendelea kusesitiza suala la kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwa mmoja, kuliko kuwa na mifuko mingi ya Hifadhi ya Jamii.

Nafurahi leo naona Kamati nao wamesisitiza jambo hili kwamba ni vyema kwamba Mifuko hii ya hifadhi ya jamii iweze kuunganishwa ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni muhimu sana kuunganisha mifuko hii tupunguze gharama za uendeshaji wa mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika Kamati ya Ukimwi kwa masuala ya Ukimwi. Kwa utaratibu, kuna fedha za Ukimwi ambazo zinatakiwa ziende katika Halmashauri zetu, lakini fedha hizi zimekuwa hazifiki kwa wakati na wakati mwingine hazifiki kabisa. Hata zikifika, nyingine unaweza kukuta zimekaa kwenye Akaunti hazitumiki, Watendaji hawazitumii kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inatia huzuni sana kama unaona hata nyinyi Serikali ya CCM, hata hizi fedha za Ukimwi pia za watu walioathirika inakuwa ni taabu kuzipeleka kwa wakati?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sana fedha hizi ziende kwa wakati katika Halmashauri zetu, ziwafikie wale Waratibu na wale Waratibu waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hao Waratibu pia wana Kamati zile za Ukimwi katika ngazi ya Kata mpaka vijiji, lakini Kamati hizi zimekuwa hazifanyi kazi kabisa.

Kwa hiyo, ni vyema mtoe msisitizo kwa Halmashauri za Wilaya waweze kuzifufua hizi Kamati, waweze kuzisimamia ziweze kufanya kazi inayotakiwa katika kutekeleza majukumu yake ya masuala ya Ukimwi.

Vile vile kuna suala lingine la Halmashauri; Kamati pia wameelezea kuhusu Halmashauri nyingi kutokuwa na mipango ya masuala ya Ukimwi. Huko mwanzo ilikuwa inafanyika, lakini siku hizi hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vyema tu Serikali ikazisimamia Halmashauri hizi ili waweze kuwa na mipango mizuri ya masuala ya Ukimwi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana, ahsante sana. Mheshimiwa Maria Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Omar.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii adimu ambayo wala hata sikuitarajia, lakini Mungu ni mwema. Nasimama kuzungumza kuhusa taarifa za Kamati ambazo zimetolewa hivi asubuhi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda tu kupongeza Wenyeviti hawa wawili ambao wametoa taarifa zao za Kamati kwa umahiri mkubwa. Pamoja na kwamba muda ulikuwa hauwatoshi, lakini wamejitahidi sana, na ninawapongeza sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARIA I. HEWA]

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuanza nacho ni suala la mambo ya Ukimwi ambayo mimi ni Mjumbe katika Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na taarifa nzuri ambayo imesomwa na Mwenyekiti wangu kwa umahiri aliouonesha, napenda tu kuanza na sentensi inayosema: "Tanzania bila Ukimwi inawezekana." Nasema hivyo kwa makusudi mazima kwa sababu binadamu nadhani tunaishi tu kwa kupuza. Mheshimiwa Rais alipotamka neno hilo na ndiye kiongozi mkubwa wa nchi hii, alikuwa na maana yake nzuri kabisa. Katika kumfuatilia kwa hatua zake na kwa utekelezaji wake ambao anaagiza vyombo vyake vifanye kazi, napenda niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani wakati sisi wa umri wetu bado tunakwenda Kliniki kwa maana ya kuwa wajawazito, ukifika pale ilikuwa hakuna hata cha kuulizwa. Umekwenda Kliniki kwenye kitengo cha ujauzito ni unafika unapimwa, kadi inajieleza kwamba unapaswa kupima hiki, unapaswa kupima hiki, unapaswa kupima hiki.

Leo tunaingiza mambo ya hiari, kwa misingi ipi? Mama mjamzito kwa tukio la sasa hivi nikielekea kwenye Ukimwi, kwanini iwe hiari? Kwamba huyu mama mjamzito ana nia ya kumkomboa mtoto wake, imefika hatua sasa ambapo mama mjamzito huyu akipewa dawa ambazo ziko vizuri zimeandaliwa, kuna uwezekano wa kupata mtoto ambaye hana virusi. Leo inafika mahali unamwanguka tu mama huyu bila kumjali ipasavyo. Mpime mama huyu na mwelekeze mama huyu na inapaswa aelekezwe kwamba akiwahi kwenda Kliniki kuna uwezekano wa asilimia kubwa akampata mtoto ambaye hajaathirika na virusi vya Ukimwi.

Naomba niliseme hili katika vyombo hivi kwa maana ya kulitumia Bunge hili. Mahali waliko akina mama, unabeba mimba, hakikisha kitu cha kwanza unakwenda Kliniki ukajihakikishe afya yako ili uwe na uhakika wa kumpata mtoto aliye salama na janga hili. Naomba kabisa, mama zangu huko mnakonisia, mimi niko kwenye Kamati hii na hiki

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARIA I. HEWA]

ninachokisema kina uhakika ndani yake. Baada ya hivyo hata kama mama ni mwathirika, basi na yeye ataendelea kupewa dawa ambazo zitamlea kwa muda mrefu akiwa na mwanaye ambaye hana madhara hayo. Nilitaka nilizungumze hili, maana mimi nimo muda mrefu sana katika Kamati hii. Tanzania bila Ukimwi inawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, baada ya kupata uzao huo wa bila Ukimwi, kwa lugha nyingine mbele ya safari Tanzania hii inaweza ikawa na uzao wa bila Ukimwi; ni kule ambapo tunasema; kwa mfano Tumbaku: Watumiaji wa Tumbaku wanatangaziwa kabisa hadharani hata kwenye vyombo vya habari kwamba wewe vuta tu, lakini cha moto utakiona. Utapata haya, utapata haya, utapata haya. Yote yanatolewa wazi.

Sasa mimi ningelipenda nishauri ifuatavyo kwa upande wa Ukimwi; maana ya madhara ya kuanguka mbele ya safari ukinywa pombe ya kuzidi ndiyo ujue unaelekea huko, kwa kusahau hata kutumia zana za kinga.

Kwanini katika vinywaji vyetu tusiweke *labels*, yaani kuweka maandishi kwamba unawekewa bia yako mbele ya uso wako, si uwekewe hata kale kamchoro ka Ukimwi kale kekundu ili ujue kwamba mbele ya safari ukizidisha hata kinga utaisahau! Hata kama ni maji ya kunywa, mtoto akiiona alama hiyo nyekundu si atauliza, mama hiki ni nini? Ukimpa tu chupa ina alama yoyote ile, atakuuliza Mama hiki ni nini? Au Baba hiki ni nini kimechorwa? Unamweleza. Kwa hiyo, atakuwa akijua kwamba Ukimwi ni hatari. Ataishi na yeye akijua mbele ya safari kwamba kumbe ninavyokua mambo mengine katika dunia hii ni hatari ni pamoja na ka alama haka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa ombi langu na ushauri kwamba hivi vinywaji vyetu kwanini visiwekewe alama hizo ili tuwe tunaulizana hiki ni nini? Hata ukiandika tu neno Ukimwi ni hatari kwenye *label* ya bia, kwenye *label* ya mambo mbalimbali hata kwenye maji ya kunywa. Narudia, Ukimwi ni hatari! Inaweza ikasaidia mbele ya safari.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARIA I. HEWA]

Naishauri Serikali yangu ifanye hivyo, siyo kuishia kwenye ma-*Tshirt* tu au na kwenye nini, ni gharama yale! Weka kwenye maji, kwenye vinywaji mbalimbali au kwenye vyombo mbalimbali ambavyo mtu ataweza kuuliza, ajue, atahadhalishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la kutahiri. Watu wananeemeka kwa kuunda *NGO* kwenda kung'ang'ana na watu wanaotahiri. Hivi kuna ubaya gani kama tumepiga vita ukeketaji kwamba una madhara haya, haya na haya, na tunasema kwa mwanaume ambaye hakutahiri ni moja ya njia ya kueneza Ukimwi. Hivi kwanini watoto wadogo wanapotoka hospitali wasitahiriwe?

MBUNGE FULANI: He!

MHE. MARIA I. HEWA: Eti, yoh! Ng'waa, nini? (*Kicheko*)

Ni wazo langu kwa sababu kutahiri mnakuja kutahiriwa mkiwa wakubwa, wengine mnakimbia na vifo vinatokea huko kwa kutahiriwa kwa njia isiyo salama. Hivi kwanini mtoto mchanga asitoke mle tu tayari yuko *safe* amekuwa *circumcised* vizuri, kiusafi na nini? Au nini? Mnapatamo nini, mkitahiriwa wakubwa? (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Maumivu makali.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba basi katika haya niliyoyazungumza naomba elimu iendelee. Kwa wale ambao mna *NGO's* za namna hii mwendelee kutoa elimu ili mbele ya safari kweli tuwe na Tanzania bila Ukimwi. Tanzania bila Ukimwi, inawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishia hapo. Ahsante kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maria Hewa kwa mchango wako wenye uwazi na ukweli. Mheshimiwa Rashid Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. RASHID ALI OMAR: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie kuhusu taarifa hii iliyopo Mezani ya masuala ya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka niseme kwamba Ukimwi ni janga la Taifa. Ukimwi katika Taifa letu unaangamiza vijana ambao ni nguvukazi waliomo katika umri wa miaka 19 hadi kufika miaka 49. Vijana hawa ndio tegemeo kubwa la Taifa letu katika kuzalisha na katika kujenga Taifa hili katika misingi mbalimbali inayohitajika ya kiuchumi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukimwi unaambukizwa katika hatua mbalimbali. Ukimwi katika nchi yetu unaweza kuambukizwa katika hatua zifuatazo:-

Kutumia ngono zembe; pia madawa ya kulevya, jambo ambalo matumizi haya ya madawa ya kulevya, mtumiaji wa madawa ya kulevya hana njia yoyote atakayoweza kujikinga na Ukimwi mbele yake. Baada ya kutumia madawa ya kulevya anaamua kufanya masuala ya ngono bila kujifikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niende katika Ofisi ya Mkemia Mkuu. Ofisi ya Mkemia Mkuu ni sehemu ambayo inashughulikia masuala muhimu ya nchi yetu yanayohusiana na Mahakama. Mahakama zetu zinapata taarifa rasmi za uhakika na ushahidi kupitia Ofisi ya Mkemia Mkuu kuhusiana na madawa haya ya kulevya. Lakini kinachoshangaza Taasisi hii ya Mkemia Mkuu majengo yake ni chakavu, Taasisi hii inakabiliwa na changamoto nyingi kabisa wakati ni kiungo katika kutafuta ushahidi katika kesi zilizoko Mahakamani kuhusiana na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizokabili Ofisi hii ya Mkemia Mkuu, kwanza majengo ni chakavu na ni ya zamani kabisa wakati shughuli za Mahakama zote katika kupata ushahidi wa madawa ya kulevya zinapitia pale na majengo haya ni chakavu, hayamithiliki. Taratibu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RASHID ALI OMAR]

zinazochukuliwa sasa hivi ni kwamba majengo haya yanafanyiwa ukarabati, lakini ukarabati huu kwa ushauri wangu, Serikali isimamie kikamilifu na kuchukua hatua za dharura ili Taasisi hii iwe na zana za kisasa zinazohusiana katika kufanya utafiti au uchunguzi wa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Ofisi ya Mkemia Mkuu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Wataalam. Idadi yao ni ndogo sana na idadi ya wafanyakazi katika Taasisi hii bado ni ndogo haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya Ukimwi nataka niishauri Serikali kwamba katika Kamati ambazo zimeteuliwa katika Halmashauri zetu, Serikali izisimamie vizuri na iziwezeshe ili ziweze kupambana na kudhibiti maambukizi ya Ukimwi. Taarifa zinazotolewa kuhusu kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya Ukimwi, zisitusababishie kuona kama suala hili ni suala la kulifanyia mchezo. Ni suala ambalo linatuathiri vibaya sana. Vijana wetu ambao ni nguvukazi kila siku maambukizi yanazidi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka niishauri Serikali kwamba vile vituo vinavyohusika na kusaidia watu walioathirika na maambukizi ya Ukimwi ambavyo kwa nchi yetu sasa hivi ni vitatu tu, yaani Mwananyamala, Muhimbili na Temeke kwa Dar es Salaam; Serikali iongeze vituo hivi katika maeneo yote angalau kila Wilaya kiwepo kituo kimoja.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nijielekeze katika suala la...

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru.
(Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rashid Omar. Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwijage.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika taarifa hizi za Kamati ya Viwanda na Biashara pamoja na masuala ya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanzia na Viwanda na Biashara. Nichukue nafasi hii kusema kwamba biashara zinachangia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa. Ni muhimu Serikali iweze kutambua umuhimu wa biashara. Mara nyingi wafanyabiashara mbalimbali hasa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanafanya biashara katika sekta isiyokuwa rasmi, Serikali imewaacha kabisa, lakini wana mchango mkubwa sana katika pato la Taifa. Hao wafanyabiashara ambao wapo katika sekta isiyokuwa rasmi mara nyingi *TRA* wanawasumbua sana. *(Makofi)*

Nilishuhudia mwaka huu pale Katoro ilitokea wafanyabiashara hawa *TRA* wakifika pale kwa mfanyabiashara, anampa tu karatasi anamwambia, unatakiwa kulipa faini Sh. 3,000,000/= na ukiangalia biashara yenyewe haina uwezo wa Sh. 3,000,000/=. Kwa hiyo, *TRA* inatakiwa ihakikishie kwamba wafanyabiashara hawa tunawajenga, tunawaelekeza mambo ya kufanya. Hata kama ni suala la kulipa kodi, waelekezwe, wafundishwe; mimi nina uhakika tukiwaelekeza vizuri wafanyabiashara hawa wanaweza kufanya kazi zao vizuri na hata baadaye wataweza kuchangia katika pato Taifa na pato la familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiasharai hawa wanahitaji kupewa mikopo, wanahitaji kupewa mitaji. Sasa mara nyingi Benki zipo Mijini na maeneo ya Vijijini Benki hazipo. Sasa hawa wafanyabiashara walioko vijijini watapata wapi mitaji? Kwa sababu bila mitaji, bila kuwezesha katika mitaji, haiwezekani kuweza kufanikishwa katika biashara. Biashara bila mtaji haiwezekani kufanya vizuri. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuweza kuangalia wale wafanyabiashara walioko Vijijini namna ya kuwafikia kuweza kuwapatia mikopo. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi mikopo mingi inapatikana Mijini. Ukienda Mijini, Makao Makuu ya Mkoa unakuta Benki zipo nyingi sana, lakini vijijini huwezi kukuta Benki. Kwa hiyo, naomba Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuweza kuwakopesha hata wananchi walioko vijijini. Natangaza kwamba vijiji vingi wapo wafanyabiashara wazuri. Kuna SACCOS nyingi ambazo zinahitaji kuwezesha na kupewa mitaji ili waweze kufanya vizuri katika shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine katika wafanyabiashara hawa, ni vizuri tukawapa elimu. Mara nyingi elimu ya biashara haitolewi. Kwa hiyo, unakuta watu wengi hasa vijana ambao pengine wanaanzisha biashara zao inakuwa rahisi biashara hizi kuanza na kushindwa kuendelea kwa sababu hawana elimu ya biashara. Lakini Serikali hasa kile Kitengo cha Uwekezaji na Uwezeshaji nilikuwa naomba sasa Kitengo hicho kianzishe utaratibu wa kuweza kuwawezesha kuwapa elimu na kuwapa mitaji hasa vijana ambao kusema kweli vijana katika sehemu zote Tanzania nzima hata Jimboni kwangu kule Busanda kuna vijana wengi ambao wanahitaji kweli kuwezesha, wanahitaji kupewa elimu ili waweze kuanza biashara zao kwa uhakika na kuweza kumudu maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la Benki, mara nyingi kuna Benki ambazo zimeanzishwa, kwa mfano Benki za Biashara na Benki za Kilimo, lakini hakuna Benki yoyote ambao inashughulikia wachimbaji wa madini wadogo wadogo wazawa. Nichukue nafasi hii kuiomba sasa Serikali kwamba, ni wakati muafaka sasa kuangalia uwezekano wa kuanzisha Benki kwa ajili ya wachimbaji wa madini wadogo wadogo ambao ni wazawa. Kwa sababu wachimbaji wa madini wanahitaji mitaji mikubwa, haiwezekani kuweza kuinua kipato cha mchimbaji wa madini bila kumpa mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuiomba Serikali kwamba kweli kuna Benki ya Wakulima, kuna Benki ya Vijana itaanzishwa, kuna Benki ya Wanawake, lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA]

ningeomba Serikali ianzishe Benki kwa ajili ya Wachimbaji wa Madini wazawa ili kuwawezesha kwa sababu Sekta ya Madini ina mchango mkubwa sana katika Pato la Taifa letu. Sasa haiwezekani kuweza kuongeza mchango katika pato la Taifa endapo Sekta hii haitaweza kuangaliwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi Wizara ya Nishati na Madini imepeleka fedha *TIB* na kushauri kwamba wachimbaji wa madini waanze kukopa fedha *TIB*. Mimi nasema kwamba haiwezekani, kwa sababu wachimbaji wa madini wadogo wadogo ni watu wa chini ambao hawana dhamana. Sasa itawezekanaje kupata fedha hizi *TIB*? Najua Benki nyingi zina masharti magumu. Maana yake ni kwamba tunatoa nafasi kwa wale tu wenyeye uwezo kuweza kukopa fedha hizi. Lakini kusema kweli zile *SACCOS* za wachimbaji wa madini wadogo wadogo wazawa kweli hawana uwezo wa kuweza kukopa katika Benki hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie namna ya kuanzisha hii Benki ili kuweza kuwawezesha wachimbaji wa madini ili kuweza kuongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la viwanda. Nasikitika kusema kwamba viwanda kweli sijui kunakuwa na upendeleo katika baadhi ya maeneo. Kuna baadhi ya sehemu hatuna viwanda kabisa. Kwa mfano, katika Mkoa ya Kanda ya Ziwa viwanda ni vichache sana. Nikiangalia Mkoa wetu wa Geita, viwanda hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali sasa, kwa kuwa wawekezaji huwa wanakuja kuwekeza na wanapitia pale kwenye Kituo cha Uwekezaji, waangalie na maeneo ya pembezoni ambako hakuna viwanda. Kiwanda cha Saruji kijengwe Geita. Nilikuwa naomba Serikali iangalie uwezekano huo. Maana saruji ambayo tunaipata sasa inatoka Dar es Salaam, Dar es Salaam saruji inauzwa mfuko Sh. 15,000/=, lakini ikifika Geita saruji hiyo hiyo inauzwa mfuko moja Sh. 25,000/= mpaka Sh. 30,000/=. Sasa saruji hii inaongeza ugumu wa maisha, yaani maisha yanakuwa juu. Kwa hiyo, kipato

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA]

cha mwananchi wa kawaida anakuwa hana hata uwezo wa kujenga nyumba iliyo bora. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Sekta ya Uwekezaji wahakikishie viwanda vya saruji, Viwanda vya Samaki katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Kiwanda cha Nyama kwa sababu tuna wafugaji wa mifugo kama ng'ombe.

Kwa hiyo, naomba kweli Serikali iangalie namna ya kuwekeza katika viwanda; viwanda vya matunda. Kama ni matunda, tunayo; mananasi yapo ya kutosha. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Sekta ya Uwekezaji katika Wizara inayohusika, wawekezaji wa nje wanapokuja waangalie uwezekano wa Mikoja ambayo ipo pembezoni kuweza kuwekeza pia katika viwanda. Kupitia viwanda hivi tutakuwa na uwezo wa kuweza kujajiri pia hata vijana wengi ambao wanaomaliza Kidato cha Nne ambao pengine hawana fursa zaidi za kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba pia tuanzishe na VETA ili kuwawezesha...

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, dakika kumi ni chache sana. Mheshimiwa Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nichukue fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa uwasilishaji wao. Nami ninayo machache ya kuongea kuhusu Kamati hizi mbili.

Jambo la kwanza, kuhusu Kamati ya Ukimwi au suala la Ukimwi; Waheshimiwa Wabunge jambo ambalo Kamati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHARLES J. MWIJAGE]

haikulizungumza walishindwa kutukumbusha kwamba Ukimwi upo.

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu, Ukimwi upo na unaendelea kuua. Lakini jambo la hatari au lililonishtua kwenye Taarifa ya Kamati hii ni kwamba hata hii Huduma ya Kupambana na Ukimwi kuweza kuvidhoofisha hivi vidudu, sehemu kubwa ya madawa tunayotumia tunategemea kutoka nchi za nje. Sasa akili yangu nikawa na mashaka kwamba hawa wahisani wanaotuhisani ili kusudi kufubaza hivi vidudu, itakuwaje wakiamua kuacha? Takribani Watanzania kama milioni tano wanaumwa. Naungana na Kamati kwamba kuna haja ya kuanzisha Mfuko. Tuanzishe Mfuko ukae *standby* kusudi hao wahisani wakiwa na mambo mengine, tuweze kusimama sisi wenyewe. (*Makofi*)

Lakini jambo lingine ambalo nataka niishauri Serikali na uzoefu nimeupata kwenye Kamati ambayo imefanya kazi nzuri, sisi watu wa Visiwani kutokana na shughuli za uvuvi, wanakuja watu kwenye maeneo yetu wanaambukiza watu wetu Ukimwi. Kwa hiyo, Serikali mnalo jukumu, mnapofaidi minofu ya samaki na kupata fedha za kigeni...

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Taarifa, Mheshimiwa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Taarifa hiyo ipo upande gani? Haya itolewe. Aah, Mheshimiwa Kigwangalla.

TAARIFA

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayesema, anaongea mambo muhimu na anayaongea kwa umahiri wa hali ya juu. Lakini nilipenda tu kuweka sawa jambo moja kwamba kauli za kwamba "Ukimwi unaua," "Ukimwi upo," ni kauli ambazo zinaleta mtazamo wa unyanyapaa kwa watu ambao tayari wameshaambukizwa ugonjwa huu. Kwa hiyo, wataalam na Wanaharakati wa mambo haya huwa hawapendi zitumike

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tukizitumia zinakuwa na madhara kwa watu wanaohusika.

Hivyo, nilipenda aendelee na mchango wake, lakini aondoe yale maneno kwamba Ukimwi upo na Ukimwi unaua. Kwa sababu inaleta picha kwamba mtu akipata Ukimwi tu, tayari amepata leseni ya kifo na hiyo siyo sahihi. Kuna watu wanabisha humu, lakini naomba tu taarifa hiyo ipokelewe.

NAIBU SPIKA: Natumaini umeeleweka. Huo ni ushauri wa Daktari.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, anayezungumza ni Daktari kwa *Profession* na mimi nina *Profession* yangu nikishauriwa huwa sikatai, nakubali ushauri wako. Lakini mimi kwa ndugu zangu wanaonijua, Ukimwi unaua, Ukimwi unaua. Mtakayemfuata Daktari kwamba Ukimwi hauui, shauri yenu. Namna ya kupambana na Ukimwi ni kufuata maadili. Tujenge maadili ya watoto wetu, tujenge maadili ya ndugu zetu. Ambaye ndugu yake hajawahi kuuawa na Ukimwi, shauri yake. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nazungumza, sisi kwetu tuna ziwa kubwa lile la Afrika. Kuna shughuli za uvuvi. Wavuvi wanafuata samaki, samaki wanauzwa dunia kote. Kutokana na shughuli za uvuvi wananchi wetu wameambukizwa Ukimwi, wanaletewa magonjwa kutokana na watu wanaokuja. Ninachoomba kwa Serikali yangu, ni kwamba watusaidie sisi katika visiwa vyetu; mchangia mada alizungumzia visiwa vya Musoma, hapana. Muleba yote tuna Visiwa, mimi na mama yangu tuna visiwa 39, Muleba Kusini na Kaskazini, mtusaidie tukamilishe Zahanati zetu kwa sababu biashara ya samaki mnayoishabikia sisi kwetu imekuwa ni madhara. Samaki wanavuliwa, tunaachiwa Ukimwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Mwenyekiti wa Kamati unapokuwa unahitimisha hilo, naomba utufikirie. La muhimu katika upande wa Ukimwi tuache mambo ya utalaam, ni kwamba tunategemea watu wa nje katika kupata hizi dawa za kufubaza haya matatizo. Kweli ukipata zile dawa; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHARLES J. MWIJAGE]

nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu, amehangaika sana. Unaweza kujisikia unaumwa, lakini ukapata vile vidonge, unakaishi miaka 30 au hata miaka 40. Ndiyo hapa ninapokubaliana na Daktari wangu Mheshimiwa Dkt. Kigangwalla. Mimi na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla hatuwezi kutofautiana bwana. Zile pesa zenu za Nzega nilikuwa na Mheshimiwa Bwana Zedi tunazipigania, watu wengine wanaziingilia hawajui zilitoka wapi. Tulikuwa wote tunazipigania! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la biashara. Katika suala la biashara nizungumze watu wa *Weights and Measures*. Kamati yangu ya Biashara hamkuangalia watu wa Vipimo na Mizani. Watanzania tunakatwa kinamna. Kaangalieni saruji mnayonunua, imeandikwa *50 Kilograms*. Siyo *50 Kilograms!* Kimsingi kuna ukataji wa kinamna. Katika vitu unavyonunua *packaged*. Ningeomba watu wa *Weights and Measures*, msibaki kuangalie vile vipimo vya kwenye mafuta. Mwende mpaka kwa mlaji wa mwisho hasa kwenye sementi, kwenye unga, kwenye mchele, tunakatwa kinamna. Kuna tatizo, watu wanaumia. Sementi inayofikia kwa mteja haifiki ikiwa na kilo 50 acha yale matatizo ya *rebagging*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie watu wa *TBS*. Nasikitika watu wa *TBS* pamoja na upungufu wa kimfumo kwamba kuna bidhaa hazipitii bandarini, lakini soko la Tanzania na niwambie na nyinyi Wabunge mnaohusika, vilainisha mitambo mnavyotumia, *lubricant and greases* ni *absolute* zimepitwa na wakati, ni *sub-standard*. Hizi *duplicate* zipo madukani, zinaonekana. Unakuta *duplicate CB level, CC level, lubricants* za miaka 1970 ndiyo zipo madukani. Sasa hivi *lubricant* unayokwenda kununua kama gari lako la *petrol* inapaswa iandikwe *SJ*, lakini nyie mnanunua *lubricants* za miaka ya sabini na *TBS* wanaliona.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kumnong'oneza Mheshimiwa Dkt. Kigoda hili, lakini kwa sababu nimeliona, nimeona nikwambie hadharani. Kuna matatizo upande wa *TBS*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHARLES J. MWIJAGE]

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine, kama alivyozungumza Mwenyekiti wa Kamati, kuna tatizo la Bandari bubu. Bandari bubu za Mbegani; bandari bubu zinaingiza bidhaa nyingi ambazo zinapelekea watu wapate *sub-standard*. *Sub-standard* ya *duplicant* inaweza kuua injini, uka-*tolerate*, lakini kuna *sub-standard* hata ya madawa ya malaria ni *sub-standard*. Sasa hiyo sijui na yenyewe ni biashara gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzungumzie suala la biashara. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, Salam ya Krisimasi ambayo nataka kuwapa kwa sababu nadhani ni mara yangu ya mwisho kuhutubia leo, kuna suala la kiuchumi. Tunayo matarajio ya kuipeleka nchi hii katika uchumi wa kati. Kama walivyosema wataalam wa biashara katika Kamati yao, uchumi wa kati utaupata mkiwa na viwanda.

Kama Watanzania mnakubali hiyo, tujiandae tufanye mgomo. Watanzania wote wakiongozwa na Kamati ya Viwanda, tugome. Tugome kula mafuta yanayotoka nje ya nchi, tule mafuta ya Singida. Tukikubaliana wote hivyo, tutaleta mabadiliko ya viwanda na *TIB* mtuchukue mashine, msitafute dhamana. Tafute mashine China za kutengeneza alizeti, mwalettee watu wa Dodoma, Singida na Kongwa kusudi waweze kutengeneza mafuta. Yale mafuta *semi processed* mpeleke kwenye viwanda vingine vifanye *double refined*. Msipokubali kufanya mgomo, mkayakatalia mazao yanatoka nje, hamwezi kutoka hapo mkafika kwenye uchumi wa kati. Ndiyo walivyofanya India. Ndiyo maana ya *Campicola*, ndiyo maana ya Maruti Suzuki na ndiyo maana ya Nacet. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuja nikusimulie mapinduzi ya India yalivyoleta mabadiliko ya wembe. Wahindi walipokata kununua nyembe kutoka nje, India wanatumia nyembe kiasi kwamba huwezi kuelewa. India ikapata soko. Sasa bila Watanzania kuamua wenyewe kwa makusudi kwamba tuanzie kwenye mafuta yetu, hatatengeneza viwanda. Kiwanda kidogo tu cha kukamua mafuta; hivi viwanda vilivyopo Singida (Mheshimiwa Waziri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHARLES J. MWIJAGE]

wa Viwanda utanikosoa) siyo vizuri. Hizi mota za kokoto; mota ya kokoto kupasua alizeti unatumia umeme mwingi mno. Kwa hiyo, lazima twende China, *TIB*, mama mwekezaji uko hapa, kanunue mashine, Watanzania usiwape pesa, uwape mashine. Mtendaji wa Kata anasimamie ndiyo namna ya kutengeneza mapinduzi ya viwanda. Tutengeneze alizeti, tulime mpaka Mwanza, tulime mpaka Jimboni kwangu kule Muleba yote tulime na Tanzania nzima tuanzia hapo.

Tanzania inachukua tani 350,000 za mafuta ya kupikia kila mwaka. Tukiweza ku-*save* fedha hizo. Ukaziweka kwenye uchumi wa watu wa kawaida, ndiyo namna ya kuwavuta watu wako. Tanzania sasa tunapigana kuhakikishia kwamba kila mtu anapata umeme. Lakini umeme hauna maana kama ni umeme wa *bulb*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakia kila kheri ya krismasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage. Mheshimiwa lazima amesome huyu! Anasema tusitumie mota ya kokoto kukamulia alizeti. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwijage kwa mchango wako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Zitto amejitoa, nafasi yake amempa Mheshimiwa Wenje. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Diana Chilolo. Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kupata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba miaka 10 iliyopita idadi ya Wamachinga waliokuwepo Mwanza walikuwa ni kidogo kuliko ilivyo leo. Idadi ya Wamachinga waliokuwepo Dar es Salaam na waliokuwepo Arusha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

hawakuwa wengi kama walivyo leo. Sababu kubwa ni Serikali yenu iliipoamua kuuza viwanda ovyo ovyo na viwanda vikafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *MWATEX* Mwanza kwa mfano, ilikuwa inaajiri watu mpaka 4,000, watu wasomi na wale ambao hawana elimu, mpaka watu wa kubeba marobota. Leo tuna idadi kubwa ya akina mama Jijini Mwanza wanaouza samaki jioni, maembe, dagaa, ndiyo waende wapate chakula. Lakini hii inatokana na kwamba mliamua kuuza viwanda ovyo ovyo na vikafa vyote. Mkaua *Tanneries* iliyopokuwepo Mwanza, mliua Philips iliyokuwepo Jimboni kwa Mheshimiwa Lema, mliua *General Tyre* ikafa Jimboni kwa Mheshimiwa Lema, viwanda hivi vyote vilikuwa vinaajiri Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitegemea kilimo peke yake, hatuwezi tukaendelea kwa kutegemea kilimo peke yake. Lazima twende kwenye *manufacturing* na hii inatoa fursa kwa ajira kwa kiasi kikubwa. Nyie *technically*, Serikali yenu ndiyo imezalisha wamachinga wanaozagaa leo mitaani. Kwa sababu viwanda mmeuza, hawana kazi nyingine, ndiyo maana leo wako mtaani. Halafu mnarudi kwa njia nyingine kwenda kufanya harambee na kuwalaghai kwa Shilingi milioni kumi kumi ili waendeleo kuwachagua, wakati kimsingi matatizo yao na majonzi yao nyie ndio mmesababisha kwa kuuza viwanda. Leo wanateseka kwenye jua, wanauza chupi na soksi ili watoto waweze kula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *MWATEX* Mwanza kilifungwa ghafla kipindi bado kipo mikononi mwa Serikali. Wafanyakazi waliokuwepo *MWATEX* hawakulipwa fedha zao mpaka leo. Ni muda mrefu, walienda Mahakamani, Kesi ipo Mahakamani, ni muda mrefu kweli. Siku moja nikamshauri Mheshimiwa Kigoda kwamba fanyeni *stocktaking*, ikiwezekana hii kesi iwe *withdrawn* kwenye Mahakama wafanye mazungumzo na wale wafanyakazi wa *MWATEX* zamani ili walipwe fedha zao ili usumbufu kama huu usitokee tena. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hali ngumu kwenye viwanda. Mwanza tuna viwanda vya samaki, tuna viwanda vingine vingi vidogo vidogo, vingine vya chakula. Hali ya ajira kwenye hivi viwanda ni mbaya sana, wafanyakazi wanalipwa fedha kidogo sana, mazingira yao ya kazi ni magumu sana, hata kufukuzwa kazi wanafukuzwa ovyo ovyo, hakuna *job security*. Juzi kulikuwepo na mgogoro mkubwa sana kwenye kiwanda kimoja kipo Mkuyuni kinaitwa Kiwanda cha Magodoro; wafanyakazi wananyanyaswa, watu hawalipwi fedha zao. Sasa Serikali yenu hii ina jukumu la kuangalia pia maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi katika hivi viwanda.

Kwa mfano, kuna wengine wameanzisha Makampuni. Hizo zote ni biashara za ulinzi. Mtu analinda, anaumwa na mbu *the whole day* mwisho wa mwezi analipwa Sh. 70,000/=. Nafikiri kama Taifa tuna kazi. Kama viongozi na nyie Serikali yenu, tuna kazi ya kulinda wafanyakazi wa Tanzania wanaofanya kazi kwenye hivi viwanda vya watu binafsi ili maslahi yao yawe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mazingira ya biashara kwenye nchi yetu. *The cost of doing business in Tanzania*; leo ukipata mfanyabiashara wa Libeti Mwanza au mfanyabiashara anayetoka Lumumba gharama za kufanya biashara imekuwa kubwa sana. Miaka mitatu iliyopita au miwili kulikuwepo na leseni za biashara zinatolewa Halmashauri kwa fedha ndogo sana sijui Sh. 2,000/=. Leo hiyo leseni ya biashara inatolewa mpaka Sh. 200,000/= kwamba wameanza mfumo wa kukadiria. Sasa hili ni ongezeko maradufu. Kwa hiyo, unakuta mfanyabiashara mmoja ana duka Libeti, anatakiwa alipe leseni ya Halmashauri ambayo sasa hivi ni bei ngumu, anatakiwa huyo mfanyabiashara mmoja alipe kodi ya mapato ya *TRA*, anatakiwa huyu mfanyabiashara mmoja anayelipa mpaka kodi ya bango.

Sasa naomba niwaulize hapa. Mtu ameweka bango kwamba labda yeye anauza simu kwenye duka. Hili bango kazi yake ni kuwaonesha wateja kwamba huyu anauza simu ili wateja waende wanunue kwa wingi, ili *TRA* ije ipate

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

mapato. Kwa nini mpaka bango mtu anatozwa? Kama hii haitoshi, huyu mtu analipa hiyo kodi ya bango, anatakiwa sijui alipe kodi ya usafi, usafi ambao pia wakati mwingine haufanyiki.

Kwa hiyo, unakuta mfanyabiashara mmoja ndani ya mwezi mmoja gharama ya kufanya biashara anazolipa, *cost of doing business is so high*. Kumbuka hizi gharama zote, kwa sababu mfanyabiashara anataka apate faida, lazima irudi kwa mlaji. Yaani yule mtu anayekwenda kununua sasa bei ya bidhaa mwisho wa siku lazima iwe kubwa kwa sababu ya gharama ya kufanya biashara imekuwa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotaka kuzungumzia ni kwamba Mwanza kuna nyumba zinaitwa Nyanza *Glass*. Hizi nyumba ziko chini ya *NDC*. Kuna wananchi wameishi kwenye hizi nyumba miaka nenda rudi kwa muda mrefu kweli! Wamezikarabati wao, lakini majengo mengine yamechakaa kweli! Wakaomba Serikali kwamba hizo nyumba wauziwe. *After all* Serikali kama inataka kukarabati zile nyumba, gharama ya kukarabati zile nyumba ni *almost equivalent* na gharama ya kujenga nyumba mpya. Lakini cha kushangaza, Serikali haitaki kuwauzia hawa watu nyumba wakati kuna nyumba moja kati ya hizo nyumba aliuziwa Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa. Sasa hii ni nini? Yaani ni ubaguzi au Wenyeviti wa CCM ndio muhimu kuliko wananchi wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilichukue hili, hawa watu wanaoishi kwenye nyumba za Nyanza *Glass* wauziwe na wako tayari kulipia gharama ambayo Serikali itahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninaloomba kuzungumzia ni kwenye hii suala la Ukimwi. Nasema maambukizi ya Ukimwi hayatapunguzwa kwa kuandaa makongamano na semina za kila siku. Napendekeza, sijui kama kuna sheria na kama ipo sasa isikumwe zaidi. Kila hoteli na kila *guest* nchi hii iwekwe kisheria kwamba wauze *condom*. Ikiwezekana badala ya kuchukua maji, unamwekea mteja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

chumbani kama *incentive*, waweke *condom* kama *incentive*. *I am telling you, this is the only way out!* Hata muuza *chips* pale anapouza *chips* akae na yeye na boksi la *condom*. *Let condom be life style* kama kweli tunataka kusaidia Taifa kupunguza maambukizi ya Ukimwi.

Hatuwezi tukapunguza maambukizi ya Ukimwi kwa kupoteza fedha nyingi kwenye semina na makongamano. *We can only achieve this dream* aliyoyasema Mama Hewa kwamba Tanzania bila Ukimwi inawezekana, *we can only get to that dream if the condom will become life style* ya Watanzania, lakini pia kama maadili aliyokuwa anasema Mheshimiwa Mwijage itakuwa *upheld*, maadili huko tunakotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nashukuru sana Mheshimiwa Wenje. Sikutaka kumkata tu, alikuwa anasema Serikali yenu hii; nikawa najiuliza, Serikali yake yeye ni ipi? (*Makofi/Kicheko*)

Sasa namwita Mheshimiwa Diana Chilolo, mchangiaji wetu wa mwisho.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nichukue nafasi ya awali kabisa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati ya Viwanda na Biashara pamoja na Mwenyekiti wangu wa Masuala ya Ukimwi ambaye mimi ni Makamu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mwenyekiti wangu wa Masuala ya Ukimwi amewasilisha taarifa nzuri kweli kweli na amewasilisha kwa uwezo wa hali ya juu. Nashukuru Waheshimiwa Wabunge walisikiliza kwa makini. Hii inaonesha kwamba suala hili la kupambana na Ukimwi linamgusa kila Mbunge.

Ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge, napenda nimshukuru Mheshimiwa Lukuvi, tunazungumzia hapa suala la kuanzisha Mfuko wa Ukimwi, Mheshimiwa Lukuvi hili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANNA M. CHILOLO]

ameshalifanyia kazi, tayari kwenye Baraza la Mawaziri limeshapitishwa, ametueleza kwenye Kamati yetu. Kwa hiyo, naamini Bunge litakalofuata la kawaida kama hili, Muswada huo utaletwa hapa, Waheshimiwa Wabunge tuje tuunge mkono wote, tuanzishe Mfuko wetu tuachane na tabia ya kutegemea wenzetu ambao sasa hivi wameanza kung'atuka. Sio nchi zote ambazo zilikuwa zinasaidia zinaendelea kusaidia. Nchi nyingine zimeshajichomoa tayari.

Naomba sana hili litakapoletwa hapa, tuliunge mkono kwa nguvu zote ili Muswada huo uanze kufanya kazi, Mfuko wa Ukimwi uanzishwe hapa Tanzania kwa lengo la kupata fedha za kutosha za kupambana na janga la Ukimwi hasa kununua madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, naomba nizungumzie Ukimwi mahali pa kazi. Ndugu zangu naona suala hili la Ukimwi tunalizungumza kimzaha tu, *seriousness* ya kupambana na Ukimwi bado ndogo. Ukiangalia Wizara zetu, hivi kweli zina mkakati wa kupambana na Ukimwi kwenye maeneo yao ya kazi? Ukienda kwenye Taasisi zote za Serikali, ukienda kwenye Mashirika ya Umma: Je, mkakati wa kupambana na Ukimwi upo? Kweli sera tunayoitumikia ni moja, ni hiyo sera ya nchi lakini lazima kila mahali pa kazi pawe na mkakati wake. Naomba nitumie nafasi hii kupongeza Mashirika mawili ambayo yameleta taarifa mbele ya Kamati na tumeyatembelea. Shirika la *PPF* pamoja na Shirika la *NSSF* hawa wenzetu kwa kweli wamejipanga na wanapambana kweli kweli na suala la Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wao kwa wao wanafundishana, wana mikutano, wamejipangia ratiba ya mwaka mzima na wana mikutano ya kila mwisho wa mwaka na wanafanya kazi ya kupima na wale wanaobainika, kwa siri wanapata huduma inayostahili. Naomba Mashirika haya mawili; Shirika la *PPF* na *NSSF* na Mashirika mengine na Taasisi nyingine za Serikali ziige. Mtu akifanya jambo jema ni vizuri tukaiga jamani. Maana wengine hawapo kabisa, wanazungumza tu, ukiwaambia leteni taarifa mbele ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANNA M. CHILOLO]

Kamati, wakikusomea taarifa mpaka unashangaa. Hii taarifa kweli, hawa watu hivi suala la Ukimwi lipo au wamekurupuka baada ya kusikia wanakuja mbele ya Kamati?

Naomba sana Waheshimiwa Wabunge kule tunakotembelea, huko tunakofanya kazi za Kamati zetu mbalimbali, suala la Ukimwi wala siyo la Taifa tu, ni janga la kila mtu. Kila Kamati ihakikishe suala la Ukimwi inalzungumza kwenye Taasisi yake kwa sababu tusipozungumza wote suala hili hatutalimaliza, hatutafikia kwenye 0.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Halmashauri zetu. Huko ndiko kabisa shamba la bibi. Fedha zinapelekwa lakini Kamati zipo, Kamati zile zipo picha tu, hazifanyi kazi na mfuatiliaji hayupo. Naomba ndugu zangu, naiomba Serikali yangu pamoja na Kamati hii kufanya hiyo kazi, pia Serikali ihakikishe inafuatilia hizi fedha kama zinafanya kazi ipasavyo. Kwa sababu Watanzania wanapata shida, wako yatima kule, hawasomi kwa sababu wazazi wao labda walikwishakufa, hawana fedha, hawana watu wa kuwasomesha; lakini fedha zinaenda, Halmashauri kazi yake ni makongamano, mikutano, warsha, semina, mambo haya sasa yafike mahali yakome, tufanye kazi yenye kuonesha mafanikio ya haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya ziara Mkoa wa Njombe. Ndugu zangu Ukimwi kweli unatishia maisha yetu. Tumejaribu kuwauliza; wenzetu, kulikoni huku? Mbona kasi bado inapanda tu? Wengine wanasingizia baridi! Huku tunakunywa pombe sana ili tulewe tupate joto. Kumbe wanapolewa ndio wanashawishika na masuala mengine. Hebu tuwasaidie wenzetu wa Njombe. *(Makofi)*

Vile vile suala la tohara kwa wanaume huko, halipo. Wameelimika, sasa hivi wanatahiri lakini ameingia ibilisi mwingine anawaambia kwamba nyinyi mnaoambiwa kutahiri, nyinyi akina baba mnaoambiwa. Mnataka kuingizwa Uislamu wote! Hivi kweli kuna mada ya namna hiyo hapa duniani? Ipo hiyo? Hapa Tanzania kuna mada ya kuwaingiza watu Uislamu kwa sababu ya kuwatahiri tu?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANNA M. CHILOLO]

Naomba tusiwapotoshe Watanzania. Wako watu, wapo Wachungaji wasiojulikana wanapeleka salamu ambazo zinataka kudhohofisha nguvu ya Serikali, nguvu ya Kamati ya kupambana na Ukimwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleo kwa kuzungumzia suala la wenzetu wa Viwanda na Biashara. Nampongeza sana Mheshimiwa Mchimwa, ametoa taarifa nzuri sana.

Sasa namwomba, huko Singida sisi tunalima alizeti. Nashukuru kupitia msukumo wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Kiwanda cha kusafisha mafuta mara mbili kimeshapatikana. Lakini kiwanda hicho kimoja hakitoshi. Alizeti Singida imelimwa ya kutosha kweli kweli! Naomba tuongezewe na kiwanda kingine ili mafuta yote ya Mkoa wa Singida yawe na kiwango ambacho yataweza kununulika katika ulimwengu wa sasa. Naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nimeona Dar es Salaam wanaingizwa kuku wa kusindika kutoka nje ya nchi. Jamani! Kweli tunahitaji fedha za kigeni, lakini mpaka kuku wa kusindika watoke nje ya nchi, wakati Singida kuku wamefurika! Dodoma kuku wamefurika na mikoa mingine! Hivi kwa nini tusitengeneze Kiwanda cha Kusindika hawa kuku wa asili ambao hawana hata maradhi kuliko kuku hawa walikuzwa kwa madawa? Hata ubora katika afya zetu ni mdogo.

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Naomba sana tupate fedha za kigeni kupitia vitu vingine. Hawa kuku wa kigeni wanaosindikwa, wanaoingizwa sasa Tanzania, naiomba Serikali isitishie. Fedha ya kigeni tunaitaka lakini tuna namna nyingi za kupata fedha za kigeni. Kwa hiyo, naomba sana tufanye hivyo, tutakuwa tumesaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hizi mashine za CD4. Nashukuru siku ya Maadhimisho ya Ukimwi Duniani Kitaifa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANNA M. CHILOLO]

tumefanyia Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri wa Afya ndugu yangu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Oh, ya pili au?

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili eh!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Diana Chilolo - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Ukimwi. Tunakushukuru sana. Nami niwaambie Wajomba zangu huko Njombe, jamani eeh, tohara siyo kusilimishwa! *(Makofi/Kicheko)*

Sasa namwita Mheshimiwa Lukuvi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mwinyi, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami naomba nizipongeze sana hizi Kamati mbili kwa taarifa zao, lakini zaidi niipongeze Kamati yangu inayosimamia Masuala ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya kwa kazi kubwa sana na ushauri mwingi ambao kwa ufupi sana umetolewa hapa, lakini ushauri mwingi tumekuwa tunaupata tunapokutana kwenye Kamati. Hawa watu siyo kwamba wanafanya tu kwa sababu ni Wabunge, lakini wana nia ya kufanya kazi yenyewe.

Kwa hiyo, nawapongeza sana, lakini nawapongeza zaidi kwa kuhudhuria Mkutano mkubwa sana wa Kimataifa kule *Cape Town* wili iliyopita, ambapo nasikia timu yetu ya Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati hii walifika kule, michango yao ime-*shine* katika Mkutano ule, kwa sababu kulikuwa na Wajumbe zaidi ya 10,000. Nawapongeza sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Nampongeza Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo machache nitachangia juu ya mambo ya Ukimwi na Madawa ya Kulevya. La kwanza, ni hili alilolisema Makamu Mwenyekiti kwamba kweli Baraza la Mawaziri limesharidhia kuwepo kwa Mfuko wa Ukimwi. Sasa kilichobaki ni kufanya mapitio ya Sheria Na. 22 ya mwaka 2001.

Kwa hiyo, kwa upande wa Serikali tumeshamaliza, sasa tunajiandaa kuja Bungeni. Ni matumaini yangu kwamba hapa Bungeni tutaielewana ili tuanze kujiandaa kwa tahadhari ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba endapo hawa wenzetu wafadhili wakitoka, basi tuwe na chetu ambacho tumeshaanza kuzoea namna ya kutumia. Lakini pia kwenye taarifa ya Kamati ilizungumzia juu ya fedha ambazo CAG alizona hazijatumika Sh. 1,500,000,000/=. Ni kweli hizi fedha zilionekana lakini tatizo lake ni kwamba zilipokelewa mwisho wa mwaka ndiyo maana zilionekana kama hazijatumika, lakini hivi sasa zinaendelea kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna fedha za *TACAIDS* kama Sh. 222,000,000/= nazo hivyo hivyo zilipatikana mwishoni, lakini zinaendelea kutumika hivi sasa. Ni kweli pia kwamba ingawa Serikali kwa mfano mwaka huu imetenga Shilingi bilioni 17 kwenda kwenye Halmashauri zote nchini kwa ajili ya masuala ya Ukimwi lakini Halmashauri zenyewe kwa vyanzo vya ndani ambazo angalau zimeanza anza hazizidi asilimia 30. Sasa uwiano huu ni mdogo sana. Wakati sisi Kitaifa tunajiandaa kupokea mzigo kutoka kwa wenzetu wanaotusaidia Kimataifa nilidhani sasa Halmashauri na zenyewe zianze kujiandaa ili Serikali Kuu iweze kupokelewa baadaye na Serikali za Halmashauri za Wilaya kwa sababu hizi ndizo zenye watu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hapa naomba tu Kamati za *LAAC*, *TAMISEMI*, *UKIMWI* na Madawa ya Kulevya, mimi naomba sana kila moja kwa wakati wake, mkifika *TAMISEMI*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

mnapoangalia mwenendo wa uendeshaji wa shughuli za TAMISEMI kwenye Halmashauri, hebu mwulize hizi fedha zinafanya nini? Sh. 17,000,000/= siyo fedha kidogo. Lakini angalau mwone hata mipango yao ikoje, isiwe hiyo mipango ya *T-shirt* na kofia wanayoisema hapa. Lakini pia mwulize jitihada gani zinafanywa katika kuwekeza katika mapambano haya ya ugonjwa wa Ukimwi. Kwa hiyo, ningepomba Kamati yetu ya LAAC pamoja na Kamati ya TAMISEMI itusaidie sana katika kuamsha ari ya kusimamia mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kamati ya UKIMWI ningependa niwashauri kwamba hizi fedha zinakwenda na tumeshaanza kuzipeleka, lakini pia Serikali, Wizara zote za Serikali zinatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia mapambano zidi ya Ukimwi na kuwa na *program* ya mahali pa kazi kwa mambo haya. Ningeomba wakati mnaendelea kupitia, basi mjitahidi angalau katika mzunguko wa miezi 12 mpitie Wizara zote ili mwone kila Wizara imetekeleza namna gani. Huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea changamoto zote zilizotolewa na Kamati ikiwa na ujenzi wa zile vile vibanda kwenye vituo vya barabarani. Ni kweli baadhi ya vibanda na nyumba hizi zimejengwa kwa viwango visivyostahili. Ni kweli tumeanza kuchukua hatua, lakini iko moja sasa ambayo tunaijenga nafikiri vizuri zaidi ambayo tunaendelea nayo Handeni. Ziljengwa vibaya na nyingine ziko nje ya mazingira ya watu. Hiyo ni kweli. Lakini tutaendelea kushirikiana na Kamati na wadau mbalimbali ili katika ujenzi wa vituo hivi, katika siku zijazo vijengwe katika maeneo yenye watu na vijengwe vibanda au nyumba zenye hadhi ambazo zinaweza zikatumika na kuleta tija.

Kwa upande wa Ukimwi, nimalizie tu kwa kuwaomba wenzetu wa Halmashauri, wajitahidi sana kusimamia mipango na *program* zote ili wananchi waweze kuona kwamba kazi ya Halmashauri siyo kusimamia tu habari ya maendeleo na kodi, lakini pia kusimamia mapambano dhidi ya Ukimwi. Serikali inapeleka fedha za kutosha, hata wafadhili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

wengine mbalimbali wanashiriki, lakini ni kweli kwamba pamoja na kuunda Kamati zile za Ukimwi za Halmashauri, ukimwona Diwani ameteuliwa kwenda kwenye Kamati ya Halmashauri, labda Diwani huyo na Mwenyekiti haziendi vizuri. Kwanza Mjumbe mwenyewe huyo Diwani akiteuliwa ile Kamati anaona hakupewa Kamati.

Kwenye Halmashauri mtu anataka Kamati ya Fedha, Kamati ya Ujenzi, sana sana kidogo Kamati ya Elimu. Akipigwa Kamati ya Ukimwi, hapo anamwona Mwenyekiti ni mbaya sana. Lakini nafikiri tungekimbilia hizi, kwa sababu hizi tukizifanyia vizuri, zinapoponya maisha ya watu katika maendeleo tunayoishi. Kwa hiyo, Kamati za Ukimwi kwenye Halmashauri ni sawa kabisa na Kamati nyingine. Tusizone kwamba ni Kamati ambazo hazina kazi. Fikiria, kama Kamati hii peke yake imepewa kazi ya kusimamia Shilingi bilioni 17, naamini ziko Kamati nyingine za Halmashauri ambazo kwa mtandao wa bajeti hazina fedha kiasi cha Shilingi bilioni 17. Kamati hii ni muhimu, naomba sana viongozi wenzangu wa Serikali huko Mikoani tunapofanya hata ziara, basi tusimamie, tuangalie mambo haya ya Ukimwi.

La mwisho, nichangie la madawa ya kulevya, nakubaliana na changamoto zote zilizotolewa humu ndani na Kamati, lakini pia Wabunge waliochangia. Ni kweli kwamba tumegundua sasa kasoro katika Sheria, katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya, tumeanza kuchukuwa hatua. Kasi sasa ya mapambano haya imekuwa kubwa na ndiyo maana kila siku haiishi wiki utakuta kuna takwimu zinazoonesha kwamba Serikali imekamata hapa na pale. Kufanya hivi, watu wengine huwa wanafikiri sasa madawa ndiyo yanaingia kwa wingi sana, hapana. Kazi ya Serikali imeimarika zaidi na mapambano yameimarishwa zaidi, ndiyo maana ukamataji umekuwa mkubwa.

Sasa tumeimarisha viwanja vyetu vya ndege, tumeanza na kununua mashine mpya ambazo zitakuwa na uwezo wa kutambua zaidi hasa wale watu ambao wanabeba madawa haya kupitia viwanja vya ndege. Lakini tunabadilisha Sheria, tunatunga Sheria mpya kwasababu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

sasa tumepata uzoefu mkubwa ambao umetuonesha mianya katika ile Sheria ambayo inatugonganisha kati ya wakamataji na watoa haki kwa maana ya Mahakama. Kwa hiyo, tunatunga Sheria mpya ambayo tunafikiri itaziba mianya ili angalau wale wote wanaojihusisha na mambo haya waweze kuchukuliwa hatua stahili kwa mujibu wa makosa yao.

Pia tunaomba chombo kipya. Ni kweli tunaunda chombo kipya ambacho kitakuwa na nguvu zaidi kuliko vyombo vyote ambavyo vilikuwa vinasimamia mapambano haya hivi sasa kutokana na uzoefu tulioupata wa *Task Force* yetu.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema kwamba tumekubali, tumepokea mapendekezo yote ya Kamati na maelezo yaliyosomwa na Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo kushirikiana, tunaunga mkono, tuendeleo kushirikiana, mapambano ya Ukimwi ni endelevu na mapambano ya madawa ya kulevya ni endelevu. Ushindi tutaupata tu hasa kwenye madawa ya kulevya kama wananchi wataendeleo kushirikiana na Serikali. Kazi yote hii inayofanywa anayetusaikia ni mwananachi. Mwananachi ndiye anayetupa taarifa, ndiyo maana ukamataji huu umekuwa mzuri zaidi. Kwa hiyo, tuendeleo kushirikiana ili tuyashinde haya yote, Ukimwi na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Mheshimiwa Lukuvi. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Mwinyi – Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nichukuwe fursa hii na mimi niwapongeze kwa dhati Kamati hii ambayo kwa kweli inafanya kazi nzuri sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Taarifa ya Kamati iliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi na Madawa ya Kulevya kwa kutolea ufafanuzi baadhi ya maendeo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kulikuwa na hoja kwamba kuna uhaba mkubwa wa *condom* kwenye baadhi ya maeneo vijijini. Ukweli ni kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inaratibu upatikanaji wa *condom* nchini ambapo husambazwa kupitia bohari ya dawa hadi vituo vya kutolewa huduma za afya. Aidha, wadau wa huduma za *condom* hufikisha *condom* katika ngazi zote hadi ngazi za vijijini.

Kwa sasa *MSD* wana *condom* zinazotosheleza matumizi ya miezi sita. Usambazaji unaendelea kote nchini kupitia bohari za kanda za *MSD*. Ili kuhakikisha kwamba *condom* zinapatikana sehemu zote za nchi yetu kwa wakati wote, Wizara kupitia Serikali za Mitaa zina mkakati wa kusambaza *condom* zaidi kwenye maeneo ya makundi maalum kama kwenye vijiji vya Wavuvi, mashamba makubwa na kwenye Migodi. Kwa maana hiyo, kuna wakati ulitokea uhaba lakini uhaba huo sasa haupo na tunawahakikishia kwamba *condom* za kutosha zipo na zitaendelea kuagizwa ili uhaba ule usitokee tena.

Eneo lingine ni kwamba, ili kukabiliana na changamoto za ongezeko la mahitaji ya dawa za kupunguza makali ya virusi vya Ukimwi, na kutokana na ongezeko la *CD4*; kutokana na mwongozo mpya wa Shirika la Afya Duniani, Serikali inashauriwa kuanzisha viwanda vya ndani vya kuzalisha hizo dawa za kupunguza makali ya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubali ushauri uliotolewa na Kamati wa kuzingatia umuhimu wa kuanzisha na kuimarisha viwanda vya dawa vya ndani. Serikali imeshaunda kikosi kazi chenye Wajumbe kutoka Wizara ya Afya, Wizara ya Viwanda na Biashara, *COSTECH*, Chuo kikuu cha Muhimbili, *MSD* na *TFDA* ili kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa mpango mkakati wa kuendeleza sekta hiyo. Kikosi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

hicho kimeshaanza kazi na mapendekezo yatafanyiwa kazi na Serikali.

Aidha, Serikali inaweka mazingira wezeshi ili kiwanda kipya kinachojengwa Mkoani Arusha kinachoitwa *TPIRV Limited* kifikie lengo lake la kuzalisha *ARV* hapa nchini. Tutaendelea kuhamasisha sekta binafsi ili waweze kujenga viwanda vipya kwa ajili ya kujitosheleza na dawa nchini mwetu. Ni kwell kwamba dawa kwa sasa kwa asilimia kubwa tunategemea za nje, siyo *ARV* peke yake, ni pamoja na dawa zote kwa ujumla wake. Kwa hiyo, tuna kazi ya kuhamasisha sekta binafsi, tutaweka mazingira hayo wezeshi ili tuweze kupata viwanda vyetu kwa ajili ya kuepuka utegemezi kutoka nje.

Mheshimwa Naibu Spika, hoja nyingine ni uhaba wa utenganishi katika Kituo cha kutolea huduma Mdaula. Wizara ina vitandishi vya kutosha miezi minne kwenye bohari ya madawa. Hata hivyo mwezi wa Januari, 2014 *MSD* itaendelea kupokea vitendanishi vya miezi kumi. *MSD* kupitia kanda zake nchini kote inaendelea kusambaza vitendanishi hivyo kulingana na mahitaji ya vituo ikiwemo Mdaula. Kwa hiyo, ninachosema hapa ni kwamba uhaba huo sasa haupo, vitendanishi vya kutosha vipo na Januari, 2014 tutapata vya miezi kumi. Kwa hiyo, hili tatizo halitakuwepo tena.

Kuhusu huduma ya dawa ya *Methadone*, Serikali inatoa huduma za dawa za *Methadone* katika hospitali ya Taifa Muhimbili, hospitali ya Mwananyamala na Temeke. Hivi sasa waathirika 1,000 wanapata dawa ya *Methadone* na huduma nyingine za Ukimwi, Kifua Kikuu, Homa ya Ini na magonjwa ya ngono. Serikali ikishirikiana na wadau wa maendeleo, inaendelea kutoa huduma za dawa ya *Methodone* na inakamilisha mkakati wa upanuzi wa dawa za *Methodone* kwa Mkoa mzima wa Dar es Salaam na baada ya hapo nchi nzima. Hii ni dawa muhimu inayoweza kuwatoa hawa wanaotumia madawa ya kulevywa. Kwa maana hiyo, tunakwenda kwa awamu, lakini mpango huu utasambazwa nchi nzima.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Kuhusu uhaba wa wataalamu wa kuchunguza dawa za kulevya na sumu pamoja na kufanya matengenezo ya mitambo katika maabara ya Kemia Mkuu wa Serikali, watumishi katika Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni wachache hasa katika kitengo cha huduma za sayansi ya Makosa ya Jinai. Wizara imewasilisha mahitaji ya watumishi ya wakala katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mahitaji ya sasa ni watumishi 120 wa nyongeza kutokana na maombi ya kila mwaka kukosa kibali kwa ufinyo wa Bajeti.

Kwa kupitia mapato ya ndani, Wakala wamejitahidi kuongeza watumishi wa mkataba jambo ambalo kwa kweli ni mzigo kwa Wakala huu. Kwa hiyo, tunachoweza kusema hapa ni kwamba tutaendelea kuomba vibali vya ajira, tutaendelea kupunguza upungufu huu wa wafanyakazi katika wakala huu ili huduma zitolewe kwa haraka zaidi kuliko ilivyo sasa.

Kuhusu uchakavu wa miundombinu, majengo na mitambo katika Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, mitambo imechakaa kutokana na ukweli kwamba ilinunuliwa muda mrefu tokea mwaka 2003. Mitambo mingine ya maabara haizalishwi tena duniani hivyo ni vigumu kupata vipuli vyake, gharama za matengenezo zimeongezeka sana kutokana na kutumia wataalamu kutoka nje ya nchi, kuharibika mara kwa mara na hivyo kusababisha mlundikano wa vielelezo.

Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imetayarisha mpango mkakati wa kuiomba Serikali kutafuta ufumbuzi wa pamoja kwa kuhusisha Taasisi nyingine. Gharama za mpango huu iliwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu na inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 4.7 ili kununua mitambo mipya. Aidha, kuongeza ujuzi wa Wataalamu na kumalizia ujenzi maabara mbili za kanda ya Arusha na Mbeya. Majengo ya Wakala yamechakaa kutokana na kwamba ni ya muda mrefu sana na Wakala unaendelea kukarabati majengo yake pale ambapo uwezo wa kibajeti kutokana na makusanyo ya ndani unaporuhusu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachosema ni kwamba, tunatambua changamoto zinazokabili Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu. Kwa maana hiyo, Wizara itaendelea kutenga fedha katika Bajeti, tutaendelea kuomba Bajeti ya Maendeleo kwa Wakala lakini kuna huo mpango ambao tumeshawasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, wenye thamani ya Shilingi bilioni 4.7 na ni mategemeo yetu kwamba zikipatikana fedha hizo tutaweza kupunguza changamoto hizo.

Aidha, kutokulipwa kwa huduma zinazotolewa na Wakala na Taasisi nyingine za Serikali, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imehakiki deni la Polisi kutoka mwaka 2005 hadi 2013. Deni linafikia Shilingi bilioni 1.1. Wizara ya Afya imewasiliana na Wizara ya Mambo ya Ndani ili utaratibu wa kulipwa kwa deni hilo ufanyike na hivyo kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake. Tutaendelea kufuatilia madeni haya ili kuipa nguvu zaidi Wakala iweze kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya upimaji wa damu kwa wajawazito kwamba isiwe hiari. Ilitolewa hoja hiyo, nami niseme tu kwamba ni kweli. Dawa hizi zikitumiwa na wanawake wajawazito kuna uwezekano mkubwa wa mtoto kutoambukizwa. Kwa sasa uwezekano wa uambukizaji ni 15%. Yaani kila wajawazito 100 ni 15 tu virusi vinakwenda kwa watoto. Kwa hiyo, ni muhimu sana tutumie. Hali hii tunataka tuendelee kuipunguza mpaka mwaka 2015 tunategemea *transmission* ya virusi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto iwe ni 4%.

Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba wajawazito wapime afya zao na wakionekana wana virusi hivyo, basi waanze kupata dawa. Sasa tumeanza mpango mpya ule tunaoita *Plan B+* ambao unatoa dawa kwa ajili ya tiba ya wajawazito lakini vile vile inamkinga mtoto kwa maisha yake yote. Kwa maana hiyo, tunachosema hapa ni kwamba upo umuhimu wa wajawazito kupima. Lakini haki ya mhusika kupima kwa hiari yake, bado inazingatiwa. Lakini cha msingi hapa tuendelee kutoa elimu ili wanawake waweze kuelewa hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Kuhusu umuhimu wa tohara katika kukinga Ukimwi, jambo hili halina mjadala. Tohara ina kinga kwa kiwango kikubwa sana maambukizo ya Ukimwi.

Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba ni muhimu sana na ndiyo maana kuna mpango maalumu wa Serikali wa Tohara ili kukabiliana na ugonjwa huu. Kwa sasa kuna Wilaya nyingi sana; Mikoja mingi sana tayari tumeshaanzisha mpango huu na tuendeleo kuhamasishana na kuziomba Taasisi mbalimbali ziendee kuhakikisha kwamba mpango huu unaenezwa ili kupunguza maambukizi kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa kumalizia niseme tu kwamba Wizara yangu ina kazi kuu mbili katika masuala ya Ukimwi. Moja, ni kinga. Ndio maana tuna mpango wa Damu Salama ili kuhakikisha damu zote wanazopewa wagonjwa ni salama.

Vilevile tuna mpango wa tohara kama ambao nimeshauzungumzia sasa hivi, tuna mpango wa kusambaza *condom*, na mwisho tuna mpango huu wa kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Hiyo ni mipango ya kinga. Lakini sasa hivi hata kutoa dawa zile za Ukimwi ni kinga, kwasababu imethibitika kwamba wanaotumia dawa zile za Ukimwi (*viral load*) vile virusi vikipungua sana katika damu hawawaambukizi wengine.

Kwa hiyo, kuna kila sababu ya kila mtu kupima na sasa *CD4 count* zitakuwa zimepanda mpaka kufikia 500 watu wataanza kupewa dawa hizo ili hatimaye tupunguze kwa kiwango kikubwa *viral load* na yenyewe itakuwa ni kinga, ukiacha kuwa ni tiba.

Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba kuna umuhimu zaidi wa kuongeza masuala haya niliyoyataja ya kinga, lakini katika upande wa tiba Wizara sasa hivi ina zaidi ya watu 600,000 wanaopata tiba ya Ukimwi na tutaendelea kutoa dawa hizo bila malipo ili kuhakikisha kwamba dawa hizo zinawapa maisha marefu wale ambao tayari wameambukizwa, lakini wakati huo huo watapumbukiza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

uwezekano wa kuwaambukiza wengine. Kwa hiyo, tunasema masuala hayo yanashughulikiwa kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nami naomba niunge mkono hoja hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Mwinyi - Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Sasa nimwite Naibu Waziri Fedha - Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nachukua fursa hii kuipongeza sana Kamati yetu ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri ambayo tumekuwa tukifanya pamoja nao na tutaendelea kushirikiana katika kukamilisha kazi zile zilizopo. Kwetu sisi kama Wizara ya Fedha, tunachakuwa ripoti hii kama *working tool*. Tutaifanyia kazi na tutahakikisha yale yote ambayo yamekuwa *proposed* tunayatekeleza kadri ya sheria na taratibu zinavyoruhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuchangia hoja zilizotolewa kwa kutoa ufafanuzi baadhi yake na nyingine tutazichukua kuzifanyia kazi kwasababu muda umekuwa mdogo.

Kubwa ambalo limejitokeza kutoka kwa kila Mbunge ni kuhusiana na riba kubwa ya mabanki, lakini benki nyingi zipo Mjini. Hilo ni kweli halipingiki, lakini naomba nitoe ufafanuzi kwamba pengine tungefikiria kwenda mbele zaidi. Leo tukisimama hapa tukasema kwamba Benki nyingi ziko Mjini, lakini pengine labda tunadhania benki ni jengo. Lile jengo likiwepo pale na ile nembo yake mfano *NMB*, ndiyo Benki. Lakini Benki ni huduma. Kwa hiyo, mahali popote ambapo huduma zikipatikana zinazohusiana na Benki ni Benki. Kwa hiyo, tunachopigania hapa ni kule vijijini wapate huduma za kibenki na siyo Benki kuwepo Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, nikisimama leo hapa, simu yangu hii ni benki. Hii

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

simu yangu ni benki, maana humu naweza kuona akaunti yangu; kuanzia hapa naweza kufanya *transanction*, kulipia bili na kufanya kitu kingichochochote. (*Makofi*)

Sasa basi, wakati tukisema Serikali kupitia Benki kuu imeshaandaa *regulations*, inatekeleza *regulations naturally* kwamba tunafanya *Agency Banking* maana yake ni kuweka vituo ambavyo vitakuwa vinatoa huduma za kibenki mahali zilipo. Maana Waheshimiwa Wabunge kusema tujenge benki vijijini nayo ina gharama yake. Ndiyo tunaposema kwamba riba ni kubwa. Riba ni ile gharama pamoja na uendeshaji wa zile Benki huko vijijini. Maana yake ni nini? Tukiwa tumeshajihisha sana wananchi kutumia teknolojia (wakati ndiyo tunakoelekea), tumeshajihisha sana Serikali yenyewe kutumia mtandao, teknolojia, pamoja na mabenki maana ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji ikiwemo hiyo gharama za mabenki huko.

Kwa hiyo wakati Waheshimiwa Wabunge hilo tunalizingatia na tunalipigia kelele, nadhani sana tushajihishe sasa ile *Agency Banking* iweze kufanya ili kazi vijijini kuliko kushajilisha benki ziende vijijini *physically* zikaweke majengo zikajenge ama zikakodi zikaweke wafanyakazi, hapo ndipo tunapozalisha gharama nyingine. Tutashindwa, mwisho wa siku kuzi-*sustain* na badala yake, badala ya kupunguza sasa ule mzigo wa riba, tutakuwa tunamwongezea mwananchi. Naomba tuwepo pamoja katika hili, sisi kama Serikali wala hatutasema kwamba lazima mwende vijijini kwenda kusema kwamba *okay* tunajenga Benki, hapana. Tutahakikisha kwamba tunatumia teknolojia kwa wananchi wapate huduma za kibenki. Hilo ndiyo muhimu wala siyo kwenda *physically*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limesemwa sana labda ni suala la deni la Taifa. Tumeshalielezea sana, lakini mara nyingi linakuja vingine vingine katika mtiririko mwingine. Lakini nadhani eneo lote hilo, lolote linalosemwa hapa sisi tayari tumeshali-*address*. Tumeshajibu, tumeshaelezea. Pengine labda tu kumetolewa rai kwamba tuwe tunaleta hapa Bungeni kujua kiasi gani cha deni,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

tunakopa wapi; lakini Waheshimiwa Wabunge tunasahau kwamba tunapopita Bajeti ya Serikali, katika *frame work* yote ile ya bajeti tunaelezea kwamba fedha kiasi fulani Serikali itakusanya mapato yake ya ndani kupitia *TRA*; Kiasi fulani tutapata kutoka Washirika wa Maendeleo, kiasi fulani yaani tunaleta katika *holistic picture*. Pengine labda ni ushauri mzuri Waheshimiwa Wabunge tutaleta hapa tuje na *break down* kabisa.

Kikubwa tu ambacho hatutaleta hapa, tunapopitisha pale bajeti ya Serikali, hususan kwa mikopo ambayo ni ya kibiashara, bado tunakuwa hatujamtambua nani atatukopesha.

Kwa hiyo, tu litakosekana. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge. Tutaleta kwamba *this is the amount* ambayo tumekuwa tukileta siku zote, *any way. This is the amount* lakini hatutaweza kuleta maelezo kwamba nani atatukopesha, kwa riba gani, kwa sababu hivi vyote ni vitu ambavyo tuna-*negotiate*. Hivi vyote tuna-*negotiate* baadaye. Siyo pale wakati ambapo tunasoma bajeti. Hilo tutalifanya.

Waheshimiwa Wabunge, lingine lilikuwa ni kuhusiana na mashine za kielotroniki (*Electronic Fiscal devices - EFDs*). Mwezi uliopita tu tuliona sana wananchi wetu wakipiga kelele sana kuhusiana na hizi mashine za kieletroniki. Mengi yamesemwa na tumefanya mikutano mbalimbali. Maana tuseme kwamba Serikali haijatoa *statement*, hilo siyo la kweli. Tumefanya mikutano mbalimbali na Waandishi wa Habari, mpaka leo hii mwandishi wa Habari anaweza akakupigia simu anaulizia maeneo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nadhani lazima tu-*recognize* angalau tu-*appreciate effort* ya Serikali ambayo imekuwa ikifanya toka hilo lilipoibuka. (*Makofi*)

Sasa katika hili tumeambiwa kwamba ile *extention* labda ilifanywa kwa Dar es Salaam na nini na nini. Siyo kweli. *Statement* tuliyokuwa tumeitoa ya *extension* mpaka tarehe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

31 Desemba ni kwa Tanzania nzima, wala haikuwa ya Dar es Salaam peke yake.

Tulipokuwa tuki-*address* Waandishi wa Habari tuki-*address* pale mbele ya Waandishi wa Habari tulikuwa tuna-*address* Tanzania nzima. Kwa hiyo, *whatever* tulichokuwa tukikizungumza pale kilikuwa kina-*reflect* Tanzania nzima. Haikuwa kwa Dar es Salaam tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeambiwa, labda kuna tatizo lingine na hili nimelisikia mara kwa mara kwamba mtu anaponunua ile mashine halafu akiwa hafanyi tena biashara kwamba hawezi akampa mtu mwingine mashine. Labda nilitolee ufafanuzi. Unapoinunua mashine, unakwenda sasa kuunganishwa na *network* zilizo. *Network* hizo maana yake nini? Una jina lako, *TIN number* yako, una duka pale na kila kitu. Kwa hiyo, inapotoka risiti inatoka pamoja na *details* zako. Sasa ukiwa umeshafunga duka lako au hujaweza kuendelea tena na ile biashara, *obvious with those details* kutokana na taarifa hizo, huwezi kwenda kumpa mtu mwingine tu kama hivi naweza nikakupa simu yangu Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi! Nikikupa hii itabidi ni-*delete number* zangu zote, vitu vyangu vyote, halafu nakugawia hii simu.

Sasa cha kufanya hapo, hatumkatazi mtu kama amemaliza biashara yake, hawezi tena kuendelea na biashara, kwamba hawezi tena kutumia ile *EFD*. Anaweza kumpa mtu mwingine, lakini arudie zile hatua ambazo alirudia mwanzo. Uende pale ukafute zile *information* zako, ukafute zile taarifa zako ili unapomuuzia huyo mwenzako, maana yake na yeye anaanza upya ku-*register with information* zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo liko hivyo, wala huzuiwi. Hilo lisichukuliwe kwamba tena kila mtu akawa, *no*, sheria yetu iko pale pale. *Fourteen million, forty million EFD* unatumia. *Unless* kwamba kweli tukihakikisha kwamba huyu mtu amefilisika na amebaki na kile kidude chake, hawezi tena kukitumia, hiyo inawezekana. *You go* kwa huyo mtu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]
aliyekuuzia, kwa *TRA or somebody* unaondoa *informations* zako, basi. Huyu mwingine utakayemuuzia na yeye atakuja ku-*register* na yeye aingize *information* zake. Kwa hiyo, hilo liko hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine tutaendeleza kutoa elimu, tunaendelea. Tunaendelea na tutaendelea kutoa elimu, maana juu ya yote, kelele zote maana yake kila mtu anakuja na taarifa yake, mara sijui nini, sijui laki ngapi, hakuna. Sisi tutaendelea kutoa elimu. Hii yote tuligundua kwamba kweli pengine kundi kubwa lilikuwa halijapata elimu, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Tutatekeleza yale yote. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana kwa mchango wako. Dakika kumi ni ndogo sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kigoda na mwisho atakuwa Mheshimiwa Dkta. Mary Nagu.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie kidogo katika hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, naipongeza sana Kamati chini ya Uwenyekiti wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa. Kwa sisi Wizara ya Viwanda na Biashara, Kamati hii ni *think tank* na napenda kuihakikishia kwamba yote waliyoyaagiza tutayafanyia kazi. Kwanza, suala la kuimarisha *TBS* tunaendelea nalo. Nimeshukuru kwamba Kamati imekwenda Japan, imerudi na wametupa mapendekezo, wameona kwamba badala ya kuendelea pia na *PVOC* vile vile tuangalie suala la kuimarisha *Destination Investment*.

Suala la Zanzibar, tayari *Zanzibar Bureau of Standards* imeshaanzishwa na hivi sasa tunasaidiana nao kuona ni vipi watafanya kazi kwa tija. Changamoto kubwa tunayoipata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

ni kwa suala la *EPZA Bagamoyo* na *Kurasini Logistic Centre*. Hii ni ni kwa sababu ya ukosefu wa fedha, suala ambalo tunashirikiana kikamilifu na Hazina kuona kwamba fedha hizi zitapatikanaje. Mradi wa Kurasini tutakapoumaliza utatoa ajira kwa watu 25,000, utakuza uchumi wetu. Lakini mradi wa Bagamoyo pamoja na Bandari ya Mbegani inatarajiwa kuchangia karibu asilimia 25 ya uchumi wetu. Kwa hiyo, miradi hii itakapoendeshwa itasaidia sana katika kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa ambalo tunalifuatilia hapa ni kwamba tunachotaka ni fedha za fidia ndiyo tunazozipigia kelele. Tumeamua katika kipindi hiki kwamba fedha za fidia tutakazopata hatutawapa wananchi wa Bagamoyo kama fedha, lakini tutawajengea nyumba kulingana na nyumba wanazoondoka katika eneo lile. Hili pia tutalifanya huko Ngaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Assumpter na Mheshimiwa Genzabuke wamezungumzia masuala ya ulinzi wa viwanda vyetu. Tunakubali hoja zao. Tunayo *FCC*, tunayo *TBS*, tunayo Hazina kupitia *TRA*, tutaona ni jinsi gani ya kulinda viwanda vyetu, lakini vile vile tutaangalia hali halisi iliyopo. Kwa sababu sasa hivi ingawa tunazalisha *cement* tani milioni 2.9 hivi, mahitaji yetu ni 3.9. Sukari tunazalisha karibu tani 320 na mahitaji yetu ni tani 500,000.

Mafuta ya alizeti ingawa tumeyazungumza kwa kipindi kikubwa, lakini taarifa kutoka Wizara ya Kilimo inaonesha wazi kwamba bado tuna upungufu wa mafuta haya. Sasa tunachofanya ni nini? Sasa hivi tumeshatuma *researchers* katika viwanda vyote vya *cement* ili tuone *cement* ile inazalishwa kwa bei gani ili ile *affordability* kwa wanunuzi itakapofika madukani na tuweze kulinganisha na gharama za uzalishaji na zile tunazouza.

Kwenye suala la sukari tumelielewa vile vile. Tunaungana na hoja kwamba wazalishaji waingie katika utaratibu wa kununua sukari hizi ya ziada, lakini hili ni suala

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA VIWANDA NA BIAFHARA]

ambalo tutatuzungumza na wenzetu wa Wizara ya Kilimo tuone tunakwendaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *Intertek* limezungumziwa, tunalo. Ingawa Kamati imezungumzia suala la mafuta dhaifu, lakini vile vile napenda kutaarifu kwamba *TBS* vile vile wamekamata mabati dhaifu ambayo yalikwishaidhinishwa na Kampuni hii. Lakini utaratibu unaofanyika sasa hivi ni kuona kwamba tunalipeleka suala hili kwenye *Arbitration* kwa sababu suala la kimkataba na la kisheria ili tuone hatima ya kuendelea na mkataba na Kampuni hii. Kwa hiyo, nalo hili pia tunalifuatilia.

Mheshimiwa Daktari Kafumu pia ameongelea vizuri, lakini napenda kumwambia Dkt. Kafumu kwamba mkakati wa kuendeleza viwanda Tanzania tunao na mimi naweza kusema kabisa kwamba hali ya maendeleo ya viwanda katika nchi yetu inaendelea vizuri pamoja na changamoto zilizopo.

Tunao mkakati wa *Industrial Integrated Development Strategy* ambao unaangalia viwanda mama. Sasa hivi tunashughulikia kiwanda cha chuma cha Liganga na Mchuchuma ambacho tunarajia mwaka 2014 uzinduzi wake na kuanza ujenzi wa viwanda vile. Sasa hivi tuna kiwanda cha Ngaka kule Kusini ambacho kinatoa makaa ya mawe ambayo tunauza kwenye viwanda vyetu na makaa mengine ya mawe tunayauza nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuhakangaika mradi wa Engaruka wa *Soda Ash*, lakini vile vile tunahangaikia mradi wa *Singida Wind Pool* kama miradi mama ili kuweza ku-*support* kwa viwanda vingine vya kati. Kwenye viwanda vya kati, tuna viwanda hapa nchini karibu 733 ambavyo vipo na ukiacha hivyo, sasa hivi kupitia *EPZ* tayari tuna viwanda vingine 81, na kati ya viwanda hivyo vingine 81, karibu viwanda 17 peke yake ni viwanda vya nguo. Kwa hiyo, hatuwezi kusema kwamba viwanda hakuna. Tunajitahidi pamoja na changamoto zilizopo hasa changamoto za umeme.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye viwanda vidogo ambavyo ndiyo sehemu ya tatu, tuna *SMEZ* viwanda vidogo karibu milioni tatu ambavyo vinaajiri karibu Watanzania milioni tano mpaka tano na nusu. Viwanda hivi vinatoa ajira asilimia 27, lakini vile vile hivi vinachangi pato la Taifa karibu asilimia 23. Kwa hiyo, hali ya viwanda, pamoja na jitihada kubwa tunazotakiwa kufanya, hatuwezi kusema hali ya viwanda ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile viwanda vilivyobinafsishwa, tayari tumeshafanya utaratibu katika Wizara yangu pamoja na *CHC* kwa maana ya *Consolidated Holding Cooperation* kuona tunafanya utaratibu gani vile viwanda ambavyo Serikali ina mkono wake kwa maana ina *shares* zake na vile viwanda ambavyo viko moja kwa moja kwa Sekta Binafsi tuone kwamba tutavifanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nitoe tahadhari kwamba hapa tunazungumzia vile viwanda ambavyo vinasuasua tuone ni jinsi gani ya kutafuta wawekezaji kuviboresha zaidi. Lakini kwa vile viwanda vilivyokufa, cha msingi ni kuwauliza wamiliki kwa nini vimekufa. Lakini kama tunavyojua kitu kikishakufa kufufuka ni taabu tena. Inabidi katika maeneo yale tujenge viwanda vipya, tuwaitishe wawekezaji ili tuendeleze viwanda vyetu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Brella, tumeshashughulika, tuko karibu sasa kupata Mkurugenzi, *TBS* karibu tunapata Mkurugenzi na *SIDO* tumeshapata Mkurugenzi. Tunahakikisha kwamba nafasi zote hizi zitafanyiwa kazi ili tufanye kazi kwa tija na ufanisi.

Vile vile Mheshimiwa Wenje amezungumzia sana suala la Wamachinga. Mimi napenda kumhakikishia tu Mheshimiwa Wenje kwamba suala Wamachinga huwezi kuliweka na viwanda. Suala la Wamachinga ni la uchumi mzima. Lazima tufanye jitihada kubwa kwenye Sekta ya Kilimo, lazima tufanye jitihada kubwa kwenye Sekta ya Viwanda ili kuona ni jinsi gani tutajenga ajira kubwa sana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

kwa wananchi wetu ambao hivi sasa kwa kweli wapo na tunaangalia utaratibu wa kuona tunawasaidiaje.

Zile nyumba za *Nyansa Glass*, ziko chini ya *NDC*, nyumba moja iliuzwa kabla ya *NDC* kuchukua nyumba zile na kimsingi mpaka sasa *NDC* haiuzi nyumba zile. Kwa hiyo, jibu nililolitoa kwamba *NDC* haiuzi ni kwamba haitauza. Yule aliuziwa wakati nyumba zile zinamilikiwa na *Nyansa Glass Containers*.

Mheshimiwa Pindi Chana anasema tujitahidi kuhamasisha wawekezaji katika utengenezaji wa zana za kilimo. Tayari tuna mwekezaji ambaye ni *Tembo Agro* kutoka Oman anaunganisha matrekta hapa nchini. Lakini vile vile tunayo Kampuni kutoka Pakistan wanawekeza katika matrekta. Lakini vile vile tunazo kampuni kama tatu, nne zinawekeza katika usafiri mdogo mdogo ambao unaweza kusaidia hata katika maeneo ya shambani. Kwa hiyo, hayo ni maeneo yote ambayo tunaweza tukayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuseme kwamba zipo changamoto kubwa sana ambazo Wizara ya Viwanda tunaikuta hasa katika suala la viwanda na hii ni changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa *energy* ya kutosha. Ndiyo maana sasa hivi tunafanya jitihada kubwa pamoja na kuanzisha viwanda vingine vya nguo Shinyanga, pamoja na kuanzisha viwanda vya nyama Shinyanga na Ngara.

Pamoja na kufanya utaratibu wa kupeleka kiwanda cha *cement*, mimi nishazungumza na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, tumeshaweka mikakati ya kuona ni jinsi gani tunaweza kupeleka kiwanda cha *cement* kule. (*Makofi*)

Sasa masuala yote hayo yanataka ufuatiliaji na tunawahakikishia kwamba Wizara yetu tutajitahidi kuona hayo yanafanyika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Dkt. Kigoda. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii ya awali kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu.

Napenda vile vile kuungana na Mheshimiwa Kigoda na wengine kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu na Wajumbe wote kwa kazi nzuri waliofanya. Kamati hii ya Uchumi, Viwanda, Biashara na Uwekezaji iliwasilisha Taarifa ambayo kwa kweli tutakubaliana wote kwamba imefanyiwa kazi sana. Namshukuru yeye pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao wa kila siku kwa mambo mengi ambayo tunafanya pamoja. Ushauri waliotupa na hoja walizotoa ni za msingi na zitasaidia ushiriki wa Watanzania katika kusimamia na kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza inazungumzia kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa na kutolewa na Serikali kwa ajili ya Mfuko wa Uwezeshaji wananchi wa Tanzania kiuchumi na hata ya uwendeshaji. Hii ni changamoto kubwa. Sitaki kuiona kama ni tatizo, lakini ni changamoto. Mfuko wa uwezeshaji mwananchi ulizinduliwa tarehe 28 mwaka 2008 kwa kuanzia na mtaji wa Shilingi milioni 400 tu na sasa fedha zile zimefikia Shilingi bilioni 2.48. Imeongezeka, lakini kwa kweli mahitaji ya uwezeshaji ni makubwa sana. Kwa kujua hilo, nalipongeza sana Baraza, badala ya kukopesha wananchi fedha zile, waliongea na kufikia makubaliano na Benki ya CRDB ili Benki ikopeshe mara tatu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI)]

Kwa hiyo, Benki imeshakopesha zaidi ya Shilingi bilioni 11 kutokana na dhamana ya Shilingi bilioni 2.8. Kwa hiyo, ni ubunifu mkubwa. Kama mtakavyoona, fedha ni ndogo, tutahimiza, tutahamasisha Serikali kila mwaka katika bajeti yake kuongeza fedha hizo za mfuko na ikiwezekana fedha za Mheshimiwa JK nazo zipitie kwenye Baraza ili kama Shilingi bilioni 25 zitapelekwa kwenye Baraza maana yake mabanki yatakopesha mara tatu, itakuwa takribani Shilingi bilioni 75 au bilioni bilioni 100 na nina hakika hata vijana wetu watapata mtaji kwa wale ambao wako tayari kuanzisha miradi yao.

Pamoja na fedha hizi kuwa ndogo, Baraza limejitahidi sana kueneza dhana ya uwezeshaji. Ni dhana pana, nimeshawahi kueleza, lakini tutaleta semina humu ndani ili tuone upana wa dhana ile. Vilevile kwa kutambua kwamba Baraza haliwezi kumudu kazi ya kuwezesha peke yake, imetayarisha Mwongozo wa Kitaifa wa Mpango Mkakati wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwa lugha kigeni *National Multi-Sectoral Strategic Framework for Economic Empowerment*. Mkakati unatambua kuwa kuna wadau wengi wanaoweza kuwezesha wananchi wengine. Baraza peke yake na Serikali hatutaweza. Wadau hao ni pamoja na sekta binafsi. Jana tulikuwa na Mkutano mkubwa sana wa Baraza la Biashara. Jambo kubwa lililoongelewa mle ndani ni uwezeshaji wa Watanzania ili waweze kushiriki ipasavyo ndani ya uchumi na kushika hatamu ya uchumi wao wakati wakikaribisha wawekezaji kutoka nje bila ya wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishirikiana na wadau hao, ninaamini itachukua muda lakini ninaomba, Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba shughuli za uwezeshaji hazijaanza siku nyingi na imeanzia mbali sana. Tumeanza na sera mwaka 2004, lakini Mfuko umezinduliwa mwaka 2008. Kwa hiyo, kadri ambavyo kazi imefanywa, sina wasiwasi kwamba siku moja hatimaye wananchi Watanzania kuwa watazamaji, itakuwa ni historia, badala yake watakuwa wameshika hatamu ya uchumi wa nchi yao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI)]

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukua mapendekezo hayo na itaifanyia kazi kwa bidii zote.

Hoja nyingine iliyotolewa ni kuhusu viwango vya riba kuwa juu. Namshukuru Mheshimiwa Kaimu Waziri wa Fedha ameliongelea vizuri, lakini suala la riba kwa kweli ni suala la sera, na ni suala ambalo lazima tuliangalie. Kwa uchumi mdogo nilionao mimi, riba ikiwa juu kuliko faida inayopatikana kwenye ujasiriamali, maana yake wale watu wakikopa Benki watakuwa masikini zaidi. Kinachotokea sasa ni watu kutokukopa Benki.

Kwa hiyo, namsihi Waziri wa Fedha na Benki Kuu waone sera hii ambayo itafanya riba iweze kwenda chini, lakini nawaomba Watanzania nao wawe waaminifu, kwa sababu kadri ambavyo haturudishi fedha hizi za Benki, gharama inakuwa kubwa kwa Mabenki kuweza kokopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba kuna idadi kubwa ya Mifuko ya Uwezeshaji. Hili ni kweli, na ukiangalia fedha imetawanyika. Wakati fulani nilieleza kwamba, ukiangalia fedha ambazo ziko kwenye Mifuko hii ni mingi, inafikia takribani Shilingi bilioni 600 lakini huoni uwezeshaji. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ameunda kikundi kazi kuboresha ufanisi wa Mifuko ya Uwezeshaji, lakini ametaka kuona kwamba kila Mfuko unafanya nini ili ambayo inashabihiana, iweze kuunganishwa. Kwa hiyo, nawashukuru sana Wajumbe kutoa hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi ili Watanzania waweze kuwa na Serikali yao katika kuendesha miradi na katika kupewa mitaji ili waweze kuendesha miradi hiyo. Wakati mingine wale wenye mitaji yao waweze kusaidia Serikali ifanye mambo ambayo hayana faida na sekta binafsi inafanya yale yenye faida. Tuna sera, tuna sheria, tuna mikakati, na ni mtindo mpya ndani ya nchi ambao unachukua muda lakini kwa hakika tutautekeleza na nina hakika utaleta manufaa makubwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI)]

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitolewa hoja nyingine kwamba wananchi vijijini waelimishwe kuhusu uwekezaji na uwezeshaji.

Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa wananchi wa Tanzania kupitia Bungeni, hakuna Taifa ambalo uchumi wake utakua bila kuwekeza. Lakini Taifa litakuwa na uhakika uchumi wake kama Watanzania wenye watawekeza zaidi. Ndivyo ilivyo sasa hivi kwamba kwa idadi na kwa thamani ya uwekezaji, Watanzania ni wengi kuliko wale wanaotoka nje, lakini kwa kweli uwekezaji bado ni mdogo. Ungekuwa ni mkubwa tusingeweza kusikia kwamba vijana wanalilia ajira na hawapati ajira na kuna Watanzania ambao hawana ajira.

Kwa hiyo, ofisi yangu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu tutajihidi sana kuhimiza uwekezaji wa ndani na wa nje. Vilevile tutahimiza ubia ndani ya Sekta za Umma na Sekta ya binafsi. Namshukuru sana Mheshimiwa Kigwangalla, amesema kwamba wameanzisha *SACCOS* kule na wataanzisha Benki. Kwa hakika hayo ndiyo tunayopenda kuyasikia kwa wananchi kwamba wenyewe wameanzisha miundo yao na wanawekeza akiba na wanawekeza kwenye miradi mbalimbali. Baraza halitasita kuja kuwaona na watakuja, nitawaelekeza waje waone wapi ambapo wanaweza kusaidiana na ninyi ili kuimarisha miradi yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihimize *VICOBA*, naomba nihimize Ushirika, naomba nihimize uwekezaji akiba na kuwekeza kwenye miradi ambayo inafida.

Namshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo, tumeshirikiana naye sana kuweka kile Kiwanda. Kiwanda kile sasa kinafanya wakulima wapate soko ambalo lina uhakika. Sio wa Singida tu, na wa Shinyanga, Mwanza, Manyara na Arusha. Arusha kuna Kiwanda kingine. Kiwanda hiki kazi yake itakuwa ni kusafisha mafuta ambayo yamekamuliwa na vinu vidogo kutoka kwa wakulima. Kwa hiyo, Kiwanda hiki kitasaidia sana kujenga uchumi wa watu wa Singida na wale ambao wanaizunguka Singida.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI)]

Mheshimiwa Naibu Spika, naahidi kwamba hayo yote yaliyotolewa yatafanyiwa kazi, na nina hakika yataimarisha utendaji kazi wetu na tutaendelea kushirikiana na Kamati yetu hii kama wao wenyewe walivyoonesha ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninalishukuru Bunge lako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Sasa niwaite Wenyeviti wetu waje wafanye hitimisho la hoja zao nikianza na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa. Karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti, jitahidi uwezavyo isizidi dakika ishirini.

MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA - MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maadishi na kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Nagu na Mheshimiwa Dkt. Mgimwa. Kwa namna ya kipekee naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Kigoda, na Mheshimiwa Teu kwa ushirikiano mkubwa wanaoonesha kwenye Kamati yangu. Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Saada na Mheshimiwa Mbene ambao ni Manaibu Waziri wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji waliochangia kwa maandishi wako saba na wachangiaji waliochangia kwa kuongea wako 17. Michango mingi imeelekezwa kwenye sera za Viwanda. Wachangiaji wengi wameelekeza kwenye Sera ya Viwanda, wamezungumzia sana matatizo ya viwanda vilivyoko hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nchi yoyote duniani ambayo imeweza kuendelea ambayo hakuna mapinduzi ya viwanda. Hakika nchi yetu inatakiwa ilianguilie hilo na ilifanyie

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA]

kazi. Kwa hiyo, inatakiwa tujikite vizuri zaidi katika Sera ya Viwanda. Hatuna sera ya msingi ya kufufua viwanda, na hatuna sera ya msingi ya kulinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa sababu za kutoza kodi ni kulinda viwanda vya ndani. Lakini utakuta kwenye baadhi ya maeneo badala ya kuvilinda viwanda vya ndani tunavikwamisha. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo badala ya kuvisaidia viwanda vya ndani tunavizamisha kwa kulazimisha kutoza kodi kwenye *raw material*. Lakini kwenye eneo lingine kuna baadhi ya bidhaa zetu, kwa mfano bidhaa zinazotokana na *Textile Industry* tunazitoza kodi ya *VAT*, matokeo yake tunaifanya bidhaa tunayoizalisha hapa nchini inakuwa ghali zaidi kuliko bidhaa tunayoagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tutaamua kuvilinda viwanda vyetu vya ndani, tutakuwa na uhakika wa ajira ya kutosha, tutakuwa na uhakika wa mapato ya kutosha na tutakuwa na uhakika wa kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchumi mmoja alisema, *"demand of agriculture product is limited by the human capacity while of that manufactured have got no limit."* Kwa hiyo, kama hatutajimarisha kwenye uzalishaji wa viwanda hakika maendeleo yetu katika nchi yetu yatakuwa hayana matatizo.

Waheshimiwa Wabunge wengi kwenye eneo hili wamechangia. Alichangia Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Bukwimba na Mheshimiwa Paresso. Walisisitiza sana katika eneo la viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni mchango wa Mabenki katika uchumi Taifa kwamba bado ni mdogo. Tuna Mabenki 53 lakini Mabenki mawili tu, *NMB* na *CRDB* ndiyo zinapatikana katika Wilaya zote katika nchi hii. Sasa Serikali inatakiwa ilianganalie jambo hili, ihakikishe Mabenki haya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA]

mengine ambayo yanaanzishwa yanakwenda kwenye vijiji kusudi yaweze kuwasaidia wanachi walio wengi katika vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Benki zinaonekana Dar es Salam tu, zinaonekana Arusha, zinaonekana Mwanza na sababu zake za msingi hazieleweki. Kwa hiyo, kwenye baadhi ya maeneo mengine hayaeleweki. Lakini niliomba Serikali iliangalie kwa upana wake. Kuna Benki ya akina mama. Benki ya akina mama inaonekana zaidi Dar es Salaam na hakika kama Benki ya akina mama ingepelekwa katika maeneo mengi ingeweza kuwasaidia akina mama, kwa sababu akina mama ndio wanaoshiriki katika nguvu kazi zaidi ya uchumi. Benki ya Vijana bado imekuwa hadithi, na vijana wengi wanahitaji kupata mikopo ili iweze kuwasaidia katika kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunazungumza mara nyingi kuhusu Benki ya Wakulima lakini imekuwa ni hadithi. Ni mwaka wa pili sasa hivi, toka tumeanza kuzungumza suala la kuanzisha Benki ya Kilimo lakini mpaka leo Benki ya Kilimo haijaanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tunataka tuwakomoe wananchi walio wengi ambao wanalima, na asilimia kubwa wako vijijini, Benki hii ianzishwe haraka zaidi na hela zipelekwe huko kwa wananchi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatokana sana na Serikali kuchelewa kufanya maamuzi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Jambo hili kama tutachelewa kuchelewa kufanya maamuzi mbalimbali katika shughuli za kiuchumi, Taifa letu litakuwa linaendelea kupata hasara hasa kwenye miradi mikubwa. Miradi unapochelewa kufanya maamuzi matokeo yake inapanda, ilikuwa na thamani ndogo, baadae unapokuja kutoa maamuzi miradi inakuwa imehama kutoka kwenye thamani ndogo kwenda kwenye thamani kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nililokuwa nataka kuzungumzia ambalo wachangiaji wengi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA]

wamezungumzia, lililozungumzwa na Mheshimiwa Rajab, Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Mpina, ni suala la *dollarization*. Tanzania ni nchi ya ajabu. nchi nyingi duniani zinaheshimu utaratibu wa hela yake lakini sisi Tanzania tunaonekana watu wa ajabu, hela yetu inaonekana haina thamani kuliko hela za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatakiwa tuliangalie kwa upana wake. Sasa hivi sisi kama Bunge Tukufu tulisimamie jambo hili, Serikali isiendeele kuruhusu matumizi ya *dollarization*, tuifanye Shilingi yetu iendele kupata thamani na iendeele kupata heshima katika dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la *Bureau De Change*. Tumekuwa na *Bureau De Change* nyingi ambazo hazifuati taratibu na Sheria, matokeo yake kumekuwa na vichaka vingi. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie katika eneo hili ili vile vichaka vingi ambavyo vinatumika kusafirisha hela haramu visitumike tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa Serikali itoe Leseni ya *Money Transfer*. Kwa kutokutoa Leseni ya *Money Transfer*, *Bureau De Change* zinatumia mwanya huo wa kusafirisha hela haramu na matokeo yake ni kwamba Serikali inapoteza hela nyingi ambazo ingepata kwenye kodi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukaimu katika baadhi ya Taasisi kwa muda mrefu, mfano Chuo cha Mipango, *Brella*, *SIDO* na kadhalka, imekuwa ndiyo tabia. Kwa hiyo, viongozi wengi wanashindwa kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu liangalie jambo hili, na Serikali ilifanyie kazi mapema iwezekanavyo kusudi tuwape nguvu wale Watendaji Wakuu katika maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililozungumzwa na Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Khatib Said Haji, ni msongamano wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA]

mizigo Bandarini. Dar es Salaam imeanzisha *one stop centre*, kwa kiasi fulani imesaidia kupunguza mlundikano wa mizigo Bandarini. Lakini jambo hili lingeenda hadi Tunduma na Hororo, nina hakika kabisa msongamano wa mizigo usingekuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashine za kutoa risiti kwa wafanyabiashara, suala hili limezungumzwa na Mheshimiwa Zitto, limezungumzwa sana na Mheshimiwa Gekul, hata Mheshimiwa Chilolo amezungumza jambo hili. Ni kweli kwamba kwa kuwepo kwa mashine hii kunasaidia ufanisi. Lakini bado Waheshimiwa Wabunge wanakuwa wana-*doubt*, hivi mashine zinaingiaje hapa nchini? Ziliingia kwa utaratibu upi? Kamati yangu iliomba iundwe Tume kwa ajili ya kuangalia uhalali wa upatikanaji wa hizi mashine. Hatukatai, tumeona kwa *some extent* zinasaidia, lakini lazima kuwe na vitu vya msingi vya kuweza kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwijage amezungumzia suala la vipimo na mizani. Hili jambo ni kweli, lina matatizo, nafikiri Mheshimiwa Dkt. Kigoda amelisikia, ataiagiza Tasisi yake ambayo inashughulikia mizani na vipimo ishughulikie jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni deni la Taifa. Sasa hivi deni la Taifa limefikia asilimia 43 tumebakiza 3% tu kuwa deni haliwezi kuhimilika. Ni vyema sasa hivi Serikali kabla haijakopa, ilete mpango mzima kwenye Bunge lako Tukufu ili tuweze kujua kwamba hizo hela zinakopwa kwa ajili ya kufanya shughuli gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Serikali kuchelewa kulipa fidia. Kumekuwa na ucheleweshaji ambao haueleweki wa kutokulipa fidia kwenye baadhi ya maeneo. Kwa mfano, eneo la *Kurasini Logistics Centre*. Mradi huu ulikuwa unatugarimu Shilingi bilioni 60 lakini kwa sababu ya kuchelewa kulipa fidia wale watu, sasa hivi imefikia Shilingi bilioni 94. Hii ni hasara kubwa sana kwa Serikali. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilianganalie jambo hili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA]

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni *Bagamoyo Min tiger EPZ*, nalo limechukua muda mrefu kutolipa fidia, na sasa hivi eneo hili limeshafikia Shilingi bilioni 48 Serikali inazidi kupata hasara kwa kuchelewa kulipa fidia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Mchuchuma na Liganga kama alivyoeleza Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, nalo linatakiwa lilipwe fidia, lakini Serikali inaendelea kusuasua katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lililozungumziwa ni urasimu katika kufanya biashara na uwekezaji. Eneo hili limezungumziwa sana na Mheshimiwa Dkt. Hamis Kidangwalla kwamba *TAC* na *TRA* wamekuwa wanapishana katika maamuzi. *TAC* wanakuwa wametoa misamaha lakini ukifika kule *TRA* watu wanakuwa hawakusikilizi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye kazi kama wamoja, iwe na *team* moja. Kama kutakuwa na mambo ya kupishana pishana kwa kweli nina uhakika urasimu wa kufanya biashara katika nchi yetu utaendelea kuwa mgumu zaidi. *Cost of doing business* katika nchi yetu imekuwa mgumu ukilinganisha na nchi nyingine ambazo zimetuzunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa matatizo makubwa yaliopo katika uchumi ni kutokuwa na umeme wa uhakika. Tumekuwa na umeme wa ubabaishaji, na haya ni matatizo makubwa. Umeme ambao tunatumia sasa hivi ni gharama, tunanunua kwa senti 43. Kama tungeamua kwa dhati, tungejjelekeza katika maeneo ya makaa ya mawe, hakika tungenunua umeme kwa senti 10. Tungepunguza *cost of production* na matokeo yake tungepunguza mfumuko mzima wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa hakuna maamuzi yanayoeleweka hasa hasa kwenye umeme wa upepo wa Singida ambao ungeweza kuzalisha umeme wa Megawatt 120. Wenzetu wako tayari kusaidia katika hili, lakini Serikali inashindwa kutoa maamuzi. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA]

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la Bima. Serikali inatakiwa ijiangalie kwa upana wake. Serikali inasisitiza sana eneo la Bima lakini Serikali yenyewe haijawahi kukata Bima kwa ajili ya nyumba zake, wala haijawahi kukata Bima kwa ajili ya magari yake. Ni vyema sasa kwa Serikali kuangalia eneo hili na waamue kukata Bima. Kutokukata Bima Serikali inapata hasara kubwa sana katika eneo hili. Magari mengi ya Serikali yanaibiwa, magari mengi ya Serikali yanapata ajali, na yakishapata ajali hakuna sehemu ya kufidia. Nyumba nyingi za Serikali zinaungua katika utaratibu ambao haujulikani na matokeo yake Serikali inaendelea kupata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kulikuwa na suala la Mifuko ya Jamii kwa wakulima. Mheshimiwa Zitto amelizungumzia sana jambo hili, nami namuunga mkono. Serikali iangalie ya namna ya kuwasaidia wakulima waweze kuingia kwenye Mifuko ya Jamii isaidie kiasi fulani ili wakulima waweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba niwasilishe maazimio yafuatayo ili Bunge lako Tukufu liweze kutoa maazimio.

- (i) Serikali ihakikishe inalipa fidia haraka iwezekanavyo kwa wadau wote wa Kurasini ili kupisha ujenzi wa *EPZ Kurasini Logistic Centre*; (*Makofi*)
- (ii) Serikali ihakikishe inalipa fidia kwa wadai wote wa Bagamoyo kupisha ujenzi wa *EPZ Bagamoyo Min Tiger*; (*Makofi*)
- (iii) Serikali ihakikishe upatikanaji wa umeme wa uhakika;
- (iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge liwe sehemu ya kuhakiki na kuishauri Serikali kabla haijakopa ili kudhibiti ukuaji wa deni la Taifa; (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA]

- (v) Kudhibiti matumizi holela ya Dola za fedha na fedha nyingine za kigeni ili Shilingi yetu iendelee kupata thamani katika nchi yetu na duniani kote; *(Makofi)*
- (vi) Nafasi zote zinazokaimiwa zijazwe haraka sana, wapewe watu wenye uwezo na sifa bila upendeleo wowote; *(Makofi)*
- (vii) Benki Kuu ifanye kazi yake kama Benki mama (*Bank of the other Bank*) kwa mabanki mengine kwa kutoa maelekezo kwa Benki zote kufungua matawi Wilayani kwa Watanzania wengi na pia kusimamia ipasavyo riba inayoongezeka bila tija; *(Makofi)*
- (viii) Benki Kuu isimamie ipasavyo *Bureau De Change*...

*(Hapa kengele iliia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Hitimisha sasa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sema hoja yenyewe.

MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja ya maazimio ya Kamati yangu. *(Makofi)*

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Kicheko)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla sijawahoji, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwanza.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati kwa taarifa hiyo, isipokuwa nataka kuweka taarifa sahihi kwamba deni la Taifa kwa takwimu za *IMF* ambazo tumefanya na Wizara ya fedha Septemba, 2013 *present value* ya deni ya Taifa ni asilimia 19. Ukomo wetu ni asilimia 50. *19% present value* tutafanya na ukomo wetu ni asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hilo kuliweka sahihi ili tupate *record* sahihi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana Serikali imekuwa ikitoa takwimu ni asilimia 19 ya deni ya Taifa, lakini haiuambii Umma kwamba hiyo asilimia 19 ni deni la Taifa kwa *ratio* ya mauzo nje, wanatoa *external debt* kwa *GDP*. Hawatoi *total public debt* kwa *GDP*. *Total public debt* kwa *GDP* hivi sasa imefikia asilimia 51, imeshavuka asilimia 50. Anachokizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri ni *external debt per GDP* ndiyo hiyo asilimia 19 anayoizungumza.

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, yuko sahihi katika upande huo. Haya mtayamaliza kwenye Kamati na baadaye mtatuweka vizuri Bunge.

Alichofanya Mheshimiwa Mgimwa ni kutuomba sisi Bunge kwamba tupokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara pamoja na Mapendekezo na Maoni ambayo ameyasoma pale kwenye taarifa yao. Naomba sasa niwahoji Waheshimiwa Wabunge.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara pamoja na Mapendekezo na Maoni yake yaliridhiwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, taarifa hii ya Kamati imepitishwa rasmi na Bunge. Nawatakia kila heri Kamati na nawapongeza kwa kazi kubwa na muhimu ambayo mmekuwa mkifanya, mwendeleo kufanya kwa niaba yetu, lakini vilevile nazipongeza Wizara zote ambazo zinafanya kazi na Kamati hii, tunazitakia kila la heri katika mwaka ujao, tunaamini mwakani zitakuja taarifa ambazo ni bora zaidi.

Kwa vile muda wetu ni mdogo, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Ukimwi - Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Kwa vile Waheshimiwa Mawaziri wamejaribu kujibu baadhi ya mambo, nakuomba ujitahidi kutumia dakika 15.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI - MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote waliochangia katika hoja ambayo ilikuwa imewasilishwa na Kamati yangu na napenda pia nitambue wale waliochangia kwa maandishi akiwepo Mheshimiwa Leticia Nyerere na Mheshimiwa Kombo kwa sababu wao hawakuzungumza. Lakini nawashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Lukuvi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa ufafanuzi mzuri walioutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukimwi upo. Naomba nianze kusema kwamba Ukimwi upo na lazima Watanzania na sisi viongozi tusimame imara kupambana na janga hili. Naomba niseme kwamba mimi mwaka 2002 nilipata nafasi ya kuwa katika *team* ya viongozi 12 Barani Afrika walioteuliwa na Umoja wa Mataifa kwenda kukutana na Mzee wetu, Marehemu Mzee Nelson Mandela kujadili tatizo la Ukimwi na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI]

tatizo kubwa la watoto yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu. (*Makofi*)

Naomba niseme kwa ufupi maneno aliyoyasema. Alisema, viongozi wote wa Afrika tuliungana katika kutafuta uhuru na ukombozi wa Afrika na Afrika ikawa huru. Leo viongozi wa Afrika tunatakiwa tuungane kupambana na Ukimwi na kusaidia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu. Kama hatutafanya hivyo, Afrika tunayoiacha itakuwa ya viongozi gani ambao ni watoto waliotelewa kwenye shida? Mwisho wa hayo, ninayoyazungumza nimezungumza kwa ufupi. Sasa huo ndiyo msimamo na tumeona viongozi wetu hapa nchini wakiwa mstari wa mbele na Bunge hili pia liko mstari wa mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Mfuko wa Ukimwi. Yeyote anayekusaidia anapenda uanze wewe mwenyewe, hata harusi unaanza kujichangia mwenyewe, mtu mwingine ndio anaanza kukuchangia. Kwa hiyo, suala la Mfuko wa Ukimwi nashukuru kwamba Serikali iko tayari kuleta mabadiliko ya sheria Bunge ilijalo tuweze kupitisha katika bajeti ijayo ili tuwe na chombo chetu wenyewe ili kiweze kutusaidia. Vile vile mjue kwamba Watanzania waliowekwa kwenye dawa, watatumia hizo dawa mpaka mwisho wao wa maisha. Kwa hiyo, ina maana kwamba ni lazima tuwawekee utaratibu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumziwa ni suala la wavuvi. Katika taarifa yetu tumezungumza kwamba Mkoa wa Mara, Mikoa ya Ziwa Victoria na Mikoa yote ambayo ina maeneo ya uvuvi, program maalum iundwe. Kwenye hili tulizungumzia pia Wizara ya Afrika Mashariki kuangalia program ambazo ziko katika program ambazo zinaendeshwa katika Mikoa inayozunguka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limezungumzwa la matumizi ya *condom*. Napenda niseme kwamba nchi yoyote ambayo imefanikiwa katika mapambano dhidi ya Ukimwi ina matumizi makubwa sana ya *condom*. Maana yake ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI]

kwamba tujue kwamba vijana wetu tunatakiwa tuwape kila aina ya elimu, lakini pia tuwape nyezo za kuweza kujikinga. Kwa hiyo, nakubaliana na wale waliosema kwamba *condom* zipatikane kila sehemu na hasa maeneo ya vijijini na hata mahotelini.

Nakubaliana pia na hoja inayosema kwamba hata kwenye vinywaji, kwenye maji ya chupa tuweke alama ya *ribbon* nyekundu inayoonesha mshikamano dhidi ya vita ya Ukimwi na hii itasaidia pia watoto wetu kuweza kupata elimu na kujua toka wakiwa wadogo. Tunatakiwa pia tualinde wanawake na wasichana. Wanawake na wasichana ni waathirika wakubwa ambao wamepata maambukizi lakini pia hawana maamuzi, tunatakiwa elimu ianze toka mashuleni.

Kuhusu kudhibiti maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, nakubaliana kabisa na maoni yaliyotolewa na kwamba elimu ianze kutolewa kwa akina mama wote na akina baba wote au tuseme jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madawa ya kulevya, naomba nichukue nafasi hii kuwataarifu Watanzania wote na Wabunge wenzangu kwamba Tanzania imesifiwa kuwa nchi ya kwanza Barani Afrika kuweza kusaidia vijana wetu ambao wanatumia dawa za kulevya kuacha, kwa kutumia dawa ya *Methodone* na lazima tujivunie chetu. Taifa letu limekuwa la kwanza. Pia Tanzania imekuwa ya kwanza Barani Afrika katika kusimamia na kusaidia vijana ambao wameacha kujidunga sindano. Kwa hiyo, hii imetolewa hata kwenye Mkutano ambao tulikuwa Afrika ya Kusini. Lazima tujivunie mafanikio makubwa ambayo yamefanywa na nchi yetu na sasa hivi nchi zote zinakuja kujifunza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala lingine ambalo tumezungumza kuhusiana na kuweza kuhakikisha kwamba tohara inatolewa kwa wanaume maeneo yote siyo Mkoa wa Njombe peke yake, lakini pamoja na Mikoa ambayo haifanyi tohara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI]

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulizungumza kwamba uwekwe mkakati maalum sikupata jibu kutoka kwa Mawaziri kuhusu mkakati maalum wa Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa ili kupunguza maambukizi. Nafikiri pia hili linahitaji tupate viwanda ili tuweze kuwa na shughuli za kujitegemea na tuweze kuachana na shughuli ambazo zinatupelekea kupata maambukizi. Naomba Serikali hilo iweze kulijibu, mkakati maalum wa Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Njombe na Mkoa mingine ambayo ina maambukizi makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu umenipa dakika chache nahofia usije kunigongea kengele kabla sijamaliza, nimepata maoni ya Wajumbe wengine hapa wakipinga matumizi ya *condom* akiwemo Mheshimiwa Kombo. Naomba nimwambie kwamba vijana wetu, kama sisi viongozi ni lazima tuwe tayari kuzungumza mambo magumu manufaa ya Watanzania na kwa manufaa ya watoto wetu na kizazi kijacho, bila kujali kwamba mimi simo, lakini kwa niaba ya waliotuleta hapa, tutakuwa tayari kuzungumza matumizi ya *condom* kama vijana wetu yanaweza kuwasaidia katika kupunguza maambukizi kwa sababu kuna njia tatu. Kuna njia ya kuacha kabisa, hulazimishwi kutumia *condom*, kuna njia pia ya kuwa mwaminifu, lakini ukishindwa unaruhusiwa kutumia kinga na kinga ni matumizi ya *condom* yaliyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako liweze kukubali mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ambayo ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa UKIMWI ambao unatakiwa uanze katika bajeti ijayo, 2013/2014.

Naomba pia nitoe mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwamba elimu ya Ukimwi iendeleo kutolewa na matumizi ya *condom* yahimizwe na upatikanaji wake uwepo. Naomba pia nitoe mapendekezo kwamba Serikali iharakishe mchakato wa kutunga sheria mpya ya kuzuia na kupambana na dawa za kulevya na kwamba Serikali iharakishe mchakato wa kuunda chombo maalum kitakachoshughulikia masuala ya dawa za kulevya. Pia tatizo la dawa za kulevya liweze pia kutangazwa kama janga la kitaifa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kwa niaba ya wanawake wote Tanzania, maana ndiyo watumia huduma, niishukuru Wizara ya Afya kupitia kwa Waziri wa Afya, kutoa magari ya wagonjwa na magari katika hospitali mbalimbali nchini ukiwemo Mkoa wa Iringa, Njombe, Ludewa, kwa sababu tunajua watumiaji wakubwa wa huduma hizi ni wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee majadiliano tuliyojadili na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI - Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ni Mwenyekiti ambaye ametusaidia sana Kitaifa na Kimataifa katika kulisemea jambo hili la janga la Ukimwi na pia ni Mwenyekiti Chama cha Wabunge cha kupambana na masuala haya ya UKIMWI (*TAPAC*). Tunakushukuru sana kwa mchango na kwa jinsi ulivyohitimisha hoja yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mng'ong'o ametuomba tupokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika taarifa hiyo. Naomba sasa niwahoji.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI
pamoja na Mapendekezona Maoni yaliyomo
katika taarifa hiyo iliridhiwa na Bunge)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU SPIKA: Wote wameafiki. Nawashukuru sana na kuwapongeza tena Kamati ya UKIMWI kwa ujumla ya masuala ya UKIMWI kwa kazi kubwa ambayo mmekuwa mkifanya. Kamati hii inafanya kazi katika Wizara zote, Idara zote za Serikali kwa sababu jambo hili ni mtambuka, wana kazi kubwa sana. Tunawatakia kila la kheri katika kazi hiyo, msikate tama, jambo hili kubwa mno mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tuzoe kusikia lugha za wenzetu wa Kamati hii kwa sababu katika jambo hili wao wanaamini na kwa kweli ni kweli kwamba ni vizuri kidogo kuwa wazi ili kuweza kufika safari yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Kabla sijamaliza masuala yaliyoko hapa Mezani nirudie tu kutoa ufafanuzi kidogo kuhusu mwongozo ambao ulitolewa wakati ule, lakini kwa sababu hatukuwa na muda nikasema niuweke mwisho, nikasema tu kwa utani kidogo, lakini sasa niuweke mwisho mwongozo wa Mheshimiwa Wenje kuhusiana na mchango wa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

Kwa wale ambao mlikuwepo Mheshimiwa Rajab ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC alizungumzia wakati Kamati ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa ikitoa taarifa yake hapa ndani kwamba kulikuwa na fedha kama Shilingi bilioni 2.3 ambazo zilikuwa hazijatumiwa na Halmashauri ya Nzega kwa muda wa mwaka mmoja. Kwa hiyo, alikuwa anatoa wito kwa Halmashauri ile kuzipangia matumizi vizuri fedha hizo. Kwa hiyo, kama Mwenyekiti wa LAAC, hakuwa amekosea chochote katika kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kigwangalla ameamua kulizungumza jambo hilo leo. Leo ni siku ambayo Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara inasimamia pamoja na mambo mengine masuala ya uwekezaji na uwezeshaji, yale ya Mheshimiwa Mama Nagu. Alichokuwa anafafanua ni kwamba wao wamekubaliana katika Halmashauri yao kwamba watazitemia fedha hizo kama ni sehemu ya uwekezaji na kwa maana hiyo uwezeshaji wa watu wao kwa kuanzisha Benki mpya ya watu wa Nzega. Hakusema jana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKAI]

kwenye Wizara nyingine, wala hatasema kesho kwenye Wizara nyingine. Amesema kwenye maeneo ya uwekezaji kwa madhumuni ya matumizi ya fedha hizo. (Makofi)

Kwa hiyo, nani amekosea? Hayupo aliyekosea. Lakini Mheshimiwa Wenje anasimama anasema wewe Spika ni dhaifu, wewe ndio tatizo, ukikaa hapo ndiyo unasababisha migogoro. Jamani, tuheshimiane nchi hii. (Makofi)

Wale mliokuja juzi, tufahamiane CV zetu zikoje? Hizi dharau za kirahisi rahisi siyo jambo zuri sana. Inasononesha kidogo! Kuna tabia fulani ambazo, yaani hivi kweli wananchi wa Nyamagana wanaweza kukutuma wewe uje unitukane mimi Mbunge wa Dodoma hapa? Siyo sawasawa hata kidogo! Wakikusikia wapigakura wako ambao ni watani zangu mimi hawawezi kufurahi. Yako mambo unaweza ukanifanyia hapa ukasahau kwamba wewe ni Mbunge wa kuchaguliwa, unatengeneza tatizo ambalo halina sababu. (Makofi)

Wale ambao wamesoma historia ya Mheshimiwa Mandela kwenye vitabu vyake vya nyuma huko, mimi nakumbuka zamani kidogo niliwahi kusoma. Wakati fulani akipigania uhuru wa *South Africa*, akawa anatafutwa, wakati huo wakimwita *black pimpernal* akawa amejificha kule Devonian kwenye *ranch* mojawapo, anafanya kazi za *organization* ya *ANC* na mkondo wa enzi hizo na nini, usiku. Mchana anafanya kazi katika shamba moja la mifugo nadhani kama kibarua katika kujificha. Kama kibarua hivi, mchana, lakini usiku wanafanya shughuli zao zile nyingine. Kwenye shamba lile kuna vibarua. Wale vibarua wa mashamba wanahesabika kama ni watu wa hali ya chini, wale *day workers*. Sasa mchana anapowagawia kama ni uji, kama ni chai, kama ni nini, wale vibarua hawamheshimu, maana yake hawamjui maana yake anaji-*disguise*. Hawajui kama huyu ni nani. Anapowagawia chakula na nini wanavyomwita mle hawana hata nidhamu, wewe, lete chakula hapa, nini, unajua Waswahili walivyo.

Sasa yeye anapigania Waswahili na haki zao, anaona Waswahili wasivyomthamini yeye kama binadamu, kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

sababu yeye sasa ni mhudumu wao, lakini hawajui kama ni nani, akapata tatizo sana kwamba mimi napigania haki za hawa, wao hawajui hata haki za wenzao. (*Makofi*)

Sasa sisi Wabunge tunapigania haki za Watanzania, tunawasemea. Lakini sisi kwa sisi hatujui hata kuthaminiana, wala kuheshimiana hatujui, yaani ukisimama wewe unaropoka tu. Basi na ukitoka kwa sababu kuna magazeti ambayo yako tayari kuandika kesho na tuna mitandao ambayo iko tayari kuandika fulani ni shujaa kwa kuropoka kwake, *and then we will continue*, siyo sawa. Hili jambo siyo sawa hata kidogo. Tuheshimiane, litatufikisha mbali kama Taifa.

Sisi waafrika tuna upungufu huo sana wa kutokuheshimiana. Yaani tunatazamana kwa dharau. Nawe unayedharau wenzako, ulichonacho siyo lolote zaidi ya *wrong empowerment*. Yaani umekuwa *empowered wrongly* tu. Kwa hiyo, unadhani labda una elimu ya kutosha au sijui una nini, *it is a wrong empowerment*. Kwa hiyo, unadharau watu, unatukana watu, unadhaliisha watu, *and you go away with it* kwa sababu kanuni zetu zilitarajia kwamba Bunge hili ni la watu wa wastaarabu. Kwa hiyo, hazina namna ya kushughulika na watu ambao wako chini ya kile kiwango. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa shughuli za leo tumekamilisha shughuli zetu, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.39 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 18 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)